# WAHUSIKA WA KIMIMI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA *DUNIA YAO* NA *NYUSO ZA MWANAMKE*

**HAJI BAKAR ALI**

**SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**

**OKTOBA, 2018**

# WAHUSIKA WA KIMIMI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI:

# MIFANO KUTOKA *DUNIA YAO* NA *NYUSO ZA MWANAMKE*

NA

HAJI BAKAR ALI

TASNIFU KWA AJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA

UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA DODOMA

OKTOBA, 2018

# IKIRARI

# NA

# HAKIMILIKI

Mimi **Haji Bakar Ali** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi; na kwamba, haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

**Saini**……………………………..

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo: **Wahusika wa Kimimi katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kukamilisha mahitaji ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili.

...........................................

Dkt. Rashid Chuachua

(Msimamizi)

Tarehe: ......................................

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, kabla sijasema neno lolote, napenda nitoe shukrani zangu zisizo na ukomo kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu, Yeye, ndiye Mkuu; na anayepaswa kushukuriwa kwa hatua yoyote ya maisha ya mwanadamu. Ninamshukuru kwa kunijaalia afya njema, kunipa nguvu, uwezo, akili, busara na maarifakatika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Nasema kwa unyenyekevu, Mungu ndiye muweza wa kila kitu.

Pili, nawashukuru sana wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunifunza kuhusu ulimwengu. Vile vile, shukrani za pekee ni kwa mke wangu kipenzi na watoto wangu kwa uvumilivu wao, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa.

Tatu, napenda kumshukuru kwa dhati Msimamizi wangu Dkt. Rashid Chuachua kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili. Sina neno linalofaa kutoa shukrani zangu kwake, bali namuombea afya njema na maisha marefu, ili aendelee kutoa msada wa kitaaluma kwa wanafunzi wanaohitaji maarifa zaidi.

Nne, napenda kuwashukuru wote walioshiriki katika utafiti huu kwa njia moja au nyingine; pamoja na, ushirikiano walionipa kipindi chote cha kufanya utafiti huu. Nitakuwa mchache wa fadhila nisipotoa shukrani zangu kwa walimu wote walionifunza Kiswahili katika viwango tofauti.

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa baba yangu mpenzi, Bakar Ali Hamd. Baba leo shuhudia mafanikio yangu! Kwa kunilea na kunipa taaluma hadi kufikia hapa nilipo.

Kwa mama yangu mpenzi Marehemu Bi. Bahati Shaame Hamad. Mama natamani leo hii ningekuwa pamoja nawe. Mungu akulaze salama. Amin.

# IKISIRI

Utafuti huu ulilenga kuchunguza wahusika wa Kimimi katika riwaya za Said Ahmed Mohamed kwa kujikita katika miktadha ya utokeaji wa wahusika hao, namna wahusika wanavyojikengeusha na jamii; na sababu za wahusika kujikengeusha. Matumizi ya wahusika wa Kimimi hayajachunguzwa vya kutosha. Yumkini, hali hii inasababisha kutokufahamika miongoni mwa wasomaji na wahakiki wa kazi za fasihi. Kazi tulizozipigia mbizi kwa kina katika kuchunguza wahusika wa Kimimi ni riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*.

Utafiti ulifanyika maktabani. Maeneo yaliyotumika kukusanyia data ni Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Zanzibar. Hakuna data yoyote ya kitakwimu iliyotumika katika utafiti huu, bali tulitumia mbinu ya ufafanuzi. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mkabala wa kisaikochanganuzi ambapo uchambuzi ulifanyika kwa mbinu ya ufafanuzi.

Matokeo yanaonesha kuwa, riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* zimetumia miktadha ya chimbuko la kifasihi, kisiasa, shereheni, kazini, kifamilia, mahakamani na mitaani.Pia, wahusika wamejikengeusha kwa kugomea chakula, kutojali, ukivuli, kutokata tamaa, kushiriki ngono, usasa, ulevi na uongozi bora. Sababu za wahusika kujikengeusha ni ukosefu wa ajira, utandawazi, ukombozi wa mwanamke, siasa, utamaduni, habari na mawasiliano na usomi. Utafiti uliongozwa na mkabala wa Saikochanganuzi.Mchango mpya ulioibuliwa na utafiti huu katika taaluma ya fasihi ni huu. Mosi, kuibuliwa kwa miktadha ambayo wahusika wa Kimimi wamesawiriwa katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Pili, Kufafanuliwa sababu za wahusika kujikengeusha na jamii. Tatu, kuibuliwa kwa sababu za wahusika kujikengeusha ambazo ni ukombozi, siasa, utamaduni na usomi.

**YALIYOMO**

IKIRARINAHAKIMILIKI ... i
ITHIBATI ... ii
SHUKRANI ... iii
TABARUKU ... iv
IKISIRI ... v
YALIYOMO ... vi
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ... ix

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ... 1**
1.1 Ufafanuzi wa Istilahi ... 1
1.1.1 Riwaya ... 1
1.1.2 Ukengeushi ... 1
1.1.3 Wahusika ... 1
1.1.4 Nafsi ... 2
1.1.5 Utamaduni ... 2
1.1.6 Maadili ... 2
1.1.7 Muktadha ... 2
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ... 3
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ... 6
1.4 Malengo ya Utafiti ... 7
1.4.1 Lengo la Jumla ... 7
1.4.2 Malengo Mahsusi ... 7
1.5 Maswali ya Utafiti ... 7
1.6 Manufaa ya Utafiti ... 7
1.7 Mkabala wa Uchanganuzi wa Data ... 8
1.8 Historia ya Said Ahmed Mohamed ... 11
1.9 Dhana ya Riwaya ... 12
1.10 Maelezo kuhusu Riwaya Teule ... 17
1.10.1 Dunia Yao ... 17
1.10.2 Nyuso za Mwanamke ... 17
1.11 Hitimisho ... 18

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ................................................... 19**
2.1 Utangulizi ........................................................................................ 19
2.2 Dhana ya Wahusika.......................................................................... 19
2.2.1 Aina za Wahusika ........................................................................ 20
2.2.2 Mhusika Mimi ............................................................................. 21
2.3 Dhana ya Ukengeushi ..................................................................... 22
2.3.1Aina za Ukengeushi ....................................................................... 22
2.4 Mapitio kuhusu Wahusika katika Fasihi ya Kiswahili....................... 23
2.5 Mapengo yanayojitokeza ................................................................. 26
2.6 Hitimisho.......................................................................................... 26

**SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI........................................ 28**
3.1 Utangulizi ........................................................................................ 28
3.2 Usanifu wa Utafiti ........................................................................... 28
3.3 Eneo la Utafiti ................................................................................. 28
3.4 Walengwa wa Utafiti........................................................................ 29
3.5 Wango Tafitiwa................................................................................. 29
3.6 Sampuli ya Watafitiwa ...................................................................... 29
3.7 Njia na Zana za Ukusanyaji wa Data ............................................... 29
3.7.1 Mbinu ya Mapitio ya Maandiko...................................................... 30
3.7.2 Zana/Vifaa vya Utafiti. .................................................................. 30
3.8 Uchambuzi wa Data ......................................................................... 30
3.9 Itikeli za Utafiti ............................................................................... 31
3.10 Uthabiti na Uhalali wa Data ........................................................... 31
3.11 Hitimisho........................................................................................ 32

**SURA YA NNE: MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI........................... 33**
4.1 Utangulizi ........................................................................................ 33
4.2 Miktadha ya Wahusika wa Kimimi katika Riwaya Teule .................. 33
4.2.1 Miktadha ya Chimbuko la fasihi .................................................... 34
4.2.2 Miktadha ya Kisiasa ....................................................................... 37
4.2.3 Miktadha ya Shereheni.................................................................... 39
4.2.4 Miktadha ya Kazini ........................................................................ 41
4.2.5 Miktadha ya Kifamilia ................................................................... 43

4.2.6 Miktadha ya Mahakamani ........ 44
4.2.7 Miktadha ya Mitaani ........ 45
4.3 Hitimisho ........ 48
4.4 Upekee wa Wahusika wa kimimi katika Kujikengeusha na Jamii katika Riwaya Teule ........ 49
4.4.1 Kugomea Chakula ........ 50
4.4.2 Kuonesha Kutojali ........ 52
4.4.3 Matumizi ya mhusika kivuli ........ 55
4.4.4 Kutokata Tamaa ........ 58
4.4.5 Mijadala ya Nadharia kuhusu Imani ........ 60
4.4.6 Kushiriki Ngono ........ 63
4.4.7 Kupenda Usasa ........ 65
4.4.8 Kutumia Ulevi ........ 66
4.4.9 Uongozi Mbaya ........ 67
4.4.10 Kukithiri kwa Utabaka ........ 69
4.5 Hitimisho ........ 71
4.6 Sababu za Wahusika Kujikengeusha katika Riwaya Teule ........ 73
4.6.1 Ukosefu wa Ajira ........ 73
4.6.2 Athari za Utandawazi ........ 74
4.6.3 Ukombozi wa Mwanamke ........ 76
4.6.4 Changamoto za kisiasa ........ 79
4.6.5 Utamaduni wa kigeni ........ 81
4.6.6 Habari na Mawasiliano ........ 83
4.6.7 Matukio ya Usomi ........ 84
4.7 Hitimisho ........ 87
4.8 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 87

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 89**
5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 89
5.2 Hitimisho ........ 94
5.3 Mapendekezo ........ 95
**MAREJELEO ........ 97**
**VIAMBATISHO ........ 100**

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Braza la Kiswahili Zanzibar |
| Bi | Bibi |
| Bw | Bwana |
| CD | *Compact Disk* |
| DVD | *Digital Vessetile Disk* |
| FM | *Frequency Modelution* |
| Khj | Kama hapo juu |
| MA | *Master of Art* |
| PhD | *Doctor of Phyilosophy* |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

Sura hii inaeleza utangulizi wa jumla wa utafiti huu. Sura inaanza kwa kufafanua dhana za msingi zilizotumika. Aidha, kuna usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, mkabala wa utafiti, historia ya mwandishi, dhana ya riwaya, pamoja na maelezo kuhusu riwaya teule.

## 1.1 Ufafanuzi wa Istilahi

Sehemu hii inafafanua dhana muhimu zinazohusiana na utafiti huu. Dhana hizo ni riwaya, ukengeushi, wahusika, nafsi, utamaduni, maadili na muktadha.

### 1.1.1 Riwaya

Mulokozi (1996: 149) anasema kuwa, riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika na matukio yanayosukwa kimantiki yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi.

### 1.1.2 Ukengeushi

Mayaka (1991:27) akimnukuu Wanjala (1980) anasema kuwa, ukengeushi una maana ya mtengo au mbanduko au kuhisi ugeni.

### 1.1.3 Wahusika

Ndugo na Mwai (1991: 160) wanadai kuwa, wahusika ni watu au hata viumbe vilivyochorwa na mwandishi kisanii ili kuwakilisha watu anaowafikiria katika kazi yake.

### 1.1.4 Nafsi

Wikimedia Foundation (2013) wanasema kuwa, nafsi ni neno la mkopo kutoka Kiarabu. Linatumika kusisitiza dhati ya mtu (Mfano, "Mimi nafsi yangu"). Hivyo, linatumika kutafsiria neno la Kilatini "*persona*" (kwa Kiingereza "*person*") ambalo linamtofautisha binadamu (kama kiumbe wa pekee) na wanyama wote na kumpa haki zake za msingi. Nafsi ni kitu fulani kisichoonekana na kisichoweza kufa ambacho kimo ndani ya miili ya wanaadamu.

### 1.1.5 Utamaduni

Kroeber na Kluckhohn (1952) wanasema kuwa, utamaduni ni jinsi binadamu anavyoyakabili maisha katika mazingira yake. Hivyo, inajumuisha ujuzi, imani, sanaa, maadili, sheria na desturi ambavyo mtu anajipatia kama mwanajamii.

### 1.1.6 Maadili

BAKIZA (2010:213) wanalifafanua neno maadili kuwa, ni mwenendo unaokubalika katika jamii fulani.Ambapo kwa mtafiti, neno maadili lina maana pana na linaweza kuvuka kiwango cha jamii. Kwa mfano, tunawezakusema maadili ya Watanzania ni wadogo kuwaheshimu wakubwa lakini si jamii zote kama zinafanya hivyo, na hii ni kutokana na kuwapo kwa suala zima laitikeli za jamii fulani.

### 1.1.7 Muktadha

Muktadha ni hali, wakati jambo linapofanyika au panapohusika (BAKIZA, 2010). Hivyo kwa mujibu wa utafiti huu, neno muktadha limetumika kuonesha mahali au mazingira ambayo yanaonesha tendo fulani limetokea au limetendeka.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Dhana ya wahusika imekuwa ikiangaliwa na kuelezwa kwa mitazamo tofauti na wataalamu wa fasihi. Wahusika katika kazi ya fasihi ni miongoni mwa kipengele cha kifani kinachowakilisha tabia mbalimbali za wanadamu. Wahusika wa kazi ya fasihi wanaweza kuwa watu, wanyama au viumbe vyovyote vyenye uhai na visivyokuwa na uhai, vililivyokusudiwa kuwakilisha tabia za watu.

Salim (2015:03) akimnukuu Zanji (1986), anasema kuwa, riwaya nyingi za mwanzo zilitumia wahusika binadamu na wanyama. Sababu kuu ya kutumia wahusika wanyama ni kuwa, fasihi simulizi ni njia ya kuelezea na kutawala matukio ya mara kwa mara katika jamii na mazingira yao. Mawazo hayo ya Zanji yanaonyesha kuwa, hali hii ndiyo iliyosababisha waandishi wengi kutumia wahusika wa fasihi simulizi katika riwaya za mwanzo za Kiswahili, kama za Shaaban Robert, ili kusawiri mazingira yaliyoizunguka jamii. Katika historia ya fasihi ya Kiswahili tunaona kuwa, mnamo miaka ya themanini (1980), wahusika wa aina tofauti, hasa binadamu walianza kujitokeza ndani ya riwaya za Kiswahili. Kipindi hiki kilishuhudia wahusika changamani katika fasihi andishi ya Kiswahili, hasa riwaya na tamthiliya.

Hatahivyo, Madumulla (2009) anaonesha aina za wahusika wanaopatikana leo hii katika fasihi ya Kiswahili. Ameainisha aina tofauti za wahusika, ambazo ni mhusika wa kimapinduzi, mhusika wa kisaikolojia, mhusika wa kitenzi (mkwezwa), mhusika wa kidhanaishi na mhusika wa kijumui (Mhusika Mimi), huyu anaelezwa kuwa na tabia yawahusika wengi katika mmoja.Vilevile, Madumulla (K.h.j) anasema kuwa, mhusika wa kijumui ameletwa na Kezilahabi kwa mara ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili, anajitokeza katika kitabu cha *Nagona* (1990), ambapo mhusika “Mimi” anao *Id, Ego* na *Superego* ndani yake. Pia, anaendelea kusema kuwa, mhusika huyu

ni wa kifalsafa. Madai hayo ya Madumula yakwamba, Kezilahabi ndiye wa mwanzo kuleta wahusika wa Kimimi, kwa kiasi fulani mtafiti anaona ni telezi. Hii inatokanana ukweli kwamba, hata Said Ahmed alitumia mhusika huyu katika riwaya ya *Dunia Yao* ambayo ni ya mwanzo kuliko *Nagona* na *Mzingile.*

Pamoja na hayo, Madumulla (Khj) anaendelea kufafanua kuwa, mhusika Mimi aliletwa na Kezilahabi katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* kama majaribio. Ambapo, anamsawiri mhusika huyo kama shujaa na mwanamapinduzi anayejitolea kwa hali na mali katika kuitetea jamii yake. Akiunga mkono hoja hiyo, Nyenye (2011) anadai kuwa, Kezilahabi anamchora mhusika Mimi katika riwaya yake ya *Mzingile* akiwa safarini tokea mwanzo hadi mwisho wa riwaya.Hata hivyo, watafitiwengi walioshughulikia suala la wahusika hawajaonekana wakikitupia jicho kipengele hiki cha wahusika wa Kimimi hususani, katika riwaya za Said Ahmed Mohamed, mwandishi ambaye ndiye chaguo la mtafiti katika utafiti huu.

Kwa hivyo, tumeona kuwa, tatizo la upungufu wa tafiti zinazohusiana na wahusika wa Kimimi katika riwaya ya Kiswahili, linaweza kusababisha kuwapo kwa kazi za kifasihi zilizokosa mvuto fulani wa kifasihi na kuonekana kama hazijakamilika, jambo ambalo linaweza kumpotezea mtunzi hadhira yake. Pamoja na hayo, watafiti tarajali wanaweza kupoteza mielekeo ya kazi zao kwa kukosa mahali pa kurejelea. Hivyo, utafiti huu umebainisha wahusika wa Kimimi katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka katika *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*, zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed.

Aidha, tumeamua kumchagua mwandishi huyu kutokana na ubobevu alionao katika uandishi wa riwaya za Kiswahili, kwani, ni dhahiri kwamba, tunapojiuliza

kuhusubaba wa fasihi ya Kiswahili, basi jibu lisilo na shaka, bila kupepesa macho litakuwa ni Said Ahmed Mohamed. Hivyo, ipo haja ya kumuenzi mwandishi huyu kwa kuendelea kumtafiti zaidi, ili kumtangaza zaidi katika uga huu wa fasihi ya Kiswahili, na kumfanya afahamike siku hadi siku kwa kizazi kilichopo na kijacho hususani, katika jamii ya Waswahili na riwaya yake. Hii inatokana na ukweli kwamba, mwandishi huyu ameandika kazi za Kiswahili katika tanzu zote kama vile Riwaya, tamthilia nyinginezo. Inasadikiwa kuwa, hadi sasa mwandishi huyu ameshaandika kazi zaidi ya hamsini zilizochapishwa.Mfano: *Asali Chungu Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Amezid (1995 ), Nyuso za Mwanamke (2010), Mashetani Wamerudi (2016) na nyingine nyingi. (1977),Utengano (1980 ), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990),*

Hivyo, kutokana na uwezo mkubwa wa kuweza kuandika kazi zake katika mazingira na nyakati tofauti, ni miongoni mwa sababu zilizomshawishi mtafiti wa kazi hii kuweza kumtafiti mwandishi huyu, kwani, aliandika riwaya zake katika kipindi cha baada ya uhuru na kuonekana zinaendana na wakati tulionao.

Aidha, Njogu na Wafula (2007) wamekwenda mbali zaidi, katika kuzungumzia dhana ya umimi wanasema kuwa, umimi ndio humwezesha mtoto (mhusika) kutambua utu wake na ubinafsi wake. Pia, wanaendelea kusema kuwa, mtoto (mhusika) akiwa tumboni mwa mama yake, kiwiliwili chake huwa sehemu na kimelea cha mwili wa mama yake, lakini, akishazaliwa hali ya ukengeushi hutokea kwa sababu ubinafsi wake huanza kudhihirika. Ubinafsi wa mtoto hujibainisha kwa kuanza kujirejelea kama “Mimi”.

Ukengeushi wa wahusika na umimi unaoelezwa na wachambuzi wa kazi za fasihi, kuhusu usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi hususani, zile za Said Ahmed, ndio ulioamsha ari kwa mtafiti  kutafiti riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*zote za Said Ahmed Mohamed, ili kuona namna mtunzi huyo alivyomsawiri mhusika wa Kimimi katika kusanii kazi zake.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wachunguzi na wahakiki kadhaa wameshughulikia maandishi ya Said Ahmed Mohamed; lakini, kwa kiasi kikubwa uchunguzi wao umejikita katika maudhui (Wamitila 1999; Walibora 2010;Wanyonyi 2011; Ann 2013;Khamis 2014; na Mapunjo 2014). Hatahivyo, katika fani, watafiti na wahakiki wengi wamegusia baadhi ya vipengele na kukiambaa kipengele hiki cha wahusika wa Kimimi.

Hii inadhihirisha wazi kuwa, suala la miktadha, ukengeushi wa wahusika na sababu za ukengeushi wa wahusika, kama kipengele kimoja wapo katika kazi hizo hakijashughulikiwa vyakutosha na wahakiki pamoja na watafiti wa kazi za fasihi. Yumkini, hali hii imezua matatizo makubwa kwa wasomaji wa kazi za mwandishi huyu, na kazi nyingine za fasihi kwa sababu, usomaji wa maandiko mbalimbali ya kifasihi, huhitaji uwezo mkubwa wa kutumia nyanja za utambuzi na uelekeo katika kuhusisha mambo yadhihirikayo katika kazi ya fasihi dhidi ya tabia na hisia binafsi za mtunzi. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuziba pengo lililobainishwa hapo juu, kwa kuchunguza Wahusika wa Kimimi katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Dunia Yao* na*Nyuso za Mwanamke* za Said Ahmed Mohamed.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

### 1.4.1 Lengo la Jumla

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza wahusika wanaobeba dhana ya umimi kama inavyojitokeza katika riwaya teule za Said Ahmed Mohammed.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

i) Kubainisha miktadha ambayo wahusika wa kimimi wamechorwa katika riwaya teule za Said Ahmed Mohammed.

ii) Kufafanua upekee wa wahusika wa kimimi katika kujikengeusha kwao na jamii.

iii) Kutathmini sababu za wahusika wa kimimi kujikengeusha katika jamii iliyochorwa na mtunzi.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Miktadha ipi ambayo wahusika wa umimi wamesawiriwa katika riwaya teule za Said Ahmed Mohammed?

ii) Kuna upekee gani kwa wahusika hao katika kujikengeusha kwao na jamii?

iii) Kwa nini wahusika wa kimimi hujikengeusha katika jamii iliyochorwa na mtunzi?

## 1.6 Manufaa ya Utafiti

Utafiti huu una tija mbalimbali, ambazo miongoni mwazo ni kama zifuatazo:

Kwanza, kujua miktadha mbalimbali ambayo wahusika wa umimi wamesawiriwa katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*, zote za Said Ahmed Mohamed. Pili, kuona upekee wa wahusika hao na jinsi wanavyojikengeusha katika jamii zao. Tatu, utafiti huu unataja sababu za wahusika wa umimi kujikengeusha katika jamii zao. Nne, ni msaada tosha kwa watafiti wajao kufanya tafiti zaidi kuhusu mambo mbalimbali yaliyokuwa hayajashughulikiwa na mtafiti.

## 1.7 Mkabala wa Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu uliongozwa na mkabala waSaikochanganuzi katika uchanganuzi wa data. Nadharia hiyo ilichaguliwa na mtafiti baada ya kutathmini na kugundua kwamba, ingemuwezesha kufikia hitimisho la utafiti huu.

Adam (2014), akimnukuu Wamitila (2002a), anaeleza kuwa, Nadharia ya Saikochanganuzi iliasisiwa na mtaalamu mwenye asili ya Australia, aliyejuilikana kwa jina la Sigmund Freud. Mwanataaluma huyu alitumia neno (*Psychoanalysis*) lenye maana ya saikochanganuzi kwa mara ya kwanza katika mwaka 1896. Vilevile, Adam (2014:58), akimnukuu Freud (1896), anaendelea kusema kuwa, binadamu huongozwa na mambo makuu matatu, ambayo ni mahitaji, matamanio na wasiwasi katika maisha.

Mahitaji hurejelea mambo muhimu kama chakula, malazi na mavazi, ambayo humwezesha mwanadamu kuishi vizuri. Matamanio hurejelea dhana ya starehe hususani, za kingono. Wasiwasi ni hofu na mashaka juu ya maisha, kwamba, nitafanikiwa au sitafanikiwa katika maisha.

Naye, Wamitila (2002), akimnukuu Freud (1896), anaeleza kuwa, kati ya mambo matatu makuu ambayo huongoza maisha ya mwanadamu, ni lile la matamanio ndilo hutawala zaidi. Matamanio huchukuwa nafasi kubwa katika maisha ya mwanadamu; kwa hivyo, kila mwanadamu hufanya jitihada kubwa kuhakikisha anatimiza matamanio yake, katika harakati za kuhakikisha kwamba, huumiza watu wengine wasio na hatia.

Pia, Adam (Khj) anamnukuu Freud (Khj), akisema kwamba, matamanio yamekuwa ni kitu muhimu kwa binadamu kwa sababu tangu mwanadamu huyu anapozaliwa tu,

anaanza kupata raha ya kujamiiana kwa kunyonya kwa mama yake. Anaeleza kwamba, chuchu za mama huwa ni kama uume na mdomo wa mtoto ni uke. Kwa hiyo, mtoto anaponyonya kwa mama yake anapata raha ya kijinsia. Hivyo basi, mtoto anavyoendelea kukua, hitajio la kujamiiana nalo linakuwa kubwa zaidi na hufanya kila njia kuhakikisha kwamba, anatimiza hitajio hilo.

Vilevile, Said (2015) anamnukuu Wright (1997) akiifafanua nadharia hii kwa kusema;

> *Psychoanalysis is a system of psychological theory and therapy which aim to treat mental disorders by investigating the interaction of conscious and unconscious elements in the mind and bringing repressed fears and conflicts into the conscious mind by techniques such as dream interpretation and free association (uk.145).*
>
> Saikochanganuzi ni mfumo wa nadharia wa kisaikolojia na tiba wenye malengo ya kutibu watu wenye matatizo ya akili kwa kuchunguza mwingiliano wa mambo katika hali ya urazini na usorazini katika ubongo; nakufichua matatizo na kuyaweka bayana kwa kutumia mbinu kama vile ya kufasiri ndoto na uhuru wa kififkra katika kufanya maamuzi (Tafsiri yangu).

Kwa mujibu wa Wright, kama alivyonukuliwa na Said (Khj), Saikochanganuzi ni jina lililokopwa na Freud mwaka 1896, alipobadili mbinu yake ya matibabu. Anaendelea kusema kwamba, Saikochanganuzi inachunguza mambo ya zamani, ili kupata mambo ya sasa. Aligundua kwamba, masimulizi yanafungamana na elementi za kibunilizi, ingawa alikuwa anashughulikia matukio ya kweli ya kihistoria.

Aidha, anaendelea kusema kuwa, hii ni kwa sababu, kumbukumbu zinaibua hisia ambazo hazipo katika ung’amuzi tambuzi kwa wakati huo. Kwa hivyo, maana inapatikana baada ya kutafsiri tukio kwa msaada wa bunilizi. Saikochanganuzi ina mitazamo mikuu mitatu, ambayo inaweza kutumika kuchunguza matukio kupitia bunilizi. Mitazamo hiyo ni kama vile; njia ya kudadisi nafsi ya mtu, mitazamo

pangilifu kuhusu tabia za mwanadamu na njia za kutibu magonjwa ya kisaikolojia au mihemko.

Freud, mwanasaikochanganuzi maarufu alibainisha njia kadhaa za uchambuzi wa kazi za fasihi kwa kutumia unafsia, yaani Saikochanganuzi. Alibainisha mitazamo au njia nne za uchambuzi wa kazi za fasihi ambazo ni kuangalia:

Kwanza, nafsi ya mwandishi, ambapo, anamuona mwandishi kama muotaji ndoto. Mwandishi anapoandika huwa anakusudia kukuambia ukweli alionao ndani yake, uliofichama muda mrefu. Pili, unafsia wa msomaji, msomaji anapoisoma kazi ya fasihi anajiona mwenyewe ndani ya kazi hiyo, jambo ambalo linampa msukumo wa kutaka kuendelea kuisoma zaidi, ili apate maana tukio linalomuhusu. Tatu, unafsia wa andiko; anaona kwamba, maandishi si mafu bali yanazungumza na msomaji.

Mwandishi anaweza akawa amekufa miaka mingi, lakini maandishi yake bado yapo na yana athari kubwa kwa wanajamii. Nne, unafsia wa wahusika; katika hatua hii, mtu anaposoma kazi ya fasihi anakutana na wahusika ambao anawachambua kwa kuangalia mambo yafuatayo:

i) Maisha yao tangu mwanzo hadi mwisho.

ii) Mawazo ya mhusika juu ya maisha kwa jumla.

iii) Uhusiano wa mhusika mmoja na wahusika wengine.

iv) Jinsi wahusika wengine wanavyomuhukumu mhusika mwenzao.

v) Kutoa hitimisho kwa kulinganisha mambo ya wahusika na jamii.

Aidha, kama tulivyobainisha hapo juu, kuhusu msingi wa nne wa unafsia wa wahusika katika mkabala wa saikochanganuzi; na mambo ya kuzingatia yanayoambatana na msingi huo, mjadala wa uchanganuzi na uwasilishaji wa data

umezingatia viambata vya msingi huo.Kwa jumla, tulichagua mkabala wa Saikochanganuzi ulitusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuchambua data zilizokusanywa kuhusu wahusika.

## 1.8 Historia ya Said Ahmed Mohamed

SaidAhmedMohamedalizaliwaUnguja,mnamotarehe 12/12/194.AlisomashuleyaMsingi Darajani na Sekondari Gulioni,nakuendeleanamasomo ya Chuo chaUalimu cha Nkrumah Zanzibar, mwaka1966. Mwaka 1976, mwandishi alijiungana Chuo Kikuucha Dar es Salaam kusomeaShahadayakwanzaya Ualimu katika Isimu na Fasihi ya Kiswahili; na baadayamiaka mitatu, alisomea Shahada ya Uzamili katika Isimu Tekelezi Chuoni hapo (Juma, 2016).

Aidha, kutokana na umahiri na uwezo mkubwa alionao, alipata fursa ya kuelekea Ujerumani, ili kufanya Shahada ya Uzamivu (PhD), katika Chuo Kikuu cha Karl Marx- Leipzig, mwishonimwa mwaka1981, na kukamilisha mwaka1985.

Anaendelea kusema kuwa, Said amewahi kufundisha Shule ya Sekondari Kizimbani na Utaani, kati ya mwaka 1969 na 1974. Pia, aliwahi kufundisha katika shule ya Hamamni kwa muda wa miaka mitatu, na Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI) miaka miwili. Mnamo mwaka 1987, alikwenda Kenya na kubahatika kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi, mjini Aldoreti, na baadae alifundisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi hadi mwaka 1990, alipotoka Nairobi alielekea Japan katika Chuo Kikuu cha Osaka- Idara ya Lugha za Kigeni, na ndipo alipopata Uprofesa.

Aidha, alipotoka Japani, alikwenda kufundisha Chuo Kikuu cha Bayreuth, kuanzia mwaka 1997 hadi kustafu kwake mwaka 2012. Kwa sasa, Profesa Said baada ya kustaafu amerudi nyumbani kwake, Limbani Wete Pemba kwa mapunziko, na kuendeleza kazi yake ya uandishi. Aidha, akiwa Zanzibar, anaendelea kufundisha katika Chuo Kikuu cha Zanzibar ngazi ya Uzamili (MA). Kwa upande wa familia, Profesa ana mke na watoto wawili, mwanamke na mwanamme. Mwanamke anaitwa Najma na wakiume anaitwa Mahir.

Juma (khj) anamalizia kwa kusema kuwa, kwa upande wa uandishi na ubunifu wa fasihi, msanii huyu amekuwa mwandishi mashuhuri na gwiji kwa uandishi na ustadi wa fani mbalimbali, kama vile riwaya, tamthiliya, ushairi, hadithi fupi, kazi za watoto, na uandishi wa vitabu vya Shule na Vyuo. Tayari ameshaandika vitabu zaidi ya hamsini na tano, miongoni mwa kazi alizoandika ni pamoaja na;*Asali Chungu(1977),Utengano(1980 ), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990), Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Amezid (1995 ), Nyuso za Mwanamke (2010) na Mashetani Wamerudi (2016).*

**1.9 Dhana ya Riwaya**

Maana ya riwaya imetolewa na wataalamu mbalimbali wakifanana katika baadhi ya vipengele na kutofautiana katika mambo yanayounda riwaya ya Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu walioandika kuhusu dhana ya riwaya ni Nkwera (1978), pale aliposema, riwaya ni hadithi iliyo ndefu kuweza kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi. Ni hadithi ya kubuniwa iliyojengwa juu ya tukio la kihistoria na kuandikwa kwa mtindo wa lugha ya mfululizo na ya kinaganaga katika kuelezea maisha ya mtu au watu na hata Taifa.

Riwaya huwa ina mhusika mmoja au hata wawili. Maana ya riwaya inayotolewa na Nkwera (khj) inatufahamisha kwamba, riwaya ni hadithi ndefu, jambo ambalo tunakubaliana nalo kwa kiasi fulani tu, kwani suala la urefu au ufupi haliwezi kuikosesha sifa riwaya na isiitwe riwaya tena. Riwaya ni hadithi ndefu ambapo kutokana na urefu huo, huifanya kuwa tafauti na hadithi fupi, ushairi na tamthilia. Urefu wa riwaya huifanya kueleza mambo kwa kina, kiasi cha kumfanya msomaji kuelewa kisa, tukio au matukio mbalimbali yanayoelezwa katika riwaya husika. Kiasili, neno “Riwaya” lina maana ya taarifa iliyokamilika hasa katika masuala ya dini ya Kiislamu (Sengo, 2014).

Jambo jingine ambalo tumejifunza juu ya maana ya riwaya hapo juu, ni kuwapo kwa lugha au mtindo wa kishairi. Hapa tunafahamishwa kwamba, riwaya huweza kuandikwa kwa kutumia mitindo mingi na sio lazima ule wa nathari, ambao ndiwo uliozoeleka na watunzi wengi wa riwaya ya Kiswahili. Aidha, jambo jingine ambalo tunakubaliana na Nkwera (khj) kwa kiasi fulani, ni kuhusu wahusika wa riwaya. Yeye anadai kuwa, mhusika mmoja au hata wawili wanaweza kuunda riwaya. Hapa tunakubaliana naye kwa kuzingatia juu ya kuwapo kwa riwaya za kiwasifu na zile za kitawasifu, ambazo hazibebi wahusika wengi. Kwa hakika, riwaya ni utungo ambao hueleza mambo mengi kama alivyoeleza Nkwera mwenyewe.

Aidha, Mlacha na Madumulla (1991) wanasema kwamba, riwaya huwa inawahusika wengi ambapo kunakuwa na mhusika mkuu na wahusika wadogo au wasaidizi, ambao kazi yao kuu ni kumpamba mhusika mkuu aweze kukamilisha lengo la mtunzi. Maelezo ya Mlacha na Madumulla (khj), yanaonekena kuwa na mashiko ya kitaaluma zaidi kuhusu idadi ya wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

Vilevile, wataalamu wengine walioandika kuhusu maana ya riwaya ni Muhando na Balisidya (1976). Wao wanasema kwamba, riwaya ni kazi ya kubuni, ni hadithi ambayo hutungwa kufuatana na uwezo wa fanani kuibua mambo kutokana na mazoea au mazingira yake. Riwaya yaweza kuanzia maneno 35000 hivi na kuendelea, lakini tukisema juu ya urefu na tukaishia hapo hapo tu, jambo hili halitakuwa na maana. Maana mtu yeyote aweza kuweka habari yoyote ile na kuiweka katika wingi wa maneno kama hayo. Jambo muhimu hapa ni kuwa, riwaya huwa na uchangamani wa matukio, ujenzi wa wahusika na dhamira, muundo wake na hata mtindo maalumu.

Mhando na Balisidya (khj), wamekwenda mbali zaidi na kutaja hata idadi ya maneno ambayo inatakiwa kuiunda riwaya. Wanasema kwamba, riwaya inaweza kuwa na maneno kuanzia 35000 na kuendelea. Bila shaka, maneno haya ni mengi. Kwa maoni yetu, riwaya inaweza pia, kuwa na maneno chini ya hayo na bado ikaitwa riwaya. Jambo la msingi ni kwamba, riwaya hiyo sharti iwe na maudhui na hicho kinachoelezwa, kielezwe kwa ufundi na ufanisi.

Naye, Senkoro (1977), anasema riwaya ni kisa ambacho ni kirefu vya kutosha, chenye zaidi ya tukio moja ndani yake. Ni kisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani kwa mambo mbalimbali ya kimaudhui na kiufundi. Riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu na kutamba mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo mwandishi wake.

Maelezo ya wataalamu hawa juu ya riwaya yana umuhimu sana kwetu, kwa sababu wametueleza mambo ya msingi hususani, juu ya kwamba, riwaya hutungwa

kulingana na uwezo wa fanani, hivyo, tumeyatumia katika kufanikisha utafiti wetu. Hii ina maana kwamba, mtunzi wa riwaya hutunga riwaya yake kwa hadhira maalumu, na si kila mtu anaweza kuwa hadhira wa riwaya. Hivyo, maelezo hayo yanaungwa mkono na Kezilahabi (1983:235) pale anaposema:

> Hivi sasa hatuwezi kusema kuwa kuna riwaya ya Kiswahili ambayo haieleweki kabisa kwa watu; ingawadalili zakuanza kuandika riwaya na hadithi fupi zisizoeleweka kwa urahisi zimeanza kuonekana. Jambo ambalo ningependa kuonya hapa ni kuwa, mwandishi wa riwaya, asisukumwe kuandika riwaya kwa ajili ya watoto wa shule. Riwaya si kitabu cha kiada na si cha ziada. Mwandishi wa riwaya si mtu wa kufugwa, lakini si mtu anayeweza kuruhusiwa kusema chochote kile anachotaka awe hana mipaka.

Maelezo haya yanaonesha, mtunzi wa riwaya anayo fursa ya kuandikia riwaya kwa hadhira fulani ambayo yeye anataka kuiandika, na isiwe rahisi riwaya hiyo kueleweka kwa kila hadhira. Pamoja na kuonesha kwamba, mtunzi wa riwaya anao uhuru wa kuandika riwaya yake vile anavyotaka, bado ana mipaka ya kiuandishi. Kauli kwamba, “mwandishi aandike anachotaka awe hana mipaka” inamfanya mwandishi aende mbali zaidi na awe huru katika kuonesha kipaji chake. Mwandishi yeyote hutawaliwa na ujumi, ubunifu, usanii na lengo kuu la hazina ya jamii yake, ambamo yeye hupewa fursa ya kuchota kiasi cha kumtosha kwa ridhaa na kwa niaba ya hiyo jamii kuu. Mradi mwandishi ni zao la jamii; kufungwa kwake ni katika kutii mafunzo ya jamii, ili asipate mikasa ya adhabu za ulimwengu.

Akijadili dhana ya riwaya, Wamitila (2003), anasema kwamba, riwaya ni kazi ya kinathari na kibuniliziambayo huwa na urefu wa kutosha msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina, yenye kuchukua muda mwingi katika maandalizi yake na kukitwa katika mandhari muafaka. Maelezo haya ya Wamitila hayatafautiani sana na ya wataalamu wenzake.

Yeye, anatufunza jambo moja muhimu katika taaluma ya riwaya, nalo ni lile la wahusika, matukio na dhamira kuwa, ni lazima kukubalika na mandhari. Muktadha na Mandhari husaidia kumfanya msomaji ayapate maudhui kwa urahisi kwa vile yanavyoendana na fikra za jamii hiyo ya riwaya. Mandhari ni miongoni mwa vipengele vya fani katika kazi ya fasihi. Ujuzi wa matumizi ya mandhari katika kazi za fasihi hutegemea uhodari wa mwandishi.

Hatahivyo, Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa, riwaya ni utungo mrefu wa kubuni, na wenye ploti, uliotumia lugha ya nathari. Lakini ploti ni nini? Ploti inahusu maingiliano na mazuano ya vitushi. Yaani, ploti ni jinsi vitushi katika kazi ya sanaa vinavyoingiliana na kuzuana. Maana hii ya riwaya haitofautiani sana na zile zilizotolewa na wataalamu wengine ambao tumewaona hapo juu. Badala yake, wataalamu hawa wawili, wametuletea misamiati mipya lakini inarejelea mambo yale yale yaliyokwisha kuelezwa na wataalamu watangulizi. Misamiati hiyo ni “vitushi” ukiwa na maana ya visa na matukio, na “ploti” ikiwa na maana ya muundo.

Mulokozi (1996) anashadidia kwamba, ili kuifahamu vizuri maana ya riwaya, ni vyema kuzingatia mambo kadhaa, kama vile, matumizi ya lugha ya kinathari, isawiri maisha ya jamii, iwe na masimulizi ya kubuni na visa virefu, wahusika zaidi ya mmoja, iwe na msuko na mpangilio wa visa na matukio, maneno zaidi ya 35000 na kuendelea, ifungamane na wakati, yaani visa na matukio vifungamane na wakati.

Kwa upande wake, Chuachua (2011), anafafanua kuwa; riwaya ni kazi ya kibunilizi ya kinathari yenye uchangamani wa fikra, msuko, mandhari na uhusika unaosawiri binadamu na maisha yake. Maana hii ya riwaya iliyotolewa na Chuachua, kwa kiasi kikubwa imetutoa uvuliuvuli na kutuondoshea ile dhana ya urefu au ufupi kama kigezo cha kuifanya ikubalike kama riwaya. Na hii inatufanya tutamatishe kwa kutoa fasili ya riwaya kuwa, ni utungo wa kinathari wenye kubeba visa na matukio

ya kibunifu, na yenye uchangamani wa mawazo ambayo huelezea maisha halisi ya binadamu hata kama imetumia wahusika wasio binadamu.

## 1.10 Maelezo kuhusu Riwaya Teule

### 1.10.1*Dunia Yao*

Riwaya hii iliandikwa na Said Ahmed Mohamed na kuchapishwa na kampuni ya uchapishaji ya*OxfordUniversity Press*, *East AfricaLtd*; Nairobi nchini Kenya, mwaka 2006. Ni miongoni mwa kazi zake ambazo zilimpatia umaarufu mkubwa katika tasnia hii ya uandishi. Riwaya hii inazungumzia mambo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa katika jamii za Waafrika na Tanzania ikiwamo.

Aidha, inazungumzia maswala ya utawala wa viongozi katika bara la Afrika, na jinsi wanavyokuwa wabadhirifu wa mali pindi wakiwa madarakani. Riwaya hii inamchora mhusika Yungi akiwakilisha wanawake wanaotaka kuasi utamaduni wao, kwa kuachiwa uhuru wa kufanya wanalolitaka bila kuulizwa chochote. Anajiingiza katika tabia zisizokubalika katika jamii ya Watanzania, kama vile, ulevi na umalaya. Jambo linalosababisha mgogoro mkubwa kati yake na baba yake na kumfanya baba yake ajitenge na familia yake. Kadhalika, riwaya ya *Dunia Yao* inazungumzia mambo ya kidhanaishi juu ya imani kwamba, baadhi ya wahusika wake, kama vile, Ndi au Ye au Mimi kuwa, wanapokea maono/ujumbe (*wahy*) kutoka kwa Mungu, ambaye ndiye anayewapa uwezo wa kutunga kazi zao za kifasihi.

### 1.10.2*Nyuso za Mwanamke*

Wanyoni (2015:1) anasema kwamba*Nyuso za Mwanamke* (2010) ni riwaya ya nane ya Said Ahmed Mohamed, mwandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili ya kisasa. *Nyuso za Mwanamke* ni riwaya ya kisaikolojia kwa sababu imeweka msisitizo mkubwa kwenye fikira na hisia za ndani za wahusika. Wanyoni (khj) anamnukuu

(Wamitila 2003: 181) akieleza kwamba, riwaya za aina hii mara nyingi hujihusisha na mawazo ya mhusika anayesumbuka kimawazo na kihisia. Hali ya kisaikolojia ya mhusika wa riwaya ya aina hii, hudhihirishwa na matukio ya kinjozi na ishara.

Vilevile, Wamitila (khj) anasema, riwaya hii inazungumzia masuala ya mitagusano ya kimaadili, kiuchumi, kijamii na kisiasa katika jamii ya Kisiwa cha Unguja. Kazi hii inazungumzia maisha ya Nana, msichana anayejikuta katika mivutano ya kifamilia, kijamii, kitamaduni, kidini na kinafsi, anayeathirika na kubebeshwa makosa yaliyofanywa na wazazi wake, hasa baba yake.

Aidha, riwaya ya*Nyuso za Mwanamke* inatudokezea “Nyuso" yaani taswira mbalimbali walizo nazo wanawake katika harakati za kudhulumiwa na kudhalilishwa na mfumo wa ubabedume. Inamsawiri mwanamke wa Kiafrika katika kipindi hiki cha utandawazi anayejaribu kujikwamua kutokana na minyororo ya kitamaduni.

**1.11 Hitimisho**

Sura hii imeelezea vpengele mbalmbali ambavyo baada ya utangulizi kumekuwa na ufafanuzi wa baadhi ya istilahi. Vile vile, usuli wa tatizo la utafti umeelezwa kwa kina huku ukifuatiwa na tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti na mkabala wa utafiti.

Aidha, historia ya mwandishi, dhana ya riwaya pamoja na maelezo kuhusu riwaya teule ambazo ni *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Aidha, maelezo ya sura hii ni wazi kwamba yanatoa dira kuhusu namna mtafiti wa kazi hii alivyolenga kufika mbali katika kufikia malengo yote ya utafiti. Sura inayofuata itaelezea maptio ya maandiko.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii kwa ujumla inajadili mapitio ya maandiko, lakini kwa kuanzia tumeanza kuelezea dhana ya wahusika, aina za wahusika, mhusika Mimi,dhana ya ukengeushi na aina zake pamoja na maandiko kuhusu wahusika katika Fasihi ya Kiswahili,na kumalizia na mapengo yaliyojitokeza baada ya kupitia maandiko mbalimbali.

## 2.2 Dhana ya Wahusika

Khamis (2014) anaizungumzia dhana ya wahusika kuwa, ni miongoni mwa vipengele muhimu sana katika kazi ya fasihi, hasa riwaya na tamthiliya. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, wahusika ndio nyenzo kuu katika matukio na matendo yanayopatikana ndani ya kazi husika. Kwa kawaida, wahusika hufungamanishwa na wajihi wao; tabia zao, wasifu wao na hata hisia zao. Maelezo haya yanadokeza taarifa muhimu kuhusu wahusika katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtafiti wa kazi hii aliyachukua mawazo hayo, ili kumsaidia katika kukusanya na kuchambua data; na hatimae, kufikia lengo la utafiti huu.

Naye, Wamitila (2002) anasema kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hao huwa sehemu ya kazi nzima. Aidha, anaendelea kusema kuwa, wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya fasihi na ambao wana sifa ya kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa; hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wahusika pia, huweza kutambulishwa na maelezo yao au msimulizi.

Maelezo ya Wamitila (khj) kuhusu dhana ya wahusika yameingia ndani zaidi, kuhusu uchambuzi wa namna ya kugundua uhusika wa wahusika katika fasihi. Hii

ina maana kwamba, mawazo hayo yameweka msingi imara kwa watafiti wa kazi za fasihi, hasa katika kipengele cha wahusika. Hivyo basi, katika utafiti huu, mawazo hayo yalitumika ili kuchunguza usawiri wa mhusika wa Kimimi katika riwaya teule.

### 2.2.1 Aina za Wahusika

Suala la uainishaji wa wahusika ni changamani miongoni mwa wataalamu wa kazi za fasihi. Hali hii, imesababisha kuwa na miainisho tofauti na idadi tafauti ya wahusika kati ya mtaalamu mmoja na mwingine. Uchangamani huu, kwa kiasi kikubwa husababishwa na vigezo vinavyotumika katika kuainisha wahusika.

Njogu na Chimerah katika Madumulla (2009:136-141), wameainisha wahusika kwa namna nne (4) tofauti. Namna ya kwanza, wameainisha wahusika kama vile, mhusika mkwezwa, mhusika wa kisaikolojia, mhusika wa kimapinduzi na mhusika jumui. Namna ya pili, kuna wahusika wakuu, wahusika wadogo na wahusika wajenzi. Wakati namna ya tatu, wameainisha wahusika wa miraba minne na wahusika wa mraba mmoja. Na namna ya nne, ni wahusika bapa, wahusika duara na wahusika shinda. Uainishaji huu, ni ule wa kijumla ambao wataalamu wengi huangukia tapo moja kati ya manne hayo.

Kadhalika, Khamis (2014:14) akimnukuu Senkoro (2011) anataja aina tatu za wahusika, ambao ni wahusika wakuu, wanaojitokeza mwanzo hadi mwisho wa kazi husika, wahusika wadogo, ambao husaidia kukamilisha dhamira ndogondogo na wahusika bapa, ambao hawakui kifikra wala kimatendo. Vilevile, Khamis (Khj), akimnukuu Senkoro (Khj), anaendelea kusema kuwa, mara kwa mara wahusika katika fasihi simulizi wanawakilisha pande kuu mbili; upande wa wema (haki) na upande wa ubaya (uonevu).

Anaongezea kwa kusema kuwa, sifa na majina ya wahusika hubaki kuwa, ni ileile tangu mwanzo hadi mwisho. Katolea mfano riwaya ya *Rosa Mistika* ya E. Kezilahabi ambayo anadai kuwa, majina ya wahusika wake yanawakilisha tabia zisizobadilika, tangu mwanzo hadi mwisho. Hatahivyo, mtafiti wa kazi hii hakubaliani na hoja hii, kwanai, anaona wahusika katika riwaya hiyo ya *Rosa Mistika*, wana tabia ya kubadilika na kujikengeusha na jamii yao, akiwamo Rosa mwenyewe.

Mjadala huu kuhusu aina za wahusika, umetupatia uelewa wa kina wa namna ya kuchunguza wahusika. Hivyo, mtafiti alichunguza miktadha ambayo wahusika wa Kimimi wamechorwa, ili kubaini upekee wa wahusika hao katika kujikengeusha kwao. Pia, alichunguza iwapo kuna sababu zozote za wahusika kuweza kujikengeusha, kwani, wahusika hao wamekuwa wakibadilikabadilika au wakibakia katika muelekeo mmoja wa matendo na tabia.

### 2.2.2 Mhusika Mimi

Njogu na Wafula (2007) wanasema kuwa, mhusika Mimi anajitambua yeye kama yeye, na huanza kudhihirisha umimi wake mara tu anapozaliwa. Akishadidia hilo, Madumulla (2009) anamzungumzia mhusika huyo kuwa, ni mwenye tabia za ubinafsi, anajipambanua kwa wengine na asiyependa kuburuzwa; wala kuingiliwa katika maamuzi yake.

Mjadala huu kuhusiana na mhusika Mimi, umetoa mwanga mkubwa kwa mtafiti wa kazi hii, hivyo, uliweza kumsaidia katika kutambua namna mhusika huyo anavyojengwa kitabia katika kazi za fasihi. Hii ni kusema kwamba, mawazo

hayoyalimfanya mtafiti aweze kukusanya data zinazohusiana na mhusika Mimi, na baadae kujibu maswali ya utafiti huu.

## 2.3 Dhana ya Ukengeushi

Mayaka (1991:27), akimnukuu Wanjala (1980), anadai kuwa, ukengeushi una maana ya mtengo au mbanduko. Anaendelea kusema kuwa, hali hii hutokea katika mahusiano mbalimbali katika jamii.Vilevile, imani kwa Mungu inaweza kuwa chanzo mahususi cha ukengeushi.Waumini wanaamini kuwa, sio wao watendao ila ni Mungu ndani yao. Mungu anapotenda ndani yao, wao hukaa kama mashine, isipofunguliwa haifanyi kazi, kuhusu dini anasema:

> Yeye si mtenda ila anachotenda ndani yake ni nguvu fulani nyingi sana ambazo hawezi na hastahili kushindana wala kupingana nazo. Hali yake nikama ya kikaragosi tu. Hivi basi, dini humkengeusha mtu na kazi yake, matendo yake yote, fikra na hata nafsi yake. Anatenda ila matendo si yake, anafanya kazi na hiyo kazi si yake, anafikiri fikra si zake, ana nafsi lakini nafsi hiyo si yake, ametenganishwa na uhalisia wote (uk. 30).

Dondoo hilo linatuonesha kuwa, dini ni miongoni mwa mambo ambayo yanaweza kusababisha kuwapo kwa ukengeushi katika jamii. Jambo ambalo lilimnufaisha mtafiti wa kazi hii, katika kujua sababu za wahusika wa Kimimi kujikengeusha kwao katika jamii. Hivyo, mtafiti alifaidika sana kupitia kazi hiyo, ili kuweza kuusukuma mbele utafiti wake.

### 2.3.1Aina za Ukengeushi

Mayaka (1991) anajaribu kufafanua aina mbili za ukengeushi, aina hizo ni Utamaushi na Kizindushi (*Alienation Effect*). Anasema kuwa, Utamaushi ni aina ya ukengeushi ambayo, miiko na maadili ya jamii ni lazima yafuatwe na wanajamii wote; na atakayekwenda kinyume, basi anaweza kufukuzwa au kutengwa na jamii hiyo. Kwa mfano, Mugala, katika *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Kizee huyo, alidaiwa kuwa ni mchawi na kuhamishiwa katika kisiwa kisichokuwa na watu.

Mayaka (Khj) anaendelea kusema kuwa, Kizindushi ni aina ya nyingine ya ukengeushi inayotumika katika uandishi wa michezo ya kuigiza. Anafafanua ya kwamba, mchezaji mmoja hujitenga na uchezaji na kuielezea hadhira yanayoendelea mchezoni ili kuizuia isizugike. Kwa mfano, Polly, katika tamthiliya ya Brecht, iitwayo *Man Equals Man and the Elephant Calf* (1979). Vilevile, katika tamthiliya ya *Mashetani* (1971), ya Ebrahim Hussein, Juma anajikengeusha kwa kuieleza hadhira wanayotarajia kuyaonesha katika uigizaji wao, Yeye (Juma) na Kitaru.

Maelezo haya, ni wazi kwamba, yametupatia uelewa wa kina kuhusu dhana ya ukengeushi na namna ukengeushi unavyoweza kujitokeza katika kazi za fasihi, na vipengele vya fasihi. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu uliyachukua mawazo haya, ili kuyatumia katika kumchunguza mhusika wa Kimimi katika kazi teule, ili kuona namna mhusika huyo anavyojikengeusha.

### 2.4 Mapitiokuhusu Wahusika katika Fasihi ya Kiswahili

Ann (2013:31) anaeleza kuwa, wahusika ni viumbe wa kibunilizi katika kazi za fasihi wanaotumiwa na mwandishi kuyaendeleza maudhui na kutimiza dhamira na malengo yake. Katika tasnifu yake iliyohusu Usasa wa mwanamke wa kisasa katika *Nyuso za Mwanamke*, anamchora mhusika kama mtu mwenye msimamo thabiti. Anamtolea mfano mhusika Nana, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na kusema kuwa:

> Nana kupitia elimu aliyojipa kwa kusoma matopa kwa matopa ya vitabu alikuja kung'amua kuwa binadamu hustahili kupewa nafasi ya kujiamulia mambo iwapo ni jambo linalomhusu kama ndoa. Alihisi ni vyema uamuzi wake uheshimiwe maana alikuwa na hisia kama wale waliomwamulia; kwanza Nana alihisi vibaya kuchukuliwa kwa gari kila siku...Aliona kuwa maisha kwake ni shuleni nyumbani au nyumbani shuleni. Jambo hili alilitafsiri kama utumwa na akataka uhuru wa kuachwa ajipeleke shuleni na ajirudishe. Kuonesha msimamo wake,

> aligoma kwenda shule na kula chakula, baba yake alipoona basi aliamuru apelekwe shuleni kwa gari na arudi kwa miguu (uk. 33).

Mawazo hayo ya Ann (khj), yalikuwa ni kichocheo kikubwa katika kusukuma mbele malengo ya utafiti huu. Hii inatokana na kuwa, mtafiti wa kazi hii naye alitumia riwaya hii ya *Nyuso za Mwanamke* katika kuchunguza wahusika wa Kimimi. Hivyo basi, msimamo thabiti wa mhusika Nana, kwetu sisi tuliweza kuutafsiri kama ndio umimi, jambo ambalo halikufanywa na Ann.Aidha, Salum (2013) akimnukuu Madumulla (1987) anaelezea kuwa, badiliko jingine ni mhusika kuwa na saikolojia na hisia. Kwa mfano, riwaya ya *Kichwamaji* (1974) inasawiri saikolojia za wahusika, kwa kuonesha wazazi wa Manase wanavyopingana na mtoto wao (Manase), anayeshikilia msimamo wa kumuoa mchumba wake aliyemchagua yeye mwenyewe na sio chaguo la wazazi wake.

Kitendo hicho cha migongano na mivutano kati ya Manase na wazazi wake ni dhahiri kinaashiria ukengeushi wa kifamilia. Hali hiyo, inasababisha kuwapo kwa “umimi”, ambapo mhusika Manase, moja kwa moja anabeba dhana hiyo ya “umimi”. Hivyo basi, utafiti wa Salum ulikuwa na faida sana katika utafiti wetu kwa sababu, ulitupatia uelewa wa namna ya kufafanua sababu za wahusika wa kimimi kujikengeusha katika jamii zaokatika kazi teule.

Kadhalika, John na Mkude (2011) wamefafanua kuhusu wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wanasema kuwa, kwa kawaida wahusika wadogo huchomoza hapa na pale; kisha huanza kutoweka kwa muda au kutoweka kabisa. Kwa mfano, mhusika maskini anaweza kupambanishwa na mhusika mkuu, ili kubainisha ukarimu au uchoyo wa mhusika mkuu, kisha mhusika maskini akawa haonekani tena.

Maelezo hayo, yalitusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuibua wahusika wenye kubeba dhana ya Umimi, pamoja na sababu za kujikengeusha kwa wahusika hao. Hii, ni kutokana na kitendo cha kujadiliwa kwa tabia ya ukarimu na uchoyo wa wahusika hao, na kutoonekana tena kwa baadhi ya wahusika.

Fauka ya hayo, Mayaka (1991) anaeleza kuwa Kezilahabi amesawiri wahusika wasomi, wasioleta matumaini yoyote katika jamii. Akishadidia hoja yake, anaendelea kusema kuwa, Kezilahabi amemuonesha msomi kama mwanajamii mwingine aliyekosa adabu, na aliyetengana na hata nafsi yake. Amewatolea mifano, Rosa Mistika, Kichwa Maji na Tumaini. Ambao ni wahusika wakuu waliokuwa wasomi katika riwaya hizo, walikata tamaa na hawakuleta tumaini katika jamii zao, bali ni maafa. Anahitimisha kwa kusema kuwa, hatma yao, waliamua kujiua kutokana na kukata tamaa katika maisha.

Maelezo hayo ya Mayaka (Khj) yalikuwa na msaada mkubwa katika kufanikisha utafiti huu, ambao unahusu wahusika wa Kimimi katika riwaya ya Kiswahili. Hii, inatokana na wahusika hao kujitenga na jamii yao mara baada ya kukata tamaa.

Pia, Mlacha (1985) anaeleza kuwa baadhi ya riwaya zimetumia wahusika wanyama, wanyama hao huwakilisha watu na matendo yao. Anazidi kufafanua, kwa kusema kuwa, aghalabu msanii huchunguza matendo na tabia za watu, baadaye huumba wahusika wenye kufanana na watu halisi katika jamii.

Mawazo hayo ya Mlacha (Khj) yalitusaidia katika kuuendea utafiti huu, kwani amejaribu kutaja matendo na tabia za wahusika katika kujinasibisha na watu halisi katika jamii zetu. Hivyo, ilikuwa chachu ya kufanya utafiti huu usonge mbele kwa kasi ya juu.

Hata hivyo, Madumulla (2009) anasema kuwa, wahusika ni watu au viumbe katika kazi ya fasihi waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu katika maisha halisi. Hivyo, katika riwaya, wahusika huwa ni halisi, wanaoendana kwa karibu sana na maisha ya kila siku, kwa sura yao, lugha yao na hulka yao kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo, mawazo hayo ya Mlacha (Khj), yaliweza kutoa msaada mkubwa katika utafiti huu, kwani yamegusa suala la hulka au tabia za wahusika pamoja na matendo na hata lugha zao. Hivyo, yalisukuma mbele mawanda ya utafiti huu ambao ulizamia katika kubainisha wahusika wa Kimimi katika riwaya ya Kiswahili.

Aidha, baada ya mtafiti kutalii maandiko tofauti yaliyoandikwa kuhusu dhana ya wahusika, aligundua bado hakuna utafiti wa kina uliofanyika kwa nia ya kuchunguza wahusika wa Kimimi katika riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* za Said Ahmed Mohamed, kwa mkabala wa Nadharia ya Saikochanganuzi.

### 2.5 Mapengo yanayojitokeza

Baada ya kupitia kwa kina maandiko yote hayo tumebaini kuwa, watafiti na wahakiki wengi wamezungumzia suala la wahusika, lakini hawajazungumzia kwa kina kuhusu wahusika wa Kimimi hususani, katika riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Jambo hili, ndilo lililomchochea mtafiti wa kazi hii kutaka kujua zaidi, sababu hasa za wahusika wa Kimimi kutaka kujikengeusha kwao na jamii; katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed.

### 2.6 Hitimisho

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko. Katika sehemu hii, dhana mbalimbali kuhusu wahusika zimeelezewa. Ambapo, baada ya utangulizi kumeelezewa dhana ya

wahusika kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, aina za wahusika pamoja na mhusika mimi. Ki msingi sura hii imetoa mwanga kuhusiana na aina mbalimbali za wahusika kwa mujibu wa wataalamu hao.

Aidha, dhana ya ukengeushi na aina zake zimejadiliwa kulingana na wataalamu tofauti. Mwisho ni mapitio kuhusu wahusika katika Fasihi ya Kiswahili pamoja na mapengo yaliyojitokeza katika utafiti huu ambapo mtafiti alibaini mapungufuyaliyoachwa na watafiti waliotangulia na kuziba mapungufu hayo kwa kuibuka na utafiti huu. Hivyo basi, sura inayofuata inahusu methodolojia ya utafiti.

# SURA YA TATU

# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua vipengele mbalimbali vya methodolojia ya utafiti kama vile, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, wango tafitiwa, sampuli ya watafitiwa, ukusanyaji wa data, njia za ukusanyaji wa data, mbinu ya mapitio ya maandiko, zana/vifaa vya utafiti, uchambuzi wa data na itikeli za utafiti.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Utafiti ulifanyika maktabani. Data zilikusanywa kutoka katika maandiko mbali mbali aliyoyaandika Said Ahmed Mohamed, pamoja na yale yaliyoandikwa na wataalamu wengine, ambayo yaliisukuma mbele mada yetu. Mbinu ya ufafanuzi/ uelezeaji wa jambo kwa kina ndiyo iliyoweza kutumiwa na mtafiti katika utoaji wa matokeo.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani. Hivyo basi,ulifanyika katika maktaba mbalimbali, kama vile; ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Sumait (CHUKWANI) na Chuo Kikuu cha Dodoma. Kadhalika, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tawi la Pemba, pamoja na makta kuu zilitumika katika utafiti huu.Kwa mantiki hiyo nikwamba, utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Unguja, Pemba na Dodoma.Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kwamba, utafiti huu ulilenga kupata machapisho yanayohusiana na utafiti wetu.

Hivyo, chaguo la maeneo ya utafiti huu, lilitokana na upatikanaji wa nyaraka mbalimbali zilizomuwezesha mtafiti kufikia malengo ya utafiti wake. Vilevile, kwa

kutumia maktaba na utulivu wa mazingira ya maktaba, mtafiti alipata nafasi ya kusoma matini mbalimbali za riwaya teule katika utafiti huu kwa utulivu wa kutosha, ilkiwa ni pamoja na vyanzo vya mitandaoni.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu ni riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* za Said Ahmed. Tumechagua riwaya hizo kwa sababu, tunaamini kuwa kuna matumizi ya mhusika wa Kimimi ndani yake. Hivyo, ni wazi kwamba riwaya hizo zilitoa majibu sahihi kwa kile kilichotarajiwa kutafitiwa.

### 3.5 Wango Tafitiwa

Wango lililohusiana na upatikanaji wa taarifa za utafiti huulilihusishaRiwaya mbalimbali zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed,  ambazo zilisaidia kuchunguza miktadha ambayo wahusika wa Kmimi wamechorwa ndani yake.

### 3.6 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli yautafiti huu ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa.

*Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010).Sampuli ya utafiti huu iliuundwa na

Riwaya za Said Ahmed Mohamed, ambazo ni *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010).

### 3.7 Njia na Zana za Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data katika utafiti huuulifanywa kwa kutumiambinu ya Mapitio ya Maandiko yaliyoandikwa na wataalamu mbalimbali, maandiko hayo ni kama vile vitabu, majarida, tasnifu na vyanzo vingine vya mitandaoni.

### 3.7.1 Mbinu ya Mapitio ya Maandiko

Mbinu hii iliambatana na usomaji na uchambuzi wa matini za riwaya teule. Mchakato huu ulifanyika ili kupata data zinazohusiana na wahusika wa Kimimi na namna wanavyojikengeusha. Vilevile, mbinu hii ilihusisha usomaji, uchambuzi na uchunguzi wa data katika vitabu, na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti huu, kama taarifa za kwenye mtandao, majarida, vitabu na machapisho mengine.

Pia, iliweza kumsaidia mtafiti katika kutoa ithibati juu ya data zilizokusanywa kwa maandiko. Vifaa vilivyotumika katika kufanikisha njia hii ni pamoja na vitabu mbalimbali, makala, tasnifu na majarida, iwe maktabani au katika sehemu nyingine yoyote ambayo ilisaidia katika kupatikana kwake. Hivyo, mtafiti aliweza kupitia maandiko na kukusanya data za msingi kutoka katika riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*.

### 3.7.2 Zana/Vifaa vya Utafiti.

Vifaa vya aina mbalimbali tuliweza kuvitumia katika utafiti huu, ambapo, miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta, simu ya mkononi, kalamu, penseli, shajara na vifaa vingine vya aina tofautitofauti. Vifaa hivyo, kwa kiasi kikubwa vilisaidia katika kufikia malengo ya utafiti huu, hii ni kutokana na kutumika ipasavyo.

## 3.8 Uchambuzi wa Data

Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui, mbinu hii ni kuzisoma riwaya teule kwa lengo la kupata uelewa, na kubainisha matumizi ya mhusika wa Kimimi katika riwaya hizo. Sababu ya kuitumia mbinu hii ni kwamba, hii ni mbinu ambayo ilikuwa inaakisi vyema tafiti za kimaelezo. Aidha, tunaamini kuwa, mbinu

hii ilituwezesha kuzibaini na kuzitenga data zinazohusiana katika kundi moja, na kusaidia uchambuzi na mjadala wa data hizo.

Taarifa mbalimbali za kimaudhui zilichambuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti. Ambapo kila lengo liliunda sehemu ndogo ambayo kila moja ilikuwa na maudhui yanayohusiana na mada hii. Mbinu hii ya ufafanuzi wa kimaudhui ilitumika kwa sababu, sehemu kubwa ya data za utafiti huu ilikuwa ni ya kimaelezo.

### 3.9 Itikeli za Utafiti

Itikeli ni miongoni mwa vipengele muhimu sana katika utafiti wa kitaamuli, kwani, kipengele hiki kinaweza kumfanya mtafiti akose data ambazo alipangilia kuzipata kisipotumika vilivyo. Hivyo, ni vyema kwa mtafiti aelewe itikeli za jamii anayoenda kuitafiti, ikiwa ni pamoja na kuziheshimu itikeli hizo. Pia, mtafiti anatakiwa awe na sifa ya unyumbufu katika jamii ambayo ataenda kuitafiti.

Kitu cha msigi hapa ni kuwa, mtafiti anatakiwa asivunje miiko ya itikeli za jamii husika.Mtafiti alitumia itikeli za utafiti kwa kuheshimu miiko, mila na desturi za maeneo yote aliyoyatembelea kwa lengo kukusanya data. Na hii ilimuwezesha mtafiti wa kazi hii kupata data alizozihitaji bila ya usumbufu wowote.

### 3.10 Uthabiti na Uhalali wa Data

Data za utafiti huu zilikuwa za kutosha na za kuaminika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, data hizo zilipatikana katika vyanzo vinavyosadikika kuwa ni vya kuaminika. Kwani mtafiti alipata data hizo kutoka katika machapisho ambayo yaliandikwa na wataalamu waliobobea katika tasnia hii ya uandishi. Kwa kuwa

vyanzo hivyo vilipatikana katika maktaba za vyuo vikuu vinavyoaminika nchini, ni dhahiri kwamba ni halali na vya kuaminika.

### 3.11 Hitimisho

Sehemu hii inahusu methodolojia ya utafiti. Eneo la utafiti limetajwa kuwa ni Unguja, Pemba na Dodoma, ambapo maktaba za Chuo Kikuu cha Dodoma, SUZA, Sumait na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania zilitumika katika kupata maandiko mbalimbali. Walengwa wa utafiti huu walikuwa ni riwaya ya *Dnia Yao* na *Nyso za Mwanamke* za Said Ahmed Mohamed.

Sampuli ya utafiti ilipatikana kwa kutmia mbinu ya usampulishaji lengwa, wakati njia za uksanyaji wa data ni pamoja na mbinu ya mapitio ya maandiko malimbali. Vifaa vilivyotmika ni pamoja na kompyuta mpakato, kalamu, penseli na vinginevyo. Aidha, utafiti ulitumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui kwa kuzisoma riwaya teule. Kwa kutumia mawanda hayo ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuyafikia na kuweza kufanikisha utafiti wake kwa kiwango cha hali ya juu. Kwa mnasaba huo, sura inayofuata itaelezea mjadala wa matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura hii imegawanyika sehemu kuu tatu zinazoakisi malengo mahsusi yaliyojenga utafiti huu. Sehemu ya kwanza, inajadili miktadha mbalimbali ambayo wahusika wa Kimimi wamebainishwa. Sehemu ya pili, inafafanua upekee wa wahusika wa kimimi katika kujikengeusha kwao na jamii. Kadhalika, sehemu ya tatu ya sura hii, inatathmini sababu za wahusika wa kimimi katika kujikengeusha na jamii iliyochorwa na mwandishi, ikifuatiwa na hitimisho.

## 4.2 Miktadha ya Wahusika wa Kimimi katika Riwaya Teule

Sehemu hii inajadili miktadha mbalimbali katika riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso zaMwanamke,*ili kufafanua miktadha ya wahusika wa Kimimi waliosawiriwa na mtunzi wa kazi hizo. Ithibati ya kuchimuza kwa wahusika hao imejengwa chini ya miktadha mbalimbali katika riwaya hizo. Katika tasnifu hii, tumelishughulikia suala la miktadha kwa maana ya kuonesha mahali au mazingira ambayo yanasawiri kutokea au kutendeka kwa jambo fulani.

Uchambuzi wa riwaya zote umejikita kwa namna kazi hizo zinavyofafanua mfumo wa maisha ya jamii kiutawala, kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mawazo ya Said Ahmed kuhusu wahusika wa Kimimi, yaelekea kulandana na namna mwandishi huyo alivyopitia misukosuko mbalimbali katika maisha yake, na ndiyo maana akayasawiri kupitia kazi zake za kifasihi; kwani, inasemekana alipitia vikwazo mbalimbali katika maisha yake.

### 4.2.1 Miktadha ya Chimbuko lafasihi

Fasihi ni sanaa ya lughainayosawiri vipengele vya maisha, mahusiano na hisia za watu katika muktadha fulani (Mulokozi, 1996). Data zilizokusanywa katika riwaya ya *Dunia Yao* zinaonesha kwamba, msanii ametumia mhusika wa Kimimi katika miktadha yenye kuonesha chimbukofasihi, hasa anapojadili kuhusiana na dhana ya ubunifu wa kazi za fasihi. Msanii anamtumia mhusika Bi. Muse na Miza kama chimbuko la usanii wake. Yeye, anatudokezea namna Muse ambaye anaaminika ni Mungu wa Wayunani wa kale kuwa, ndiye aliyempa nguvu za kisanii katika kukamilisha utunzi wake. Msanii anasema:

> Mimi ni Muse," alipokwishaniketisha aliniambia kwa sauti yake, sauti tamu ajabu."Unatoka wapi?" nilimuuliza."Kwa asili hasa, Ugiriki-lakini siku hizi naishi popote. Mara nyengine hujificha katika vina virefu vya ardhi kabla sijachomoza kumdhuru niliyemchagua. Na leo nimekuchagua wewe. Kwa hivyo, nimechomozekea chini ya mnazi palipofukiwa kitovu chako baada ya kupiga mbizi Bahari ya Hindi kuja kukuingia kichwani mwako… (uk. 61).

Katika dondoo hili, tunaona namna dhana ya chimbuko la fasihi inavyojidhihirisha katika mjadala huu. Maelezo haya yanalandana na nadharia ya chimbuko la fasihi kama wigo. Hali hii inashadidiwa na Mulokozi (1996), ambapo anasema kwamba, nadharia hii ni kongwe sana hata kabla kuzaliwa Kristo. Kwa mfano, Wayunani wa kale huko Ulaya, walikuwa na Miungu wa ushairi na muziki waliowaita Muse, ambao wasemekana ndio waliowapa watunzi msukumo wa kiroho, kinafsi na kijaziba wa kutunga. Wale wanaokubaliana na nadharia hii wanaamini kwamba, Mungu ndiye msanii mkuu. Kaumba ulimwengu kwa usanii wa ajabu na mwanadamu pia ni zao la usanii wa Mungu.

Tunaporejelea mkabala wa Saikolojiachanganuzi tunaona kwamba, mawazo haya yanajitokeza kupitia msingi anaoamini Freud kwamba, msanii anapoandika jambo anakuwa kama muotaji ndoto. Kupitia maelezo haya tunaona kuwa,msanii

anatuambia ukweli kuhusu kile anachokiamini kuhusu chimbuko la fasihi. Hii ni kusema kwamba, msanii anaamini kuwa, chimbuko la fasihi ni Mungu.

Hali hii pia, inajitokeza katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ambapo, msanii anaonesha namna saikolojia ya mtu binafsi inavyopata matatizo na masumbuko kutokana na kadhia zilizomkabili. Msanii anaonesha namna Nana katika wimbo wake alivyokuwa na matatizo ya maisha yaliyomkabili. Tunaelezwa hili kama msanii asemavyo:

> …Ile tafkira na falsafa ya wimbo wenyewe. Yale maneno anayoyatamka na kuyapangiza mizani, maneno ambayo yanasema lakini hayasemi wazi wazi. Njia gani? Inaelekea wapi? Namna gani yeye anaweza kuzipa kisogo? Anaweza au hawezi? Kwa nini moyo wake umeshikwa na tego? Kwa nini anaungama kilio? Kwa nini njia imeziba ugo? Njia ya kwenda wapi? Kumfikia nani? Aaaa, kwa namna fulani nilihisi kama wimbo huo nimetungiwa mimi. Kwa namna fulani lakini kwa nini? Usiniulize. (uk. 40-41).

Katika dondoo hili, tunaona udodosi wa kinafsi ambao unajikita katika nadharia ya Saikochanganuzi. Mhusika anajaribu kuyadodosa na kuyaweka wazi matendo na fikra zilizomo moyoni mwake. Kwa hali hii, tunaona kwamba, anasawiri msingi wa udodosi nafsi wa nadharia ya Saikochanganuzi.

Katika Riwaya ya *Dunia Yao,* msanii anaeleza msimamo wake juu ya dhana ya maisha. Anapingana na Kezilahabi, msanii wa fasihi ya Kiswahili ambaye yaelekea kazi zake amekuwa akiziandika kwa mkakabala wa Utamaushi. Msanii hakubaliani na maana ya maisha kama anavyoiona Kezilahabi kwamba, ni fujo ya maisha. Hili tunaliona pale msanii anaposema:

> Ingawa najua hata na mimi nimeshakufa, ukweli ni kwamba siamini juu ya fikra ya kwamba maisha tunayoishi yanatustahiki. Dunia si uwanja wa fujo! Si zogo lisilosarifika. Sikubaliani na Kezilahabi. Namjua anayeharibu. Namwona akisukuma watu katika lindi refu. Uchungu wangu ni kwamba siwezi kumzuia. Wala siwezi kumvamia kutumbukia naye pamoja. Nimebaki kuning`inia ukingoni nikishikilia hodari huku jinamizi, kwa guu lake,

> linanikanyaga. Linanitimba. Linanipondaponda. Linanididimiza kooni pangu. Pumzi zinaziba. Ninapiga kelele. Sauti haitoki. Lakini pamoja na yote hayo najua hilo ni jinamizi tu. Na jinamizi limo ndani ya ndoto tu, na ndoto imo usingizini, na usingizi una mwisho. Jinamizi litakwisha kila mtu atakapoamka (uk. 144-145).

Kwa miongo kadhaa, dhana ya maisha kama inavyotazamwa na wafuasi wa nadharia ya Udhanaishi imekuwa ikikosolewa ndani na nje ya Bara la Afrika. Wafuasi wa dini mbalimbali hawakubaliani na mawazo ya wadhanaishi katika kuangalia suala la maisha. Hivyo, hata Said Ahmed Muhammed ambaye ni muumini wa dini ya Kiislamu, hakubali mawazo ya Kezilahabi katika mkabala wa maana ya maisha. Na, anaonesha kuwa, mawazo yake ni ndoto za utashi ambao ukweli wake utathibitika hapo baadaye.

Wahakiki kadhaa wamewahi kuliangalia suala la maana ya maisha kama linavyojadiliwa katika kazi za Kezilahabi, huku wakitoa misimamo yao. Mathalani, Musau (1985), katika tasnifu yake ya Uzamili, ambamo alishughulikia riwaya za *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1981), amegusia suala la maana ya maisha. Anafikia hitimisho kwamba, Kezilahabi ni mtu aliyekata tamaa, kwani, anatetea kwa kuyaona maisha kama uwanja wa fujo na mahala pasipo na furaha.

Tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi, ambayo inaongoza utafiti huu, tunaona kwamba, msingi wa unafsia wa wahusika unalandana na mawazo ya mhusika juu ya maisha kwa ujumla. Mhusika huyu wa Kimimi hakubaliani kuwa, maisha ni tanzia ya fujo na mateso ambayo yamemzunguka mwanadamu. Kuamini hivyo ni kuwapoteza wengine na kuwapeleka katika shimo la maangamizi.

### 4.2.2 Miktadha ya Kisiasa

Msanii amejadili masuala mazito yanayohusu miktadha ya siasa. Katika ulimwengu tulionao, mwanasiasa ni mtu muhimu sana kuwapo kwake. Chuachua (2010) anasema kuwa, mwanasiasa ni mtu yeyote anayejihusisha kwa vitendo au kwa nadharia katika mambo yahusuyo mfumo wa utawala wa nchi. Kwa maana hiyo, kumbe mwanasiasa anaweza kusababisha matabaka katika jamii anamoishi.

Hivyo, msanii anaonesha kuwa, utawala uliopo umejenga tabaka la waliojuu na waliochini. Waliojuu ndio ambao wanafaidika na matunda ya uhuru wa bendera na waliochini, wamekuwa katika mahangaiko na kutothaminiwa. Siasa kama hii, siyo ilioyotarajiwa na Waafrika wakati wa kupigania uhuru wao. Hivyo basi, hali kama hii, inawakatisha tamaa wazalendo wa nchi hizi.Katika riwaya ya *DuniaYao* msanii anatueleza hili kwa kusema:

> Najua mimi…najua kwa nini hutaki kubadilika mtu wewe? Hata wahakiki wako wanakusema…Naam, kama unavyojua. Nilijua anatambua. Kimya.Wamechukua kila kitu! Niliendelea. Wao wamekuwa ndio wafikiri wetu. Wasemaji wetu. Watendaji wetu. Wanaohisi kwa ajili yetu. Waona njaa na kiu zetu. Walimu, madaktari, wanafalsafa, wanauchumi, mashehe, mapadri na walinzi wetu. Kwa jumla waendesha maisha yetu yote. Sehemu za viwiliwili na akili zetu. Kwa ufupi wao ni kila kitu chetu! Sisi wengine ni mapipa matupu. Hatuna rojo la uhai. Hatuna supu ya maisha. Wala nyama ya ubinadamu. Hatuna sehemu ya utu. Hatuna rai. Hatuna maoni. Hatuna chetu. Hatuwezi kufikiri kama wao au zaidi ya wao. Hatutarajiwi kusema. Hatutarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi yetu… (uk. 43).

Katika maelezo haya, msanii anajadili hali ya mwenendo wa siasa inavyoendeshwa na wanasiasa katika jamii. Wanasiasa hao wamejipachika sifa ya kuwa wao ndio wenye uwezo wa kila kitu. Chambilecho Waswahili "Uzuri kwao." Viongozi ni waamuzi wa lile watakalo litekelezwe na watu wa tabaka la chini, kwa manufaa yao binafsi na si kwa manufaa ya jamii. Haki za msingi za kibinadamu zinakiukwa na viongozi; kutokana na kujiona Miungu watu. Hawasikilizi tena ushauri wa yeyote.

Ndio maana msanii anasema kuwa, wao ni walimu, wanafalsafa, madaktari, mashekhe na mapadri. Hii ina maana kwamba, kwao makundi haya hayana maana yoyote.

Vilevile, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* msanii anaonesha namna wavujajasho ambalo ni tabaka la wakulima linavyohangaika na kunyonywa na tabaka tawala. Kutokana na unyonyaji unaofanywa na wale walio juu kwa watu wa tabaka la chini, msanii anaonesha kwamba, tabaka la chini halikuwa kimya kutoa malalamiko yake katika maisha yao yote. Tunasimuliwa hili pale, msanii anaposema:

> Bado mpaka leo wakulima wananung`unika, na hawatasita milele ingawa hawajui wamlalamikie nani. Vipi Yule mfua vyoo jana leo awe tajiri mkubwa kiasi hiki? Wao walikuwa wapi alipojitutumua? Hakusomba mali tu, bali kaiba heshima ya wakulima baada ya kuwanyang`anya ardhi na uhuru wao. Na uhuru ni nini kama sikipato? Ghafla amepata nguvu zinazomsimamisha kumsuta kila mtu. Nguvu ambazo watu huziona kila siku zikiharibu, lakini hawawezi kuzizuia. Wanabaki kujiuliza kinatokea nini katika maisha yao? Laana ya Muungu au mapuuza ya binadamu mwenyewe? Yawapi yale yaliyoelezwa kuhusu usawa? Yawapi yale waliyoahidiwa?Uhururu na kazi. Uhuru na haki. Uhuru na maendeleo. Uhuru na nini sijui… Yako wapi matunda waliyoambiwa watagawiwa akishaondoka Mzungu na Mwarabu? (uk. 37).

Dondoo hili, linaonesha namna watu walivyokata tamaa na kile kinachopigiwa kelele na viongozi wa nchi za Bara la Afrika. Mjadala huu unaonesha kwamba, maneno ya kudhamiria kuleta maendeleo kutokana na kupatikana kwa uhuru yalikuwa ni lele mama za wanasiasa tu, ambao wanania ya kujilimbikizia mali wao binafsi. Kutokana na ubinafsi walionao, viongozi wamesahau malengo ya kudai uhuru katika bara hili, na badala yake wamekuwa wakijikushanyia mali za uma kwa manufaa yao binafsi.

Tukirejelea nadharia ya Saikochanganuzi ambayo inaongoza utafiti huu, tunaona kuwa, mawazo haya yanalandana na uzoefu wetu kwa jamii kutokana na hali ya viongozi wengi leo hii. Viongozi wamekuwa wakikiuka maadili ya uongozi wao. Haki za watu wa tabaka la chini zimekuwa zikivunjwavunjwa bila kujali kwamba, wanasiasa wapo ili kuitumikia jamii na si kuitendea maovu. Pia, wakumbuke kwamba, lengo moja la kuleta uhuru katika barala la Afrika ni kuleta usawa wa kila mtu.

### 4.2.3 Miktadha ya Shereheni

Msanii pia, ametumia miktadha ya sherehe mbalimbali, ambapo anaonesha namna miktadha ya kwenye sherehe hizo kunavyoibuka migogoro miongoni mwa wanajamii. Katika *Dunia Yao,* msanii anatuonesha namna wanawake wawili walivyokuwa wakipigana kutokana na kisasi walichowekeana wiki mbili zilizopita, wakiwa katika kumbi za starehe. Mapambano kama haya, tumekuwa tukikutana nayo katikika kumbi nyingi za starehe, hasa zile zinazohudhuriwa na watu wa tabaka la chini.Msanii anatusimulia tukio hili akisema:

> Mbele zaidi wasichana wawili waliowekeana chuki na visasi kwenye Mipasho au Rusharoho majuma kadha yaliyopita, leo walikuwa wakizitoa chuki na visasi vyao hadharani kwa vitendo. Walikuwa wakigaragazana topeni na halaiki ya watu inatazama sinema ya bure. Hakuzuka mtu yeyote aliyeingilia kati kukemea au kuamua. Hata mimi niliyechukia picha hii. Nilijifunza kuepuka mambo ya watu siku hizi baada ya kukumbwa na balaa mara nyingi nilipojifanya mwamuzi.“Yale ya majuzi hayakutosha?” Alilaumu mwanamama wa kwanza.“Wewe ndiye uliyeanza kwa kutukamatisha polisi.” “Mimi au wewe, uliyekosa adabu… uliyenivamia mbele ya wakubwa…” Nilisikia zamani habari hii ya wanawake kutukanana na kupigana mbele ya wakubwa, lakini haikunishangaza…” “Babu we` utakoma kututambia… nilikwambia zamani huna namba.” “Khhh, una nini? Hakuna asiyejua kwamba wimbo wa C. Licence shoga yako kaliimbia buzi langu.Imehusu nini? Utamuona vivi hivi Mcha. Dereva wangu yule babu… kama mlivyomchukua TX wetu, utafanya nini kwani?” Take care! (uk. 33).

Miktadha hii ya kwenye kumbi za starehe, kama inavyoelezwa katika dondoo hilo hapo juu, huibua chuki na ugomvi miongoni mwa vijana, hasa wanawake ambao wamekuwa wakigombania wanaume. Hivi ni vitendo vya aibu vinavyofanyika katika jamii, huku jamii ikishuhudia tu bila kuchukua hatua madhubuti, ili kukomesha makundi kama haya ambayo yamekuwa yakiendeleza ngono bila kujali. Matokeo yake ni kuliingiza taifa katika maangamizi makubwa, ikiwamo kuongezeka kwa tatizo la kuenea gonjwa la Ukimwi. Hali hii ndiyoanayoieleza Ali (2015), kwamba, wanawake wengi leo hii wamekuwa na tabia ya kufanya mapenzi ya nje ya ndoa bila kujali athari zake.

Pia, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, msanii anatuchorea miktadha ya mhusika Mimi katika sherehe, ambapo mhusika Nana na wenzake wako katika lango la kuingilia katika ukumbi wakiwa wamepanga foleni na wazazi wake, ili kupokea mkono wa pongezi. Hata hivyo, mhusika Nana anaeleza kwamba, hakuwa hapo kimawazo, kwani alipendelea iwe siku ya kujikengeusha. Tunaelezwa hayo na mhusika huyu pale msanii anavyosema:

> Pale langoni nilisimama huku nimedorora kabisa; kama vile nilikuwa nimepoteza hamu ya maisha. Bila shaka nilponyooshewa mkono na kila aliyeingia niliupokea. Na mikono ya kupongezwa ilikuwa ni mingi si haba. Lakini niliipokea pasi na kujua. Kusema kweli, nilijibu pongezi za kila mtu, ingawa sikusikia nilichoambiwa wala nilichojibu (uk. 34).

Tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi ambayo inayoongoza utafiti huu, tunaona kuwa, uhusiano kati ya wahusika wanawake ambao wamekuwa wakienda katika kumbi za starehe ni tata, ambao umejigawa katika pande mbili zinazokinzana. Kila upande umekuwa ukijivutia wanaume na kujiringia kuwapata wanaume hao. Matokeo yake ni wanawake kujipeleka kwa wanaume na kuwa chombo cha starehe.

### 4.2.4 Miktadha ya Kazini

Wasanii wanajadili kazi za serikali hasa nyadhifa za uongozi. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* msanii ametumia miktadha ya kazini ambapo anaonesha kuwa, katika kazi hizo mara nyingi kunakuwa na mipango ambayo imekuwa ikipangwa na viongozi, lakinihaitekelezeki. Kimsingi, kazi za ofisini huambatana na kutowa mawazo ambayo kamwe hayana matokeo chanya katika jamii. Ingawa mipango huwa ni mizuri, lakini haitekelezwi na wale waliojuu. Tunasimuliwa na msaniiyakwamba:

> Kusema kweli, mimi sikupenda kazi ya ukarani katika daraja yoyote ile- ya juu au chini. Nilidhani kwamba kazi hiyo ni mbaya mno mtu kufanya. Kukaa kitini kutwa nzima. Kupigiwa chapa barua na seketeri ili kutia saini tu. Kupanga mambo yasiyopangika. Kutoa mawazo yasiyosikilizwa wala kusikilizika. Kufanya semina na warsha zisizoleta tija ila kupoteza wakati na fedha chache zilizopo. Pia niliamini kwa namna fulani kwamba kazi ya utawala ni kazi ya ukorofi, kwangu na kwa wengine. Ilikuwa ni namna fulani ya uungumtu. Ilikuza kichwa cha mtu na kumfanya ahisi anaweza kugusa mbingu. Najua ilikuwa jeuri ya namna fulani kwa upande wangu (uk. 17).

Katika dondoo hili, msanii anaonesha namna kazi za ofisini na utawala zinavyomdumaza mtu, na kumfanya awe ni kasuku asiyehoji lolote bali kupokea amri kutoka kwa wakubwa. Aidha, kazi hizi za ofisini zinamjenga mtu kuwa na jeuri na kujiona kama mwenye uwezo wa kila kitu zaidi ya watu wengine. Msanii anakosoa semina na warsha mbalimbali ambazo kwa ujumla hazina tija kwa wanajamii, ispokuwa ni matumizi mabaya ya pesa za umma. Matumizi haya mabaya ya pesa za umma, yamewahi kukemewa vikali na Raisi wa Jamuhuri Muungano wa Tanzania wa awamu ya tano, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, na kuwataka viongozi kufanya kazi kwa manufaa ya taifa bila kusubiri semina elekezi. Hivyo, msanii anakataa kazi ya ukarani huku akiamini kuwa, kila mtu anaweza kuwa karani, lakini hawezi kuwa mwalimu au msanii. Mtunzi anaamini kwamba, kazi ya

ualimu na usanii ni ya kipekee, na haiwezi kulinganishwa na ukarani. Kuhusiana na hili, msanii anasema:

> Nilitaka tu kazi ya kutenda na kutendeka mimi mwenyewe. Kazi ya kuumba na kubuni. Kusanifu na kutengeneza. Kazi ya furaha kwangu na kwa wengine. Kazi ya manufaa kwa wote. Sikupenda kukaa kitini tu. Nilipenda kusimama na kutembea. Kwenda. Kuchangamsha kiwiliwili na bongo. Kazi ya ualimu. Kazi ya uandishi wa sanaa. Kazi ya kusoma na kuandika. Kazi ya kupokea fikra na kurudisha fikra baada ya kuzijaza pumzi mpya. Kila mtu anaweza kuwa karani kila siku, lakini si kila mtu anaweza kuwa mwalimu au msanii kila mara! (uk. 17-18)

Aidha, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* msanii ametumia miktadha ya kazini ambapo, anaonesha namna shuguli za kikazi zinavyomfanya mtu kuwa katika mahangaiko makubwa.Hili hujitokeza kutokna na haja ya kutaka kutimiza lengo la shughuli yake. Kwa mfano, tunaelezwa namna Faisal alivyokuwa akihangaika ili kutafuta vito. Ndani ya miezi mitatu alikuwa bado hajapata kitulizano. Msanii anatueleza hili kwa kusema:

> Tokea alipotua kwa *Galf Air* hajatulizana kabisa. Miezi mitatu sasa hana hamu ya mtu wala kitu, kinywaji wala chakula, sura wala mandhari. Miezi yote hiyo, kama hadithi, amekuwa akitafuta kito cha thamani. Alitafuta kama ule mchezo wa kitoto; saka mke wangu, saka mke wangu… Hapa hayupo, hapa hayupo! Hamu na matarajio yamemfanya amuulize kila mtu. (uk. 7).

Tukirejelea nadharia ya Saikochanganuzi, tunaona kuwa, mawazo yanayopatikana katika dondoo hili yanalandana na msingi wa nadharia hii, tunaona kuwa, mawazo ya mhusika Mimi yanalandana na msingi wa kuyachunguza mawazo ya mhusika katika kazi ya fasihi husika. Hivyo basi, mawazo ya mhusika Mimi, ni kuangalia kazi ya ukarani na ofisini kwa ujumla kuwa, haina tija kwa jamii. Anatilia mkazo kazi ya uwalimu na usanii, ambayo inatoa fursa ya kuisadia jamii mzima badala ya mtu binafsi. Pia, namna anavyojishughulisha Faisal kuhusiana na kazi, ndivyo tunavyowaona matajiri wengi kukosa kitulizano kutokana na shughuli zao za kibiashara.

### 4.2.5 Miktadha ya Kifamilia

Msanii anaakisi miktadha ya familia ambapo katika riwaya ya *Dunia Yao* mhusika Mimi ana mikinzano na familia yake. Hali hii inatokea kutokana na Yungi kufanya uzinzi. Jambo hili analiona kuwa si sawa, kwani ni ukiukwaji wa maadili. Pia, mwanadamu hawezi kuutumia mwili kwa utashi wake binafsi hasa katika kufanya uzinzi. Kimsingi, ngono haikubaliki katika jamii. Kufanya uzinzi ni aibu kubwa katika familia. Kwa ujumla, hali hii ndiyo iliyosababisha mhusika huyu wa Kimimi kujitenga na familia yake, na hata kugomea kula vyakula ambavyo aliamini vilipatikana kutokana na pato la ngono lililokuwa likifanywa na Yungi. Msanii anatueleza hali hii kwa kusema:

> Mimi nafahamu, niliwaza. Nafahamu Yungi. Wallahi nafahamu. Labda wewe hufahamu. Ndiyo mwili ni wako. Una haki nao. Una uhuru wa kuufanya upendavyo. Lakini wakati mwengine mwili ni silaha pekee aliyonayo mtu. Sharti autumie vizuri. Sharti aulinde. Mara nyingi mwili mwili unapokuja kudokolewa na kuendelea kumegwa udohoudoho, mtu huwa ameshapoteza utulivu wa mwili na akili na kwa hivyo ameshapoteza kila kitu. Ni bora kubaki na kitu kimoja tu kama roho, kuliko kukosa kila kitu! (uk. 107).

Katika dondoo hili, msanii anaona kuwa, ngono ni tatizo la kujitoa katika thamani. Suala hili linaondoa utu wa mtu na kumfanya asiwe na thamani katika jamii. Hivyo, anawaonesha wale wanaofanya ngono holela kuwa, wanapoteza utu na hadhi yao.

Ama kwa upande wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* tunaelezwa mikinzano iliyopo katika familia ya Nana na wazazi wake. Tunaelezwa kwamba, Nana alikuwa na mgogoro na baba yake kutokana na kutaka kumchagulia mchumba asiyemtaka.Matokeo yake Nana anaamua kujikengeusha kwa kuasi utamaduni huo. Akaamua kutosema na hata baba yake wakati anaposemezwa na baba huyo. Mgogoro huu unaelezwa na msanii kwa kusema hivi:

> Mimi huwa simjibu anaporopokwa baba. Hujijibu mwenyewe kwa mwenyewe tu, tena kimya kimya, ndani kwa ndani. Wimbo si mapenzi. Wimbo si hisia. Ni kitu cha uchawi. Humteka mtu yoyote. Hata walii. Hata kuhani. Si lazima uwe na vinanda. Silazima usikike nje na kila mtu. Huweza kuwa wimbo wa ndani kwa ndani. Moyoni mwa mtu. Hasa ule wimbo unaoingia na kukaa juu ya kiti cha moyo na kumwaga mwangwi ndani ya damu ya mtu (uk. 42).

Hali kama hii, inalandana na nadharia ya Saikochanganuzi ambayo inaongoza utafiti huu. Tunaporjelea nadharia hii na tukahusisha na wanawake wengi ulimwenguni leo hii, tunaona kwamba, wasichana wamekuwa wakijikengeusha na jamii kutokana na kutaka uhuru wa mwanamke. Mgogoro mwingine wa kimapenzi ni kati ya Bimkubwa na familia yake, kutokana na kulazimishwa kuolewa na mume ambaye si chaguo lake (uk. 152).

#### 4.2.6 Miktadha ya Mahakamani

Msanii anatumia miktadha ya mahakama za nchi za Magharibi na namna zinavyolishughulikia suala la uhamiaji. Mahakama ni mahali ambapo kesi na mashtaka mbalimbali husikilizwa na kuamuliwa(TUKI, 2004). Msanii anaonesha kuwa, mahakama hizo zimekuwa zikijua ujanja unaofanywa na watu kutoka mataifa maskini, ambao wanataka kupata makazi katika nchi hizo. Watu wamekuwa wakidanganya ili kupata fursa ya kuishi nchi hizo. Hata hivyo, ni wazi kuwa, mahakama hizo huwa zinajua kila kinachoendelea, bali wanafanya hivyo ili kufanikisha mradi wa nchi zao. Mhusika Mimi anatusimulia hili kama msanii anavyosema:

> Na wao wanajua umewahonga mawakili waje wakusemee uwongo au mashahidi waje wakulie yamini kuwa wewe ni Msomali au Mrwanda au Mburundi. Wanajua yote lakini hawajui. Unawaona wapumbavu lakini mpumbavu wewe. Wao werevu kupita kiasi. Tena hawana haraka. Ya nini haraka. Hawachukulii pupa. Wanasema wanafuata sheria walizoziweka wao wenyewe. Na huo ndio Uingereza safi. Sheria! Wanaheshimu sheria. Lakini sheria mpaka kuwa sheria kwao, hasa kuhusiana na wageni, imeshapimwa vyakutosha faida yake na hasara zake. Wanakuachia uwepo na kukugharamia makaazi yako. Unapewa pahali pa kuishi na mama. Unapewa

> hoteli, chumba, nyumba kwa kutegemea ulivyo- peke yako au na watoto. Unapewa `coupon` au fedha za chakula na mahitaji madogo madogo. Bila shaka unafanyiwa yote hayo kwa kupewa onyo. Unaambiwa huruhusiwi kufanya kazi na sheria ya kutoruhusiwa ipo. Lakini hapana asiyejua kuwa kila mgeni hapa huja kutafuta kazi… (uk.119).

Kupitia dondoo hili, msanii anatuonesha hali ya maisha ya wageni katika nchi ya Uingereza. Msanii anaonesha kuwa, kile kinachofanyika kwa miktadha ya wageni wanaoingia katika nchi hiyo, ni kiini macho cha kuendeleza ukandamizaji dhidi ya wananchi kutoka nchi changa, ambao wanaingia Uingereza kwa mwavuli wa ukimbizi.Sheria zinazozuia kuwapokea na zile zinazohusu ajira kwa wageni zipo.

Hata hivyo, sheria hizo zimekuwa zikifanyika kwa manufaa ya taifa hilo. Hivyo basi, wakimbizi wanaofika katika nchi hiyo, wajuwe kuwa, taarifa za kintelijisia huwa ziko wazi na zinawahusu wao.Wanaachiwa kufanya yale wanayoyafanya kwa manufaa ya taifa hilo tu.

### 4.2.7 Miktadha ya Mitaani

Tunadokezwa namna hali ilivyoharibika katika mitaa mingi ya Afrika. Mitaani kumejaa kila aina ya matatizo ambayo hayakuwapo hapo kabla. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* tunasimuliwa namna ambavyo mikururo ya watu ilivyokuwa ikimuongoza mbakaji aliyekamatwa na msichana wa miaka minne. Msasnii anatuonesha kwamba, hali kama hii haikuwa ya kawaida katika mitaa yetu hapo zamani. Hii ni aina ya mabadiliko ya kijamii katika kujikengeusha ambapo, hali ya maisha yaliyozoeleka hapo kabla, taratibu yanaanza kubadilika kutokana na baadhi ya vijana kuvamia mila za Kimagharibi, au kutaka kutimiza utashi wao bila ya kuangalia mipaka ya kiutamaduni. Jambo hili linaelezwa na mhusika Mimi pale msanii anaposema:

> Itakuwa miujiza nikikwambia tokea ninapotoka ng`ambo kuelekea mjini barazani, sikuona vituko vilivyonipaparisha moyo. Ingawa kusema kweli

> siku hizi nimevizoea na kupunguza hisia navyo. Hapa, zogo la kundi la watu linamuongoza kibaka aliyekamatwa na kitoto kijanajike cha maiaka minne. Damu zinamvuja. Aaaa; sikumbukii zamani mambo haya nchi hii ilipokuwa nchi! Mbele ya safari nikapita mtaa uliozuka ghafla katika shaghalabaghala mpya…vibanda vimechipuka ovyo. Labda vibanda si neno zuri kwani huku kwetu, kibanda kilikuwa na sura na heshima ya aina yake. Hivi ni vichafukizi vilivyosimamishwa na shaghalabaghala mpya (uk. 31).

Hali hii inayoelezwa na mhusika ndiyo inayoiakisi jamii ya Zanzibar leo hii. Zanzibar imepokea mabadiliko ya kijografia hasa katika mitaa yake. Watu wamekuwa wakijenga bila mpangilio maalumu ambao ungefanya mpango wa mji kuwa wa kuvutia. Aidha, wakati huu, eneo hili limekumbwa na mabadiliko ya kiutamaduni, hasa kwa vijana kujiingiza katika vikundi viovu. Ubakaji kama ulivyoelezwa umekuwa ni tishio. Ambapo, matendo haya ya kinyama yamekuwa yakifanywa na watu wa makamo na vijana bila ya hata kujali athari yake.

Pia, hali hii ya uvunjifu wa maadili haikufumbiwa macho na Mtobwa (1998: 5-6), pale alipomtumia mhusika wake Rukia akikumbwa na kadhia hii ya ubakaji, wakati akiwa njiani kuelekea nyumbani, ndipo alipokumbana na vijana wawili na kumbaka. Nia ya msanii ni kuonesha namna binadamu alivyokuwa kama mnyama, kutokana na tabia yake mbaya ya ubakaji.

Aidha, mabadiliko haya ya kiutamaduni, yamewakumba hata wanawake kama tunavyoyashuhudia katika mitaa. Tunasimuliwa namna mhusika Mimi anavyokumbana na matukio yasiyokuwa ya kawaida aliyowahi kuyazoea. Katika mitaa anaeleza kuwa, alikutana na wanawake waliokuwa wanapigana kutokana na kuchukuliana mabwana (uk.33). Kiukweli, matukio kama haya ni matukio ambayo hayakuzoeleka hapo kabla. Yaelekea msanii anaamini kuwa, ni kabla ya nchi hii kuungana na Tanganyika. Kwani anasema kuwa, matukio kama haya hayakuwapo wakati nchi hii ilipokuwa nchi.

Pia, mhusika Mimi (Ndi) anatusimulia namna anavyokumbana na tukio la kushangaza akiwa mtaani. Katika nyumba moja ambapo anakutana na watu waliokuwa katika kibanda, waliokusanyika wakimsikiliza mtoto na mama ambye anamlazimisha mtoto wake kufanya mapenzi nayeye. Msanii anailinganisha hali hii na umma wa Nabii Luti, ambapo anaona ni lini atafufuka kuja kuokoa uchafu huu. Msanii anamtumia mhusika Mimi akitusimulia mkasa huu kwa kusema:

> … nilipopita Kundemba juzi juzi. Juzi ya kijomba. Nilipokuta watu wamejazana mbele ya kibanda fulani. Wanasikiliza furja iliyokuwa ikitokea ndani ya nyumba fulani. Mama alikuwa akibumburushana na mwanawe barubaru, kumlazimisha kulala kitanda kimoja naye. Kijana alipigana kujipapatua na dhambi hizo. Lo! Salala! Lini Nabii Luti atafufuka kuja kuuokoa umma wa Sodom na Gomora? (uk. 34).

Pamoja na matukio haya ya uvunjifu wa maadili katika mitaa, pia, mhusika Mimi anatusimulia hali ya uchafuzi wa mazingira katika jamii, pamoja ulevi wa ovyo ovyo. Tunaelezwa namna mitaani mulivyokithiri wizi, pombe na uchafu ambao huweza kusababisha miripuko ya magonjwa kama kipindupindu(uk.32-33).

Kwa kuendelea, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* tunaelezwa namna kulivyokuwa na matatizo mengi. Wapo baadhi ya vijana ambao wamejiingiza katika vikundi viovu, ikiwamo ulevi. Mathalani, tunamuona Ngware anavyotumia nguvu na kufanya fujo ili kuhakikisha anajipatia pesa ya kununulia ulevi. Msanii anatueleza hili kwa kusema:

> Mtu angetaraji nini binadamu anapogeuka mnyama? Tena kuwageukia hata wale waliomzaa na kumlea? Wale waliomleta duniani na kumshibisha nguvu za kuhujumu na kupiga? Hatimae Ngware amegeuka nunda mla watu” Hana kizuizi na vitu wala mali ya watu (uk. 275).

Vijana kama Ngware, leo hii wameenea sana katika jamii yetu. Kama msingi wa nadharia ya Saikochanganuzi inavyozingatia matukiao ya kijamii, ni wazi kwamba, msanii kupitia mhusika huyu anaakisi miktadha ya mitaa mingi katika jamii zetu ambamo kumekumbwa na vijana kama hawa.

## 4.3Hitimisho

Kimsingi, mchakato mzima wa kipengele hiki ulilenga kulifikia lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu, ambalo lilikuwa ni kubainisha miktadha ya wahusika wa Kimimi katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Tumebaini kuwa, kumbe Said Ahmed hakuwa akijiandikia tu kiholela katika kazi zake za kisanaa, isipokuwa aliongozwa na dhamira fulani zenye lengo la kuyaumba maudhui yaliyomo katika kazi zake za kisanaa. Riwaya zake zimesheheni maudhui mbalimbali ambayo miongoni mwayo ni; pamoja na,changamoto za kisiasa. Katika muktadha wa kisiasa, mwandishi ameonesha namna uongozi wa Kiafrika ulivyojengwa katika misingi ya kitabaka, kwa kuonesha tabaka la juu na tabaka la chini. Mbali na hayo, maudhui yake yamejikita katika miktadha mbalimbali kama vile, miktaddha ya chimbuko la fasihi, shereheni, kazini, kifamilia, mahakamani na mitaani. Maudhui hayo yanadhihirisha kuwa, hakuwa akipendezwa na suala zima la unyanyasaji wa wanajamii; na ndio maana hakufumbia macho.

## 4.4 Upekee wa Wahusika wa kimimi katika Kujikengeusha na Jamii katika Riwaya Teule

Katika kusawiri jambo lolote lile, basi kunakuwa na hali fulani inayompa mwandishi msukumo wa kufanya jambo hilo. Chuachua (2010:124), ananukuliwa akisema kuwa, “Mwandishi yeyote husukumwa na kani fulani inayosababisha atoe ujumbe alioukusudia.” Dhamira ya mwandishi ilikuwa ni kuonesha namna wanajamii wanavyojikengeusha katika jamii zao, ndio maana amewatumia wahusika wake wakionesha ukengeushui huo ili kujiweka katika hali ya upekee. Ann (2013), Yeye, aliona kuwa, suala la ukengeushi wa wahusika huibuka kila wakati kutokana na fikra na mitazamo mipya ya wanajamii.

Kuibuka upya kwa hali hizi, kumechangiwa na uvumbuzi wa teknolojia mbalimbali, na uvumbuzi huo ukitokana na ujuzi na maarifa anuwai ambao binadamu anaendelea kujipa kupitia masomo, maingiliano ya tamaduni na hali ya kutaka kuifahamu zaidi dunia yake. Fikra, mwono wa ulimwengu na mtazamo wa mambo kulingana na yalivyokuwa katika karne ya kumi na tisa, ni tofauti sana na wakati wa sasa wa kipindi tunachoshuhudia wanawake wakitaka kujikomboa. Ukengeushi huu tunaousawiri ni kuanzia karne ya kumi na tisa hadi kipindi tulichomo. Hivyo basi, masuala hayo mapya ndiyo tunayorejelea kama dhana ya ukengeushi. Hali hii husawiriwa na namna baadhi ya wahusika wanavyouchukulia ulimwengu wa wakati huu, na bidii anazochukua mwanamke katika kujikomboa. Hivyo basi, wahusika katika *Nyuso za Mwanamke* na *Dunia Yao*, wanaonekana kujikengeusha kama ifuatavyo:

### 4.4.1 Kugomea Chakula

Mgomo ni tendo la kuacha kufanya kitu hadi masharti fulani yatekelezwe (BAKIZA, 2010). Mwandishi wa riwaya ya*Dunia Yao* amemtumia mhusika Mimiambaye anaamua kugoma kula chakula nyumbani kwake, kutokana na kuamini kuwa, chakula hicho kinaletwa na Yungi. (Msichana ambaye amejiingiza katika ukahaba). Hivyo, ili kuonesha anachukia kitendo hicho, anaamua kugomea chakula nyumbani kwake. Huu ni ukengeushi, kwani, katika jamii za Uswahilini, mzazi huwa anatumia juhudi za kila aina ili kuhakikisha amekomesha tabia kama hii, lakini si kugomea chakula. Kuhusiana na hilo msanii anasema:

> La! Hapana! Sitajiua wala sitakula chakula cha ukahaba, Mungu wangu! Dini yako tukufu inakataza kujiua au kula chakula cha ukahaba. Funguaaaa! Sifunguiiiii! “Nitavunja mlango…” Vunjaaaa. Baada ya hapo, sauti ya Bi M. ikapotea (uk.22).

Aidha, msanii anamuonesha mhusika Mimi akijikengeusha kutokana na kujitenga na familia yake. Hali hii inajitokeza kutokana na kukataa vitendo vya umalaya alivyokuwa akivifanya Yungi. Kwa muda mwingi mhusika huyu alijitenga akiwa hana hata mwenza wa kuzungumza naye, kutokana na kuchukia matendo ya Yungi. Tunachokiona si chakawaida hapa, ni kutokana na mhusika huyu kuamua kujitenga na familia nzima, badala ya kujitenga na Yungi tu. Hivyo, amemuingiza katika makosa aliyemo na asiyekuwamo. Anajaribu kufuata msemo wa Waswahili unaosema “Samaki mmoja akioza, Huozesha mtungo mzima.” Kwa hali hiyo, makosa yanafanywa na mtu mmoja, lakini wanaingizwa familia nzima. Katika kulithibitisha hili, mwandishi anasema:

> Ilinijia tu niinuke hatimae niinuke. Niinuke kusema na wahusika wangu kwani sikuwa na mwingine wa kusema naye katika hii dunia ndogo, ndani ya kijichumba hiki kamajela, humu nilimojikmelea mimi mwenyewe kwa hiari yangu. Kabisa sikutarajia kama ningefika chini hivi (uk.2).

Pia, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* mwandishi amemtumia mhusika Nana akionesha msimamo wake wa kutaka kuwa huru, na kuruhusiwa kufanya analolitaka. Jambo hili linasababisha mgogoro mkubwa kati yake na baba yake, na kusababisha mhusika Nana kuweza kugomea chakula ili tu apate uhuru wake. Chambilecho waswahili "Papo kwa papo, kamba hukata jiwe" Hatimae, Nana anafanikiwa madai yake kama msanii anavyosema:

> Alihisi ni vyema uamuzi wake uheshimiwe maana alikuwa na hisia kama wale waliomwamulia; kwanza Nana alihisi vibaya kuchukuliwa kwa gari kila siku...Aliona kuwa maisha kwake ni shuleni nyumbani au nyumbani shuleni. Jambo hili alilitafsiri kama utumwa na akataka uhuru wa kuachwa ajipeleke shuleni na ajirudishe. Kuonesha msimamo wake, aligoma kwenda shule na kula chakula, baba yake alipoona basi aliamuru apelekwe shuleni kwa gari na arudi kwa miguu (uk. 33).

Vile vile, katika riwaya hiyo ya *Nyuso za Mwanamke* tunaelezwa kwamba, Nana anadhamiria kujiingiza katika shughuli ya uimbaji, ili baadae aje kuwa muimbaji mzuri wa taarabu. Kutokana na utashi huo, Nana anajikuta akiwa kwenye foleni ili kusubiri nafasi ya kupata fursa ya kuchaguliwa kuwa muimbaji. Mhusika Nana anatusimulia hili kama msanii anaposema:

> Nilikuwa nimeketi ncha ya mwisho ya mlolongo wa vijana watano na mimi nikiwemo hesabuni. Wanawake wawli na wanaume watatu. Nilishukuru kwamba sikuwa mwanamke peke yangu. Isingekuwa ajabu katika jamii hii kutopata mwanmke anayejipendekeza kimuziki, au anayetaka kutambuliwa kuwa mwimbaji mzuri wa taarabu. Licha ya kwamba hapa sambejambo bado muziki unachukuliwa haramu, ilitazamiwa pia kwamba si laiki ya mwanamke kusimama mbele ya watu kuimba. Hali hii ilinishangaza, kwani huu haukuwa wakati wa Siti binti Saad. Ni wakati wa vita vya kila mtu kugombea kupenya kwenye tundu ya shindano kwa hali yoyote ile. Uimbaji, hasa wa taarab, haukuwa na thamani sana katika jamii hii. Haijambo muziki wa hip hop au wa rap, na hasa uwe na arki za Kimarekani (uk. 140).

Hata hivyo, Nana alitakiwa na Meneja kujikengeusha na kuimba kwa mitindo ya kisasa. Ambapo, nyimbo za kisasa nyingi zina mielekeo ya matusi, misubukuo,

tashtiti na kung'ong'ana vichwa. Pia, Nana alitakiwa avae nguo fupi ambazo zitawavutia watazamaji. Masharti haya yanamfanya Nana aigomee kazi hiyo, huku akiamini kuwa, yeye hawezi kupangiwa namna ya kuvaa au kutunga. Hivyo basi, pamoja na mshahara wa shilingi laki tatu alizoahidiwa, Nana alikataa kazi hiyo. Nana anatusimulia hali hii kama msanii anavyotuambia:

> …Sikutaka kulazimishwa nyimbo za kuimba- nyimbo za matusi na masimango, nyimbo za mipasho na rusharoho. Nilizizarau mno nyiimbo hizo zisizo mwala wala murua. Zisizofikia viwango na upeo mkubwa wa kisanaa. Pia, sikutaka kulazimishwa kuvaa nguo wanazotaka watu wengine, fupi au ndefu. Nilitaka nivae nguo ninazopenda kuvaa mimi mwenyewe. Basi hatimae nikapasukwa na kicheko cha kejeli tu. Nilicheka tu. Kisha nikamwambia meneja 'asante' sikuwa tayari kuifanya kazi hiyo (uk. 144-145).

Kupitia dondoo hili, tunamuona namna Nana anavyojikengeusha, na kutofautiana na waimbaji wengi wa kisasa waliomo katika jamii zetu leo hii. Ni wazi kwamba, waimbaji hao huwa hawako huru kuchagua namna ya mitindo ya kuimba na hata mavazi. Matokeo yake, waimbaji wengi wa kike leo hii wamekuwa wakipanda katika majukwaa wakiwa wamevaa nguo ambazo haziendani na maadili ya jamii yetu. Waimbaji hawa wamekemewa vikali na Raisi wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kutokana na mavazi yao yasiyoendana na maadili ya Watanzania.

### 4.4.2 Kuonesha Kutojali

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Yungi ni mhusika ambaye amejitumbukiza katika biashara ya ukahaba. Hajali hali hiyo mbele ya wazazi wake na hata kwa jamii. Mama yake, Bi M. anasikitika kwamba, amekuwa akitoka nyumbani na kurudishwa na wanaume huku akiwa amelewa. Aidha, Yungi anasema kwamba, lazima afanye kazi kwa sababu anamuona baba yake hawezi tena kuhudumia familia. Hali hii

inaleta mgogoro mkubwa ndani ya familia ya mhusika Mimi. Hali hii tunaiona kupitia mhusika Bi. M pale mwandishi ananaposema:

> Aliniambia lazima afanye kazi. Wewe eti huwezi tena kuiendesha nyumba hii. Na mimi kizee cha Mungu, tena kwa mwanamke. Alisema kwamba hii ni dunia yao. Dunia ya vijana.”Enh!“Ndiyo.”Kazi gani anafanya?Nilipomuuliza hakujibu. Lakini mimi najua si nzuri, maana anaporudi hapa, wewe labda husikii. Umelala fofofo. Umaji kwa machofu yambio za mchana kutwa na kuambulia patupu. Huja kushushwa kwa gari mlangoni petu. Tena kwa shangwe la mabarubaru na hashuo la majanajari! Kama huo ujanajari umo tena!”Lahaula! Niliduwaa nikaganda hapo. Sikuweza kubanduka. Nilizama juu ya hilo sofa. Nikatia nia kumngojea Yungi arudi (uk. 24).

Maelezo haya yanatuonesha namna mhusika Yungi anavyojikengeusha na jamii ya Waswahili. Katika jamii ya Uswahilni, mwanamke alizoeleka kuwa ni mtu wa kubaki nyumbani, huku mwanamme akiwa ndiye mtafutaji wa huduma za kifamilia. Aidha, mwanamke anatakiwa kujituliza bila ya kufanya ngono, kwani, katika ndoa za uswahilini mwanamke aliyeondolewa ubikra kutokana na uzinzi ni aibu iliyokubwa. Kama anavyolieleza hili Sengo (1992:1), anasema kuwa, ubikra ni ada kubwa sana Uswahilini. Kwani taasisi ya ndoa ni taasisi muhimu katika maisha ya mtu. Hivyo, wazazi, masomo pamoja na makungwi hushiriki katika kuwaelimisha watoto juu ya umuhimu wa ndoa na kutunza ubikra.

Hii ni aina ya ukengeushi ambayo, Mayaka (1991) anaitambua kama Kizindushi, ambapo mhusika hujitenga na kuieleza hadhira yanayoendelea mchezoni ili kuizuia isizugike. Ingawa Mayaka anaona mbinu hii hujitokeza tu katika michezo ya kuigiza, hata hivyo, katika riwaya na hadithi fupi huweza kujitokeza kama tunavyoiona hali hii kupitia riwaya ya *Dunia Yao*.

Vile vile, mhusika Nana katika *Nyuso za Mwanamke* anaamua kujikengeusha, ambapo anahama nyumbani kwao na kujitafutia sehemu nyingine ya kuishi. Hili

linafanyika ili kupata uhuru katika kufanya kile anachokiamini kwamba, ni sawa kwa maisha yake bila ya kuzuiwa na baba yake. Ukengeushi huu unaofanywa na Nana, unaakisi nadharia ya udhanaishi ambayo kama asemavyo Njogu na Wafula (2007), kwamba, binadamu inampasa afanye harakati zozote ili aweze kujitafutia uhuru wake binafsi. Ili kutafuta uhuru wake, Nana anaamua kutengana na familia yake bila kujali. Mwandishi anasema:

> Nana alianza kwa kupigana na nafsi yake na anaendelea kupigana nayo. Kisha akaamua kupigana na mazingira yake ya nyumbani mpaka yakamfikisha kuhama na kutengana na babake. Tena akapigana na kuishi katika mazingira mapya na watu wapya. Akapania kufanya anachokitaka kwa ajili ya kuendesha maisha yake. Ndani ya yote hayo, kama alichokiona Kezilahabi, mna ugumu na maumivu na furaha, mna ugumu wa kutema roho yake mtu na kuisafisha. Yaani maumivu kila siku yana upande wa pili (uk. 222).

Katika dondoo hili, tunaona namna suala la ukombozi wa mwanamke lilivyo na changamoto zake. Ili mwanamke ajikomboe, lazima ajikengeushe na jamii na hata kugoma kufanya baadhi ya mambo ambayo anadhani hayaendi sawa. Kwa sababu jamii imekuwa na mila na desturi zake ambazo zilionekana kukubalika. Kwa mantikihi hiyo, tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi, tunaona kuwa, uhusiano uliopo wa mwanamke na jamii yake ni waunyonyaji na ukandamizaji kwa baadhi ya vipengele vya maisha. Hivyo basi, ili kuondokana na hali hiyo, lazima mwanamke akate jongoo kwa meno na kuamua kufanya mapinduzi yake binafsi.

Aidha, ndoa tunayoiona katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kati ya Nana na Amour, Nana anaonekana kugoma kufuata matakwa ya baba yake ya kuchaguliwa mchumba. Hivyo basi, Nana na Amour wamejikengeusha na utamaduni wa Waswahili. Ukengeushi huu unatokana na vile kukutana kimapenzi baina ya wapendanao. Nana na Amour walitafutana, wakapatana na wakaamua kuishi

pamoja. Bwana Hila alitaka kumuoza Nana kwa Dusa, maana alitoka kwenye familia ya wenye nacho. Hata hivyo, hilo halikufanikiwa. Baadaye, Nana na Amour walikutana na kupanga mapenzi ili wasiwe na shaka na mwingine. Baada ya hapo, ndio wakafunga ndoa. Mwandishi anasema:

> Wametafutana, wamefukuzana mbio kwa masafa ya mbingu na ardhi. Wametazamana kwa mbali kwa miaka hadi wakakutana. Wametishana. Wameogopana. Hata wamekejeliana. Hatimae wamejadiliana na kukubaliana kuanzisha ndoa ya kisasa (uk. 193).

Ndoa inayoelezwa katika dondoo hili, ni ndoa ya kisasa ambayo vijana wengi leo hii hawako tayari maamuzi ya ndoa zao kuwa mikononi mwa wazazi wao. Suala hili wanaliona kwamba, ni sulala la mtu binafsi. Hivyo basi, uhuru wa kuchagua mwenza wa kuishi naye, lazima uwemo mikononi mwa wanandoa wenyewe. Kama asemavyo Ann (2013), kwamba, usasa huu umeleta mapinduzi ya utamaduni wa ndoa katika jamii. Ambapo vijana hutaka kuridhiana kila upande ndio wafunge ndoa zao. Pia, vijana hawataki tena kuchaguliwa wachumba na wazazi wao.

Tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi, ambayo moja ya msingi wake ni kuangalia namna wahusika wanavyoweza kuchambuliwa na hatimae kutoa hitimisho. Hivyo basi, tunapomuangalia mhusika Yungi na Nana wanavyofanya ukahaba, pamoja na ulevi bila kujali kwa kisingizio cha kutaka kujitegemea pamoja na kumaliza masomo bila kupata kazi, jamii ya Uswahilini inalichukulia tukio hilo ni la aibu si tu kwa mtu binafsi, bali kwa familia na kwa jamii kwa jumla. Hapa tunachoweza kusema ni kwamba, jamii haikubaliani na matendo kama haya.

### 4.4.3Matumizi ya mhusika kivuli

Msanii katika riwaya ya *Duni Yao* ametumia mhusika kivuli. Mhusika huyu ni wa ukengeushi kutokana na sifa ambazo zimekiuka uhalisia wa kijamii. Msanii

anamueleza mhusika kivuli kwamba, alikuwa ameshakufa lakini bado aliweza kumuingia mhusika Mimi na kumning`inia kichwani. Hiki ni kivuli cha mhusika Shaibu, ambaye pia, amekuwa akitumiwa na msanii kama mhusika Ye- Mhusika Mimi anatusimulia hali hii kama msanii anaposema:

> Baraza ya taaluma. Tulikuwa Peke yetu. Mimi na Shaib. Ndiye mtu pekee niliyeweza kuzungumza naye hapa. Kivuli chake nakusudia. Siku hizi sisemi na mtu ila na kivuli cha Shaib.Ye-, yaani Shaib, huzungumza nami ingawa simwoni. Alikuwa ameshakufa – kwa maana halisi ya kufa. Lakini bado alikuwa na uwezo wa kuniingia na kuning`inia kichwani. Niliweza kumhisi ndani ya nafsi yangu wakati wowote. Lakini zaidi nilipokaa kwenye baraza hii ya taaluma (uk. 40).

Katika maelezo haya, tunaona namna msanii anavyoakisi matumizi ya mhusika wa kisaikochanganuzi. Ambapo mhusika Shaibu anayewakilishwa na kivuli anaweza kusimama  kama mhusika wa nafsi ya kwanza. Na hivyo, anaposema kuwa, ndiye mhusika pekee anayezungumza naye hasa anapokaa katika baraza ya kitaaluma. Anaashiria kwamba, nguvu za mtagusano kati ya nafsi yake na yale ambayo yamekuwa yakimtokea yeye binafsi, au yaliyowahi kuigusa jamii yake, ndiyo yanayomsukuma kueleza matukio.

Matumizi ya mbinu hii ya mhusika kivuli pia, imetumiwa na mwandishi Said Ahmed Mohamed katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi,* ambapo anamtumia Mtolewa kama kivuli ambacho kimekuwa kikiendeleza mapambano kati ya tabaka tawala la kinyonyaji, dhidi ya tabaka tawaliwa ambalo limekuwa likionewa chini ya utawala wa Bi. Kirembwe.

Tukirejelea nadharia ya Saikochanganuzi ambayo inaongoza utafiti huu, tunaona kuwa, ukengeushi wa aina hii unalandana na matukio ya mtunzi ambayo amewahi kuyapitia katika maisha yake. Wazo hili linakubalika kutokana na namna mhusika

Mimi anavyosimulia masaibu mbalimbali aliyowahi kukutana nayo, yakiwamo kufukuzwa kazi pamoja na kunyimwa haki zake.

Aidha, masikitiko yake juu ya Bara la Afrika kutothamini wasomi. Kwa sababu mtunzi wa riwaya teule ni msomi aliyebobea, ambaye amewahi kuishi nchi za Ulaya, ni dhahiri kuwa, anachokieleza katika riwaya hii ni kubainisha kwamba, kuondoka kwake katika nchi yake hakupenda, bali ni kutokana na msukumo ambao ulitokana na kutotilia maanani wasomi pamoja na haki za watu binafsi. Hivyo basi, riwaya hii imekuja kutoa kilio cha wasomi na jamii kwa jumla dhidi ya tabaka tawala.

Kwa upande wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, pia, mwandishi amejaribu kutumia mhusika kivuli kwa kumtumia mhusika Nana akizungumza na kivuli cha mama yake, huu ni ukengeushi kwa kiasi fulani. Hali hii inatokana na kuwa inaaminika na watu wote ya kwamba, mamake Nana alishafariki dunia, jambo ambalo Nana haliamini, kwani anaona kuwa, anafanya mawasiliano naye kila uchao.Hali hii tunaweza kuiona pale msanii anaposema:

> Mara nyingi hukumbuka pale unapofurutu ada. Pale unapokuja kuninyukua au kunizaba kibao ili kunizindua na hatari inayonikabili. Nami hujua ni wewe, kwani hapana mwingine ambaye angethubutu kunikamata mkono kunivusha barabara ya hatari. Na ingawa hulalama na kulaani huku nasugua mchonoto pajani au shavuni, hujikuta hatimaye nimeonyeka. Nimenusurika. Nimeepuka hatari. Kwa nini basi niwasikilize wao? Kwa nini niamini wewe hupo? Kwa nini nikubali umeshatoweka? Kwa nini nifanye hivyo wakati najua upo nami karibu au mbali? Niking’ang’ania kuwepo kwako watu wote huniona mpumbavu. Huniona nimerukwa na akili. Hunambia nina ugonjwa. Wengi hunicheka na kunijeja. Wachache wanioneao huruma, wao hunionya; “Nana aliyekufa hasimami tena.” (uk.19).

Dondoo hili linatuonesha jinsi Nana alivyoathirika kisaikolojia, kutokana na kutokuwapo kwa mama yake katika mazingira ambayo yeye anaishi. Hali hiyo

inamfanya achanganyikiwe kwa kiasi kikubwa, kwani, imani yake inamlenga aamini kuwa, bado mamake yuhai. Inawezekana mawasiliano hayo wanayafanya kupitia ndotoni, lakini yeye, bila kujua anaona labda ni maongezi halisi. Lakini, huo ni mtindo tu wa baadhi ya waandishi Said Ahmed akiwamo, ili kutaka kujitofautisha na waandishi wengine. Ukengeushi huu huufanya ili kuzipamba kazi zao na kuonekanwa zenye mvuto.

### 4.4.4 Kutokata Tamaa

Bori ni mhusika ambaye alishindwa kuendelea na masomo yake. Mhusika huyu, pamoja na kushindwa kuendelea na masomo yake, hata hivyo, hakati tamaa katika maisha yake. Anaamini kwamba, iko siku ataweza kujikomboa na hali mbaya ya maisha iliyomkabili. Ni mhusika ambaye hakati tamaa na anapambana na hali ya maisha kwa vyovyote vile. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* tunasimuliwa kuhusu Bori ambaye ni mhusika wa kimimikama msanii asemavyo:

> …Njiani, alipishana na kupigana kumbo na Bori. Ghafla, nilimuona Bori, kabeba mredio mbovu ambao sijui kauokota wapi. Kaja kunisimamia na kunitumbulia macho. Haikuwa ajabu kwangu kumuona hivi. Tokea aliposhindwa kuingia darasa la kumi na moja na kutoweza kuendelea mbele na masomo, tabia yake imezidi kuwa ya kichakaramuchakaramu.Uchakaramu wake lakini ulikuwa wa aina mbili: unyamavu na kuokota vitu visivyofaa. Chumba chao kilikuwa kama chumba cha kacharakachara. Kila kitu kimo. Kila kitu kisichofaa. Aliokota tangu vyakula vilivyotupwa mapipani, vipande vya nyuma na visu na vijiko, mpaka mikebe, vibati, nguo, mabuti mabovu, vidani vikuukuu vya kareti na kaure alivyoviona njiani. Vitana na mashanuo yaliyon’goka meno. Betri zilizotumbuka na kupapa rojo. Na kushinda vyote, alipenda kuokota vyombo vya umeme visivyokuwa na haja tena. Tabia yake hii nzima ilinikumbusha bwana mmoja tulieyekuwa tukimwita utotoni, Babu Rokotea. Kila siku Babu Rokotea alikuwa akipita majaani na mkapu wake kuokota viatu… (uk. 110).

Vitendo hivi vya Bori, ni uhalisia wa maisha ya Watanzania ambao wamekosa la kufanya, ili kujikimu na hali ngumu ya maisha. Vijana kama Bori tumekuwa

tukiwaona katika miji mingi. Vijana hao wamekuwa wakiokota taka ngumu ili kuzikusanya na baadae kuziuza ama kuzitumia wao binafsi.

Bori anaonekana kujikengeusha zaidi, kwani anaonekana hachagui hata cha kuokota. Uokotaji wa chakula katika madampo ni dalili ya kuchanganyikiwa. Akishadidia kuwapo kwa hali ngumu ya kiuchumi, Mbogo (2002) anamsawiri mhusika wake Pita Lomolomo akiokota chakula kibovu kilichotupwa kwenye madampo, kutokana na umaskini na ukosefu wa malezi bora.

Tukirejelea nadharia ya Saikochanganuzi tunaona kuwa, mhusika huyu anaendana na hali ya vijana wengi wa Tanzania, ambao wamekuwa wakisoma hadi ngazi za elimu ya juu. Hata hivyo, vijana hao wanapomaliza masomo yao wanashindwa kujitegemea. Vijana hao hubakia mitaani na kujikuta hawana la kufanya. Matokeo yake ni kukata tama na maisha, na hata wengine kujiingiza katika vikundi viovu.

Said Ahmed Mohamed katika tamthiliya ya *Mashetani Wamerudi*, ambapo analaumu mfumo wa elimu wa Afrika na Tanzania ikiwamo kwamba, umejaa wingi wa nadharia ambazo kiukweli hauwezi kumkomboa kijana na kumfanya aweze kujitegemea. Hivyo, anataka tuachane na mfumo huo wa elimu ya kinadharia.

Aidha, Nana anajikengeusha kutokana na suala la uongozi. Tunaelezwa kwamba, Nana amejikengeusha na mikatale ya utamaduni ambayo haikumpa fursa mwanamke kuwa kiongozi katika jamii nyingi za Afrika. Kwa kulibaini hilo, bila kukata tamaa, Nana anavunja mikatale hiyo na anakuwa mwanamke anayepata fursa ya kuchukua uongozi, sambamba na anavyopewa mwanamume. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* tunamuona Nana akijiingiza katika taarab ya biashara, yeye akiwa Mkurugenzi Mkuu. Yeye na Faisal wanashughulikia kuzalisha video, CD na

DVD. Pia, anashughulikia matangazo ya radio ya masafa ya FM. Tunasimuliwa hili kuhusu Nana kama msanii anavyosema:

> Nana siku zote anapoamka asubuhi kabla hajatimka kwenda kutekeleza miradi yake, maswala yake huwa: Nini nataka? Nini nataka kufanya? Kimeshafanywa au hakijafanywa na mtu mwengine ninachotaka kukifanya? Kikiwa kimeshafanywa kakifanya nani? Vipi? Kwa njia na kasi gani? Njia gani nitapita mimi sasa? Nani atanikalia mbele?...Nana alianza kwa taarabu ndiyo, lakini haikuwa taarabu ya kawaida. Ilikuwa taarabu ya biashara, yenye Mkurugenzi Mkuu (yeye mwenyewe) na msaidizi mshauri (Faisal), na ofisi zao na vitengo vya kutolesha video, CD na DVD, vya watembeza biashara ya taarabu wenyewe, vya wahasibu, wakuza biashara hiyo wanaoitwa `promoters`, vya redio yake ya FM ya kutangaza vibao vipya na vikongwe ili kushindana na vibao vya wengine: kwani hii si dunia ya mashindano kupitia vyombo vya habari? Si dunia inayoendeshwa na maajenti wa utandawazi kuanzia ndani hadi nje. Maajenti wa kumpatia na kumtayarishia Nana safari za ndani na nje? Mbali na washauri na mawakili wa kumlinda na unyang`anyi wa ndani na nje (uk. 196-197).

Hivyo, kupitia dondoo hili, tunaona namna Nana anavyojikengeusha na jamii iliyomkuza, kutokana na kujiingiza kuwa kiongozi katika shughuli za kibiashara. Tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi tunabaini kwamba, mhusika huyu ameasi mila na desturi za wanawake wa Uswahilini, ambao kwa miongo kadhaa wamekuwa wakibakia nyumbani na wanaume kuwa na fursa ya kukamata nafasi za uongozi pamoja na kufanya biashara za ndani na nje.

#### 4.4.5 Mijadala ya Nadharia kuhusu Imani

Mhusika Mimi anajadili nadharia za fasihi. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Miza ni mhusika wa kinadharia. Mhusika huyu ni wa kinadharia ambaye anaaminika kwamba huwatia moyo na nguvu waandishi wa kazi za fasihi ili kuandika kazi zao. Mulokozi (1996:4) anasema kuwa, katika jamii za Wayunani inaelezwa kuwa, Muse ni Miungu wa ushairi na muziki amabao yasemekana waliwapa watunzi nguvu za kiroho, kinafsi na kijazba za kutunga. Maandishi ya wasomi wa kale wa

Kiyunanihasa; Hesiod na Plato, yanaanzia kwenye imani hii. Kwa mujibu wa nadharia hii, fasihi imekuwapo tangu kuwapo kwa mwanadamu duniani, haikugunduliwa au kutokea katika kipindi fulani tu cha maendeleo ya mwanadamu, bali ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu.

Katika riwaya hii, Muse anasema kwamba, kwa asili, hasa ni Ugiriki, lakini leo hii amekuwa akionekana kila pahali. Ukengeushi huu unajitokeza kutokana na riwaya hii kuwa na sifa za riwaya ya kisasa. Ambazo, kama asemavyo Wamitila (2013:5), kuwa, riwaya hizi zimekuwa na sifa ya usimulizi uliokiuka mipaka ya urazini na ujarabati wa kawaida. Matukio mengi yanavuka kiwango cha kawaida. Msimulizi anayesimulia matukio katika riwaya za aina hii, haelekei kushangazwa na matukio yasiyokuwa ya kawaida, na kwa kiasi kikubwa anamtarajia msomaji wake akishangazwa nayo. Msomaji anashawishiwa na msimulizi kukubali kuwa, matukio yaliyomo katika ulimwengu wa hadithi ni matukio ya kawaida, licha ya kwamba, yanakiuka kanuni za kawaida anazozifahamu kutokana na uzoefu na tajriba yake kwenye ulimwengu halisi.

Hali hii anayoileza Wamitila (khj), ndiyo ya ukengeushi wa mhusika Muse katika riwaya ya *Dunia Yao*. Kwa kawaida, si hali ya kawaida kumuona Mungu amekaa na kujitokeza katika ulimwengu wa kiuhalisia, huku akijadiliana na waandishi ambao wanaandika kazi za fasihi, kama tunavyooneshwa kikao hicho kati ya mhusika Mimi na Muse. Hali hii inaelezwa na msanii hivi:

> Mimi ni Muse," alipokwishaniketisha aliniambia kwa sauti yake, sauti tamu ajabu."Unatoka wapi?" nilimuuliza."Kwa asili hasa, Ugiriki-lakini siku hizi naishi popote. Mara nyengine hujificha katika vina virefu vya ardhi kabla sijachomoza kumdhuru niliyemchagua. Na leo nimekuchagua wewe. Kwa hivyo, nimechomozekea chini ya mnazi palipofukiwa kitovu chako baada ya kupiga mbizi Bahari ya Hindi kuja kukuingia kichwani mwako…(uk. 61).

Hapa msanii anatusimulia na kuchopeka nadharia ya chimbuko la fasihi ulimwenguni. Nadharia hii ni nadharia ya Wigo, kama tulivyokwisha ijadili hapo juu. Ni wazi kwamba, kama riwaya nyingine za kimamboleo za Kezilahabi, riwaya za *Nagona* na *Mzingile* ambazo zimetumia mtindo wa kujadili baadhi ya nadharia. Riwaya ya *Dunia Yao* nayo inajadili nadharia, hasa zile zinazohusishwa katika uchambuzi wa kazi za fasihi ulimwenguni. Pia, mhusika Mimi anajadili nadharia ya Udhanaishi ambayo inaelezwa na Njogu na Wafula kwamba, moja kati ya msingi au mhimili wake, ni kuchunguza maana ya maisha. Hivyo basi, hakubaliani na Kezilahabi ambaye anaamini kuwa, maisha ni fujo. Mhusika Mimi anatusimulia hayo pale msanii anaposema:

> Ingawa najua hata na mimi nimeshakufa, ukweli ni kwamba siamini juu ya fikra ya kwamba maisha tunayoishi yanatustahiki. Dunia si uwanja wa fujo! Si zogo lisilosarifika. Sikubaliani na Kezilahabi. Namjua anayeharibu. Namwona akisukuma watu katika lindi refu. Uchungu wangu ni kwamba siwezi kumzuia. Wala siwezi kumvamia kutumbukia naye pamoja. Nimebaki kuning`inia ukingoni nikishikilia hodari huku jinamizi, kwa guu lake, linanikanyaga. Linanitimba. Linanipondaponda. Linanididimiza kooni pangu. Pumzi zinaziba. Ninapiga kelele. Sauti haitoki. Lakini pamoja na yote hayo najua hilo ni jinamizi tu. Na jinamizi limo ndani tu, na ndoto imo usingizini, na usingizi una mwisho. Jinamizi litakwisha kila mtu atakapoamka (uk. 144-145).

Kwa upande wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, mwandishi hakuwa nyuma katika kuonesha mjadala wa nadharia ya Saikochanganuzi, kwa kumtumia mhusika Nana akiwa katika hali ya udodosi nafsi kama msanii anavyosema:

> La muhimu ni kuwa sijafa. Nimebaki mimi Nana. Mimi mwanamke. Binti. Kijana mwenye roho ya kimamboleo na tama ya kesho. Nimebaki ingawa katika kijisehemu kidogo kilichobaki. Yatosha. Nitakiimarisha. Kile kijisehemu cha roho yangu kilichoachwa ndani ya ufu wangu. Hapo nilikishika kijisehemu hicho, maana nilijua kilikuwa fumbu la uhai wangu. Kilianza kunitonesha kijisehemu hicho. Nikajijua nihai kwa vile sasa nilihisi nafsi yangu inaanza kunikandamiza kwa masuala yasiyo na majibu. Mimi nani? Natoka wapi? Nakwenda wapi? Nitakuwaje kesho? Hapa wapi nilipo? Nini maana ya baba au mama? Nini maana ya kwetu? Nini maana ya nchi yangu? Ndani ya masuala haya nilitambua kwamba

> mna hofu. Hofu. Wasiwasi. Woga. Nasikia kwamba woga ndio kiini kikubwa cha maangamizo ya binadamu na dunia yake hii sijui kama ni kweli (uk.61-62).

Dondoo hili linatudhihirishia namna gani mwandishi anavyoonesha ubobevu wake katika kusana kazi zake, huku akichopeka nadharia za kifasihi, ambapo anamuonesha mhusika Nana akianza kuidodosa nafsi yake kwa maswala mbalimbali, ili kutaka kujua yeye ni nani? yuko wapi? baba na mama yake ni nani? Na mambo mengine ambayo yanatumiwa na waandishi mahiri katika kuzifanya kazi zao ziwe na vionjo vyenye kumvutia msomaji.

### 4.4.6 Kushiriki Ngono

Wasichana wengi wamekuwa wakijikengeusha na utamaduni wa Mwafrika kwa kufanya ngono kabla ya kuolewa. Wasichana wamekuwa wakitumbukia katika wimbi hili la mapenzi holela kutokana na sababu kadhaa, ikiwamo hali ya umaskini. Ili kutatua tatizo la umasikini, wanajitumbukiza katika vitendo hatari vya uasharati. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, Msanii anatusimulia ukengeushi huu unaofanywa na wasichana kwa kusema:

> …Kisha huzuka changudoa wa miaka kumi na mitatu kumi na minne waliosheheni ndani ya majumba ya ngono wanamotakiwa kulipa madeni yasiyomaliza waliyokopeshwa na ma-Gangster au ma –Mafya wa huku. Kisha waliwatokezea NGOs wanaowaonea huruma wanawake wasiojua kujionelea wala kujitetea wenyewe.Alizisikia sauti zinazopinga ngono kwa kukaribisha ngono. Fashion za tumbo-cut na fundi –kasahau –mshono, na Rap za vijana kukobeana na mipasho ya kutukanana. Hizo ni feshini tu, huo ni usasa, huo ni utandawazi wewe mpumbavu Nana. Tumia soksi tu. Endeleza utamaduni wa ngono. Aliisikia sauti yake mwenyewe ikimsusuika Nana.Ilikuwa kama Nana akiisikiliza sauti yake ikigombana na nyingine-Hauhusiani usasa na ukimwi wewe. Ukimwi utaondoka kwa kuvaa soksi na mawaidha ya kuhimiza soksi kwenye vyombo vya habari. Ukimwi utaondoka kwa wingi wa fedha na misaada inayotoka nje (uk. 181).

Katika dondoo hili, tunaona namna wasichana wanavyojikengeusha na utamaduni wetu kwa kujiingiza katika ngono. Hali kama hii, tunaiona katika riwaya ya *Dunia*

*Yao* ambapo msanii anatusimulia namna wasichana wawili walivyokuwa wakipigana kutokana na kujipendekeza kwa wanaume ambao wamekuwa wakifanya nao ngono. Msanii anatusimulia kwa kusema;

> Mbele zaidi wasichana wawili waliowekeana chuki na visasi kwenye Mipasho au Rusharoho majuma kadha yaliyopita, leo walikuwa wakizitoa chuki na visasi vyao hadharani kwa vitendo. Walikuwa wakigaragazana topeni na halaiki ya watu inatazama sinema ya bure. Hakuzuka mtu yeyote aliyeingilia kati kukemea au kuamua. Hata mimi niliyechukia picha hii. Nilijifunza kuepuka mambo ya watu siku hizi baada ya kukumbwa na balaa mara nyingi nilipojifanya mwamuzi. “Yale ya majuzi hayakutosha? Alilaumu mwanamama wa kwanza.“Wewe ndiye uliyeanza kwa kutukamatisha polisi.”“Mimi au wewe, uliyekosa adabu… uliyenivamia mbele ya wakubwa…”Nilisikia zamani habari hii ya wanawake kutukanana na kupigana mbele ya wakubwa, lakini haikunishangaza…”“Babu we` utakoma kututambia… nilikwambia zamani huna namba.”“Khhh, una nini? Hakuna asiyejua kwamba wimbo wa C. Licence shoga yako kaliimbia buzi langu.  Imehusu nini? Utamuona vivi hivi Mcha. Dereva wangu yule babu… kama mlivyomchukua TX wetu, utafanya nini kwani?”“Take care!” (uk. 33).

Haya ni mabadiliko ambayo yameikumba jamii miongoni mwa wasichana. Ngono holela kama hizi, ndizo ambazo zinasababisha ongezeko la magonjwa ya zinaa kama vile, Ukimwi. Kama ilivokwishaelezwa na Ali (2015), kwamba, wanawake wengi leo hii wamekuwa na tabia ya kufanya mapenzi nje ya ndoa bila kujali athari zake.

Mwangwi tunaoupata kupitia mawazo ya Nana na wasichana hawa, yanayowasukuma kujiingiza katika ngono, yanalandana na nadharia ya Saikochanganuzi ambapo;*Id*na *Ego* zinamsukuma aingie katika mtego huo, bila kujali gonjwa hatari la Ukimwi. Kama asemavyo Njogu na Wafula (2007), kwamba, katika Saikochanganuzi,*Id* na *Ego* humsukuma mtu kufanya matendo kwa kutumia utashi bila ya kujali na kuchunguza kwa kina athari zake.

### 4.4.7 Kupenda Usasa

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, Nana, Amour na Faisal walifanya tafrija kubwa. Mathalani, usiku saa mbili kulifanyika karamu ya ndoa, ingawa ilitatizwa na habari mbaya ya kuungua moto kwa jumba la Nana. Burudani pia, ni jambo linaloenziwa na wengi. Burudani zenyewe zilifanyika hotelini. Mathalani, Amour walikutana hotelini Samra kwa mazungumzo na Nana (uk.56).Pia, msanii anaonesha vile Nana na Faisal baada ya mazoezi wakirudi hotelini Mizengwe kwa burudani (uk.132). Uimbaji kama kadhia ya burudani ulifanywa kwenye hoteli ya *Five Stars* na hoteli *Selwa*.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* tunamuona namna Yungi anavyojikengeusha na jamii kutokana na kupenda starehe na kung`ang`ania usasa. Tuanaelezwa kuwa, alikuwa anatoka wakati wa usiku na kurudi usiku wa manane, akitokea katika vilabu vya starehe. Katika vilabu hivyo, alikuwa analewa bila kujali kwamba, hapaswi kuwa na tabia kama hizo (uk. 38).

Huu ni ukengeushi wa vijana wengi leo hii pamoja na jamii kwa ujumla. Hali hii husababisha upotevu mkubwa wa pesa. Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba, huu ni uharibifu wa pesa. Kama asemavyo Salim (2015), akifanya uchambuzi wa maandishi ya Shaabarn Robert katika riwaya ya *Kusadikika* kwamba, twaoana kila siku na kuzaana kila siku, lakini watoto wetu hatuwalei kiungwana. Mali zetu nyingi zinamalizikia katika ngoma na tafrija mbalimbali. Tunakubaliana na mawazo ya Shaabarn Robert (khj) kwamba, tafrija kama hizi ni utumiaji mbaya wa pesa. Leo hii tunapokuwa na arusi hata walalahoi hukopa pesa nyingi ambazo hawana uwezo nazo, ili kufanya sherehe za ngoma. Mara tu baada ya sherehe hizo, kinachobakia ni deni pamoja na masikitiko.

#### 4.4.8 Kutumia Ulevi

Vijana wetu wamekumbwa na suala baya la mihadarati. Kwa mfano, katika *Nyuso zaMwanamke* mhusika Ngware kijana wa Bi. Chuma. Tabia zake potovu za kuiba na ugomvi, zilisababishwa na kiu ya mihadarati. Ilimbidi aibe chochote kile hata kwa nguvu, kama alivyotaka kuchukua kidani cha Bi. Mau (nyanyake), ili auze apate pesa za mihadarati. Ngware alikuwa amepewa nasaha na kuonywa aache tabia hiyo, lakini alikataa katakata, kwa kujua aliyemnasihi kuacha alikuwa ni mwanamke, kulingana na yeye (Ngware), mwanamke hawezi kumtisha mwanamume. Kuhusiana na Ngware, mwandishi anasema:

> Kwa muda mrefu amenasihiwa na kila mtu katika jumba hilo: na Bi Chuma mamake, na Bi Mau bibi yake, hata na ndugu zake wa kike pia. Kwa hakika alinasihiwa na kila mtu aliyekuwa akiishi humo, lakini hakusika. Hata hivyo, hakuacha uafiriti wake…(uk. 275).

Pia, suala la vijana kujiingiza katika ulevi tunaoneshwa katika riwaya ya *Dunia Yao*. Tunaelezwa kwamba, Yungi alikuwa akitoka na vijana wengine kuenda katika vilabu vya usiku na anaporudi huwa tayari ameshalewa. Yungi hakuwa anajali mbele ya wazazi wake kutokana na tabia hii ya ulevi. Badala yake aliona kwamba, yuko sawa kwa yale anayoyafanya. Msanii anatusimulia kwa kusema:

> Aliniambia lazima afanye kazi. Wewe eti huwezi tena kuiendesha nyumba hii. Na mimi kizee cha Mungu, tena kwa mwanamke. Alisema kwamba hii ni dunia yao. Dunia ya vijana."Enh!"Ndiyo."Kazi gani anafanya?Nilipomuuliza hakujibu. Lakini mimi najua si nzuri, maana anaporudi hapa, wewe labda husikii. Umelala fofofo. U maji kwa machofu yambio za mchana kutwa na kuambulia patupu. Huja kushushwa kwa gari mlangoni petu. Tena kwa shangwe la mabarubaru  na hashuo la majanajari! Kama huo ujanajari umo tena!"Lahaula! Niliduwaa nikaganda hapo. Sikuweza kubanduka. Nilizama juu ya hilo sofa. Nikatia nia kumngojea Yungi arudi (uk. 24).

Hali kama hii ya mhusika Ngware na Nana, tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi na kuangazia mhimili wa kuangalia matukio ya kijamii tunaona kwamba, vijana wameathiriwa na tatizo la ulevi. Kilio kikubwa kimeikumba jamii

na taifa kwa ujumla, hali hii inatokana na kupotea kwa vijana ambao ni nguvu kazi kwa kusukumwa na tatizo la ulevi.

### 4.4.9 Uongozi Mbaya

"Mwamba ngozi huamba upande wake." Huu ni msemo unaodhihirisha ubinafsi na ufisadi wa baadhi ya viongozi ambao matendo yao huwa ya kujinufaisha tu, pasi kujali wenzao. Jambo hilo linaendelezwa hata hivi sasa na limekuwa suala sugu. Katika *Nyuso za Mwanamke,* Bwana Hila (babake Nana), anafanya ufisadi uliokithiri. Hili linadhihirika kupitia jengo alilolijenga kwenye shamba kubwa mno, kwa kuwalaghali wakulima waliomuuzia vipande vidogovidogo na mwishowe wakawa wamesukumwa nyuma kabisa na kuwa mbali na jengo hilo. Kilichobaki kusikika, ni sauti za mbwa wakibweka pamoja na sauti za televisheni, video na redio, au vicheko siku ya sherehe. Isitoshe, wakulima na walalahoi hao, hawangekaribishwa kwenye sherehe zilizofanywa kila uchao nyumbani kwa Bwana Hila, walibaki kunusa harufu ya vinono tu. Kuhusu hili, mwandishi anasema:

> Nyumba hii kila jambo sherehe. Hata mtu akiingia msalani au akitoka-sherehe. Wala si uongo, sherehe zilikuwa kiburudisho chetu. Na sherehe zenyewe zote hazikuwa ndogo. Zilikuwa kubwa, nene, pana, ndefu, zilizonyooka na kujaa-zilizonona vyakula, vinywaji, mapambo, kivazi na fahari. Zilizofufurikwa waalikwa walioarifiwa kwa kadi, kwa simu au kwa mdomo; marafiki, wahisani, maafisa, wanasiasa na wafanyabiashara wenzake baba; majirani, ndugu, wanafunzi wenzangu, shoga wa mamangu wa kambo na shoga zangu mimi na wenzi au waliotuhusu sote. Wote, hakusahauliwa hata mmoja. Kwa jumla, watu wote hao na zaidi ya hao walikuwa wageni wetu siku ya sherehe- siku ya *party*. Kulikuwa hata na wale walioalikwa kutoka nje ya nchi kwenye zile zilizonuiwa kuwa *party* kubwa kuliko zote miongoni mwa *party* zetu. Mradi tu wawe watu wakubwa kama sisi. Hakuna mchochole aliyealikwa kwenye sherehe hizo, isipokuwa watumishi wetu ambao walikuwa si watumishi mburumatari kama watumishi wa watu wengine wasiojipata kama sisi (uk.31).

Aidha, bwana Hila alikuwa amejaza taa nyingi kwa fujo kwenye jumba lake, wakati taa hizi zikiwaka kwa kukonyezana, hapo karibu kwenye vitongoji vya walalahoi giza nalo ndilo lililowatawala. Huu ni ubinafsi usiomithilika. Utajiri wa Bwana Hila alikuwa ameupata kupitia njia za ufisadi, na ndio maana alibadhiri mali kwa sherehe nyingi za kila aina, maana fedha hakuzipata kwa jasho lake, bali kwa hila zake. Alisahau kuwa, "Msitu mpya komba wapya," utawala mpya usiobembeleza mafisadi na wenye uroho haungempa nafasi. Ama kweli, "Mpanda ngazi hushuka," bwana Hila alifutwa kazi. Ubinafsi pia, umekithiri miongoni mwa wazazi wanaopotoshwa na dhana ya mali wakati wa posa au uchumba wa mabinti zao.

Pia, kwa upande wa riwaya ya *Dunia Yao*, tunaelezwa namna viongozi walioshika hatamu walivyokuwa hawajali wananchi. Kutokana na hali hii, viongozi wengi wa bara la Afrika wamekuwa Miungu watu. Wamekuwa wakichukua kila kitu kutokana na ubinafsi walionao. Aidha, kutokana na ubaya wao, wamekuwa wakikiuka haki za kibinadamu na matokeo yake ni kutawala kimabavu. Viongozi hawa, kila kitu huwaamulia tu wale waliochini na kulazimisha kutekelezwa kama wanavyotaka wao. Hali hii hufanya waonekane kwamba, kila kitu wanakijua wao. Hivyo basi, ushauri wa wale waliochini hausikilizwi. Tunaelezwa hili na mhusika Mimi pale msanii anaposema:

> Najua mimi…najua kwa nini hutaki kubadilika mtu wewe? Hata wahakiki wako wanakusema…Naam, kama unavyojua. Nilijua anatambua. Kimya.Wamechukua kila kitu! Niliendelea. Wao wamekuwa ndio wafikiri wetu. Wasemaji wetu. Watendaji wetu. Wanaohisi kwa ajili yetu. Waona njaa na kiu zetu. Walimu, madaktari, wanafalsafa, wanauchumi, mashehe, mapadri na walinzi wetu. Kwa jumla waendesha maisha yetu yote. Sehemu za viwiliwili na akili zetu. Kwa ufupi wao ni kila kitu chetu! Sisi wengine ni mapipa matupu. Hatuna rojo la uhai. Hatuna supu ya maisha. Wala nyama ya ubinadamu. Hatuna sehemu ya utu. Hatuna rai. Hatuna maoni. Hatuna chetu. Hatuwezi kufikiri kama wao au zaidi ya wao. Hatutarajiwi kusema. Hatutarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi yetu…(uk. 43).

Kutokana na hali hii, inayoelezwa katika dondoo hili, kuna baadhi ya watu huamini kwamba, bado uhuru wa bara hili haujazaa matunda. Hii inatokana na viongozi wetu kuvaa viatu vya kikoloni. Jambo ambalo, huendeleza ukandamizaji na unyonyaji wa tabaka la chini. Kutokana na kutothaminiwa utu wa mtu hata kwa masuala ya mtu binafsi.

### 4.4.10Kukithiri kwa Utabaka

Ann (2013) anasema kuwa, utabaka ni hali inayojitokeza katika jamii ambapo watu hujigawa kulingana na mali waliyonayo, elimu, madaraka kazini ama imani za dini. Kujigawa huko ndiko hujitokeza utabaka. Kati ya matabaka mengi yanayoshuhudiwa katika jamii, tabaka la wenyenacho na wasionacho ndilo linaloshamiri sana, ikawa hakuna maelewano kati ya matabaka haya mawili. Maisha ya leo yameshamiri matabaka ya kila aina.

Katika riwaya ya *Nyuso za mwanamke*,upekee wa wahusika wa kimimi unajitokeza katika hali yautabaka. Upekee huoumedhihirika kupitia maisha ya Bwana Hila, Nana na Faisal. Mwandishi anaeleza namna mhusika Nana anavyoshangaa kuona kwamba, baba yake kahama mtaa wa kifahari wa Mabwanyenye uitwao Chukuachukua na kuhamia mtaa wa Madongoporomoka wa Walalahoi. Baba yake alifia ndani ya nyumba na sio hospitali, maanake pesa za matibabu zilikuwa haba. Hili linatokana na uharibifu wa pesa alioufanya bwana Hila. Msanii anasema:

> Aaa, siwezi kuamini? Baba kafilisika?Kwa nini huwezi kuamini? Ndivyo ulivyo mfumo huu mzima tunaoupenda. Ukiwa na nguvu utadumu, ukikosa nguvu utaangamia. Na si unamjua baba yetu alivyozoea fahari na makubwa na kwa sababu elimu yake ndogo na tena kicwa-mchungwa aliendelea kufanya aliyoyapenda yeye mwenyewe tu. Hatungelimuasa, angelikuona wewe huna akili (uk. 305).

Wakati akiwa na uwezo, bwana Hila alifanya sherehe nyingi mpaka zikakosa maana. Hakuwahi kuwaalika walalahoi majirani zake. Aliowaalika walikuwa watu waliotajika na wenye mali kama baba Dusa. Bwana Hila anatueleza kama msanii anavyosema:

> "Na wewe unamthamini huyu mpiga-gita badala ya mtoto wa mfanyabiashara mashuhuri – unamwambaa Dusa! Kwa nini unathamini takataka, tena takataka zinazotupwa jaani" (uk. 47).

Kwa upande mwingine, Nana na Faisal waliishi mtaa wa kifahari ulioitwa Mnyongehajengi, ili kuonesha kuwa, pesa walikuwa nazo za kuwatenganisha na walalahoi. Mwandishi ametumia mfano wa dunia ya Chukuachukua, dunia ya Sambejambe na Kwawazingapole. Chukuachukua ina migao midogo ndani yake. Kwanza, matajiri waliopindukia amewaita walio haihai, na matajiri wa kadiri waliohai wamekufa. Nako, Sambejambe ndiko umaskini ulikokithiri hadi kutia kitu mdomoni ni kwa kubahatisha. Dunia Kwawazingapole ni wale walioenda jongomeo tayari. Hali hii inaelezwa na mwandishi kama ifuatavyo:

> Dunia ninayoifuata imegawika sehemu tatu. Kwanza: dunia ya chukuachukua, ambamo walio hai hai huishi. Hii nayo si hali moja imegawika viapndevipande. Ndani yake wanaishi hao walio hai hai, na wale walio hai wamekufa. Wale wanaojidai tu wahai. Hata hivyo, ndani ya dunia hii mna wingi wa watu waliojaa hofu ya kukosa mkate wa leo sikwambii wa kesho ingawa mikate imejaa tele madukani…(uk. 87).

Kwa upande wa riwaya ya *Dunia Yao,* tunaelezwa namna viongozi na wenye nacho wanapojaribu kwa maksudi kujitenganisha na watu wenye kipato cha chini. Wanaonesha dhahiri kuwatenga watu wa kawaida, bila wao wenyewe kujitambua. Lakini, kama waswahili wasemavyo, "Shida haizoeleki," mwisho wa siku wanajitambua kuwa, wamekuwa wakinyonywa na kutengwa na mabwana wakubwa hao wenye nacho. Msanii anasema:

> Mwisho wa yote nilikuja kutambua maana vivuli kukimbiana. Hasa vivuli vya watu waliokuwa na nyadhifa kubwa zamani. Walea ambao sasa

> wameporomoka kama mimi. Hivi vilikuwa vivuli vilivyojitahidi zaidi na zaidi visionekane, isipokuwa vilipokuwa na haja. Wengi wetu tuliokuwa miaka saba iliyopita, tukining'inia hodari katikati- pale mabwana wakubwa walipokuja kukata miguu ya ngazi zetu…Ilikuwa kama sisi tunatiwa pumzi za kujichukia. Kila tulipozidi kuvimbiana kwa unene wa pumzi tupu, ndipo tulipojikataa zaidi. Kama watu tulioamka kutoka ndoto ya jinamizi na kujisahau na hatimaye kujiuliza: sisi nani? Asili yetu ipi? Tunatoka wapi? Tupo na tunaelekea wapi? (uk.29).

Tukirejelea nadharia ya Saikochanganuzi inayoongoza utafiti huu, tunaona kwamba, inalandana na hali ya maisha ya jamii nyingiz za Afrika, hasa wakati huu tulionao. Jamii imegawanyika katika matabaka. Maingiliano kati ya matabaka ya wenye nacho na wale walalahoi ni madogo sana. Thamani ya walalahoi mbele ya wale wenye nacho nindogo, ama haipo kabisa. Pia, jamii imejenga tabia ya kujikengeusha hata katika kujenga nyumba zao. Yapo maeneo maalumu ambayo huonekana walala hoi. Maeneo haya hutambulika kama maeneo ya Uswahilini. Aidha, yapo maeneo ambapo hujenga wale wenye nacho. Kutokana na gharama za viwanja pamoja na ujenzi wa majumba hayo au kodi kubwa, walalahoi hawawezi kuishi mazingira hayo.

**4.5Hitimisho**

Katika muktadha huu, tulilenga kulifikia lengo mahsusi la pili la utafiti huu. Lengo hilo lilikuwa ni kufafanuaupekee wa wahusika wa kimimi katika kujikengeusha kwao na jamiiiliyochorwa na mwandishi. Ambapo, mifano tuliyochukua ni kutoka katika riwaya ya *Dunua Yao* na *Nyuso zaMwanamke* zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Tumegundua kuwa, mwandishi huyu anapoandika kazi zake, huwa anakusudia kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Mara nyingi hupenda kujitofautisha na waandishi wengine katika kusawiri maudhui yake. Aidha, tumebaini kuwa, kumekuwa na hali ya upekee juu ya mambo mbalimbali

yanayomfanya mwandishi huyu aweze kuwasawiri wahusika wake wakiwa ni wenye kujikengeusha.

Hatahivyo, miongoni mwa mambo ya ukengeushi yanayofanywa na wahusika ili kuonesha upekee, ni pamoja na baadhi ya wahusika hao kugomea chakula. Mathalani, amewatumia wahusika Nana na Ndi (Mimi) wakiwa katika mgomo huo. Kadhalika, miongoni mwa mambo mengine tuliyoyabaini, ambayo yanaonesha upekee wa wahusika ni kama vile; kuonesha kutojali, matumizi ya mhusika kivuli, kutokata tamaa, mijadala ya nadharia ya fasihi, kushiriki ngono, kupenda usasa, uongozi mbaya, kutumia ulevi na kukithiri kwa matabaka.

### 4.6 Sababu za Wahusika Kujikengeusha katika Riwaya Teule

Tukiwa katika mwendelezo wa kumwangalia mwandishi Said Ahmed Mohamed, tumetumia sehemu hii kwa madhumuni ya kukamilisha lengo mahsusi la tatu la utafiti la utafiti huu. Lengo mahususi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni "Kutathmini sababu za wahusika wa kimimi kujikengeusha katika jamii iliyochorw na mwandishi." Data tulizozikusanya zinaonesha kwamba, suala la ukengeushi wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Yao na Nyuso za Mwanamke*linatokana na sababu kadhaa, miongoni mwazo ni kama vile; ukosefu wa ajira, utandawazi, ukombozi wa mwanamkwe, siasa, utamaduni, habari na mawasiliano na usomi. Hali hizi zinajidhihirisha kama ifuatavyo:

#### 4.6.1 Ukosefu wa Ajira

Katika riwaya ya *Dunia Yao*,tunamuona Yungi, mhusika wa kike ambaye amesoma shule na kuhitimu masomo yake. Hata hivyo, kutokana na hali ya ukosefu wa ajira anabakia nyumbani hana la kufanya. Hivyo basi, anaamua kujikengeusha na jamaii kwa kujiingiza katika masuala ya umalaya. Anajikingia kifua kwa kudai kwamba, tangu amalize masomo yake hajapata kazi yoyote ya kufanya. Pia, Bori anaamua kuokota vitu majalalani akiamini kuwa, iko siku atajikomboa. Mwandishi anasema:

> Ghafla, nilimuona Bori, kabeba mredio mbovu ambao sijui kauokota wapi. Kaja kunisimamia na kunitumbulia macho. Haikuwa ajabu kwangu kumwona hivi. Tokea aliposhindwa kuingia darasa la kumi na kutoweza kuendelea mbele na masomo, tabia yake imezidi kuwa ya kichakaramuchakaramu….Chumba chao kilikuwa kama chumba cha kacharakachara. Kila kitu kimo. Aliokota tangu vyakula vilivyotupwa mapipani, vipande vya nyuma na visu na vijiko, mpaka mikebe, vibati, nguo, mabuti mabovu, vidani vikuukuu vya kareti na kaure alivyoviona njiani, vitana na mashanuo yaliyong'oka meno. Betri zilizotumbuka na kupapa rojo. Na kushinda vyote alipenda kuokota vyombo vya umeme visivyo na haja tena (uk.110).

Vilevile, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*,tunaona kutokana na ukosefu wa ajira, wanawake hujikuta wakijikengeusha katika maisha yao ya kila siku. Ili kutatua hali ngumu ya maisha, wanawake wanajikuta wakijiingiza katika biashara ya ngono. Kuhusu suala hili msanii analieleza kwa kusema:

> Kisha huzuka changudoa wa miaka kumi na mitatu kumi na minne waliosheheni ndaniya majumba ya ngono wanamotakiwa kulipa madeni yasiyomaliza waliyokopeshwa na ma-Gangster au ma –Mafya wa huku. Kisha waliwatokeza NGOs wanaowaonea huruma wanawake wasiojua kujionelea wala kujitetea wenyewe. Alizisikia sauti zinazopinga ngono kwa kukaribisha ngono. Fashion za tumbo-cut na fundi –kasahau –mshono, na Rap za vijana kukobeana na mipasho ya kutukanana. Hizo ni feshini tu, huo ni usasa, huo ni utandawazi wewe mpumbavu Nana. Tumia soksi tu. Endeleza utamaduni wa ngono. Aliisikia sauti yake mwenyewe ikimsusuika Nana. Ilikuwa kama Nana akiisikiliza sauti yake ikigombana na nyingine- Hauhusiani usasa na ukimwi wewe. Ukimwi utaondoka kwa kuvaa soksi na mawaidha ya kuhimiza soksi kwenye vyombo vya habari. Ukimwi utaondoka kwa wingi wa fedha na misaada inayotoka nje (uk. 181).

Kama inavyojidhihirisha katika dondoo hili, suala la ukosefu wa ajira limekuwa likiwasukuma wanajamii kujikengeusha na kujiingiza katika vikundi viovu. Vijana wamekuwa wakishiriki katika wizi, ujambazi pamoja na ngono, ili kutatua hali ngumu ya maisha iliyowakabili, bila ya kujali kwamba, kufanya hivyo kunaweza kuwaingiza katika janga hatari likiwamo kupata maambukizo ya virusi vya Ukimwi, kwenda chuo cha mafunzo na hatakupoteza maisha yao.

### 4.6.2 Athari za Utandawazi

Utandawazi ni uhusiano wa kimataifa wa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni usio na mpaka baina ya mataifa kutokana na urahisi wa mawasiliano uliosababishwa na teknolojia ya habari (BAKIZA, 2010). Sula la utandawazi limeikumba jamii ya Afrika hasa wakati huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Wimbi la vijana kutaka uhuru bila ya kuzingatia miktadha ya kijamii limeongezeka kutokana na kuiga Umagharibi.

Katika riwaya ya *Dunia Yao*, tunaelezwa namna utandawazi unavyomsukuma Yungi kufanya atakalo bila ya kuingiliwa na baba yake kwa sababu za kiutamaduni. Yungi anamkosoa baba yake kwa kuendelea kung`ang`ania kutomruhusu kufanya atakavyo. Mhusika Mimi anaona kwamba, yote hayo yanatokana na nguvu za utandawazi. Mhusika Mimi anatusimulia hili kwa kusema:

> …Lakini nilijua ni vigumu kwa vijana hawa kufahamu hatari iliyomo ndani ya usasa wanaoutaka. Na wao hawalaumiki, ukitazama kasi ya mambo ya usasa na utandawazi inavyosonga. Yetu si yetu tena; ya wenzetu ndiyo tunayoyafanya yetu. Tukitaka tusitake. Mabaya au mazuri! Lakini mimi nani? Baba. Baba maana yake nini? Kitambuzi kidoooogo! Labda! Hata maoni hayo pia nilikuwa na wasiwasi nayo… (uk. 26).

Pia, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, nyimbo za muziki wa taarabu katika jamii ya Nana zilionekana za thamani ndogo, na hivyo kupuuzwa. Nafasi hiyo ilichukuliwa na muziki wa *hip hop,* au muziki wa *rap* na wenye arki za Kimarekani ndio ambao ulithaminiwa(uk. 140). Aidha, Pamoja na kuwa, Nana ni mkereketwa wa usasa na mwimbaji alietakiwa kuimba kwa mtindo wakisasa, ambao nyimbo zake ni zenye mwelekeo wa mipasho ya matusi, misubukuo, tashtiti na kung'ong'ana vichwa. Hata hivyo, Nana anakataa vikali masharti hayo. Hili linaonekana wakati Nana anapokwenda kwa Meneja, ili kufanyiwa usaili iwapo anafaa kuwa muimbaji au hafai. Nana anasema hayo pale msanii anapotuambia:

> …Sikutaka kulazimishwa nyimbo za kuimba- nyimbo za matusi na masimango, nyimbo za mipasho na rusha roho. Nilizizarau mno nyimbo hizo zisizo mwala wala murua. Zisizofikia viwango na upeo mkubwa wa kisanaa. Pia sikutaka kulazimishwa kuvaa nguo wanazotaka watu wengine, fupi au ndefu. Nilitaka nivae nguo ninazopenda kuvaa mimi mwenyewe. Basi hatimae nikapasukwa na kicheko cha kejeli tu. Nilicheka tu. Kisha nikamwambia meneja 'asante' sikuwa tayari kuifanya kazi hiyo (uk. 144-145).

Utandawazi uliolikumba bara la Afrika, kama unavyoelezwa katika dondoo hilo hapo juu, umewagawa wanajamii. Wapo wanaouchukulia kuwa ni mzuri moja kwa

moja, wakisukumwa na utashi wa*Id* katika nadharia ya Saikochanganuzi, na wapo wanaouchunguza upi ni usasa wenye kufaa na upi haufai. Kundi hili hutumia fursa ya *Super Ego* katika nadharia ya Saikochanganuzi. Hivyo, Nana anakataa masharti anayopewa na Meneja kwa sababu, anaona ni usasa usio na maana.

Tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi tunabaini kwamba, wimbi la mabadiliko yanayosukumwa na utandawazi limekuwa kubwa miongoni mwa vijana kama dondoo hilo linavyobainisha. Hatari iliyopo ni kwamba, vijana hufuata mila na desturi za Kimagharibi bila ya kutathmini athari zake. Mavazi na mitindo ya maisha yao yameathiriwa na mila na desturi za Magharibi. Tukichukulia mfano wa mavazi ya vijana hawa, tunaona kuwa, yamejikengeusha na mavazi yale ya jadi yaliyomo katika jamii za Afrika.

### 4.6.3 Ukombozi wa Mwanamke

Harakati za ukombozi wa mwanamke ni miongoni mwa mambo yanayosababisha kutokea kwa ukengeushi miongoni mwa vijana. Baadhi ya wanawake hujikuta wakijikengeusha na jamii kutokana na kutaka uhuru. Halii hii ndiyo tunayoishuhudia katika *Dunia Yao* ambapo Yungi anawaona wazazi wake kwamba, wamepitwa na wakati kutokana na kung`ang`ania kumuweka katika utawa. Madai ya Yungi ni kwamba, wazazi wake wabadilike na wawe kama wazazi wengine ambao wamekubali kubadilika kutokana na kuwaruhusu watoto wao kuwa huru. Msanii anasema:

> Fungua macho… aliniambia kwa ukali, “majirani wote wanawaachia watoto wao wa kike na kiume wafanye wanavyopenda siku hizi. Wewe bado unang`ang`ania ukale. Wewe bado unataka kukamata na kudhibiti. Unataka uongozi usiouweza. Huwezi tena kutuendesha! (uk. 25).

Hali hii inayoelezwa katika dondoo hili, ndiyo tunayoishuhudia katika jamii za Afrika leo hii. Suala la uhuru wa mwanamke limeibua mjadala mkubwa miongoni mwa wanajamii, na hata wasomi wa nagazi mbalimbali. Wapo wanaoamini kwamba, wakati umefika wa kumruhusu mwanamke kuwa huru kufanya apendalo. Kwa mfano, Kezilahabi (1974), katika Diwani ya *Kichomi* kwenye shairi la *BikraMwenye Huzuni* anashadidia umuhimu wa mwanamke kuwa huru, hata katika masuala ya mapenzi na ndoa bila ya kuzuiwa na vikwazo vya dini na utamaduni. Fikra hizi ni za kimapinduzi, ambazo zinanuia kumtoa mwanamke katika nafasi zinazoonekana kama ni kandamizi na kumpeleka katika nafasi za uhuru binafsi. Ndio maana, Yungi anaamua hata kutumia ulevi kama ni kiburudisho wakati akitoka nyumbani na kwenda vilabu vya usiku. Msanii anatueleza hili kwa kusema:

> Yungi wa usiku ule, akishushwa garini kwa zogo la mchanganyiko wa sauti gonda na nyembamba, alibanduka na kusimama kwenye albamu. Baadaye nikamuona akiingia ndani kuja kunitia komango za masikio, utata wa ulimi na upofu wa macho. Yapata saa tisa na nusu ya alfajiri aliporudi, jimbi la kwanza lilipolia. Aligonga mlango huku akikiendeleza kicheko alichokujanacho. Lile kundi lake la suhuba lilikuwa limeshatoweka na gari.Mamake ndiye aliyemfungulia mlango baada ya kugonga, Akaingia ndani na uchangamfu na kicheko cha kilevi. Mtumbukio wake na mkondoupepo mpya aliokuja nao kwa nguvu za ajabu, ilikuwa ishara kamili ya utetio! Ishara ya kubadilisha kila kitu cha ukoo huu (uk. 24).

Mawazo haya yanapingana na nafasi za mwanamke ambazo ni za jadi katika maeneo ya Uswahilini. Kama yanavyoelezwa na Balisidya (1982:2), kwamba, nafasi za kijadi za mwanamke wa Tanzania kama zinavyojidhihirisha katika fasihi simulizi kwa kuzitaja kwamba; Mosi, mwanamke ni mama ambaye amekuwa mzazi wa watoto na mwenyekutunza familia. Pili, mwanamke amekuwa na nafasi ya kuwa ni chombo cha starehe. Tatu, mwanamke ananafasi ya kuwa kama bidhaa. Nne, mwanamke amekuwa akimilikiwa na mwanamme.

Misingi hii ya nafasi ya mwanamke ambayo inaelezwa na Balisidya (khj), ndiyo ianayomsukuma mhusika Yungi kujikengeusha kutokana na kuikataa. Binafsi anajiona hayuko huru kutokana na kumilikiwa na wazazi wake. Kwa hali hiyo, anapata mawazo kwamba, hayo ni mawazo ya kijadi ambayo kamwe hayawezi kuwa na nafasi katika wakati tulionao leo hii.

Hili ni suala la kitabaka, jamii imejikuta ikiangukia katika matabaka. Historia ya binadamu ni historia ya mapambano ya kitabaka. Kwa Karl Marx, matabaka ni sehemu ya mfumo wa uchumi na siasa. Hujitokeza pale ambapo kundi moja humiliki njia za uchumi za ziada inayozalishwa, na jingine likimili nguvu yake tu (Chuachua,2011:18). Anaendelea kusema kuwa, mfumo huu unaweza kubadilika kutokana na mabadiliko katika mahusiano ya kiuzalishaji mali, kwa kuwa ndiyo yanayoamua namna watawala wanavyojiimarisha kuwanyonya watawaliwa.

Hivyo, kutokana na mgawanyiko huu wa kimatabaka, hujikuta baadhi ya watu kuwa huru na wengine kukabiliwa na vikwazo ambavyo huwafanya wasiwe huru. Moja kati ya tabaka linalojikuta halikohuru katika jamii ni tabaka la jinsia ya kike. Tabaka hili limekuwa likikandamizwa na kuonewa. Kutokana na hali hii ya kihistoria, baadhi ya wanawake wanajitokeza wakiendesha harakati za kutaka uhuru wao binafsi.

Aidha, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, mhusika Nana anaamua kuhama kuishi na baba yake ili kutafuta uhuru wake binafisi. Anaamini kwamba, wakati umefika wa kila mtu kuwa huru. Pia, anamkataa mchumba anaechaguliwa na baba yake. Haya yote yanasukumwa na utashi alionao Nana. Msanii anatueleza hili kwa kusema:

> Nana alianza kwa kupigana na nafsi yake na anaendelea kupigana nayo. Kisha akaamua kupigana na mazingira yake ya nyumbani mpaka yakamfikisha kuhama na kutengana na babake. Tena akapigana na kuishi katika mazingira mapya na watu wapya. Akapania kufanya anachokitaka kwa ajili ya kuendesha maisha yake. Ndani ya yote hayo, kama alichokiona Kezilahabi, mna ugumu na maumivu na furaha, mna ugumu wa kutema roho yake mtu na kuisafisha. Yaani maumivu kila siku yana upande wa pili (uk. 222).

Kutokana hali hii, ni dhahiri kwamba, yale tunayoyashuhudia leo hii katika mitaa yetu, katika vyombo vyahabari, katika mitandao ya intaneti inayohanikiza uhuru wa mwanamke, ni harakati zinazofanywa na mwanamke ili kupata uhuru wake. Hata hivyo, ni vyema wanawake hao kuwa makini wakati wa kudai uhuru huo kwani, wasijejikutia wakitumbukia kwenye shimo la maangamizi.

### 4.6.4 Changamoto za kisiasa

Wanasiasa wanao mchango mkubwa katika kuikomboa au kuibomoa jamii. Kwa mujibu wa Chuachua (2011:20), ili mtu aitwe mwanasiasa, sio lazima apande jukwaani, bali anaweza kuitumia kalamu yake kuwafanya wananchi wayaone maovu na kuwatia hamasa wafanye mapinduzi. Suala la msimamo wa kisiasa, ni moja kati ya mambo yanayowasukuma wahusika kujikengeusha na jamii katika riwaya teule. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, mhusika Mimi anaeleza kwamba, kamwe hajawahi kuvua nguo na kushangiria masuala ya uhuru. Anachoamini ni kwamba, katika jamii kuna unyanyasaji na ukandamizaji; pamoja na, ukosefu wa haki. Demokrasia imekuwa ikikanyagwa na utu wa mtu kukiukwa. Mwandishi anasema:

> Mimi kamwe sikupata kuvua nguo zangu kwa kwenda uchi kushangiria mageuzi yoyote kwani maisha yangu yote nimekuwa siamini tabia ya kibinadamu ya uwambangoma. Kila siku ziliposonga mbele nilijikutia nachukia mambo mengi na hasa hali hii ya kukimbilia kurudi nyuma.Siku hizi bila ya shaka nakimwa na mambo mengi. Kwa kweli nina ugonjwa unaoitwa udodosi unaonienda ndani kwa ndani. Kila siku huzidi kunitia wazimu, hasa ukichanganyika na mambo mengine! Kila siku hunichochea

> kuiuliza nafsi yangu masuala milioni moja bila ya kupata jibu hata moja. Hivi sasa mathalani, najiuliza masuala kemkem. Kwa nini, kwa mfano, mtu asiweze kukataa jambo asilolitaka? Kwa nini mtu asiwe na maoni huru juu ya mwendo wa maisha yake na maisha ya waliokaribu naye? Kwa nini mtu mwingine awe na haki ya kuharibu maisha yangu na ya ukoo wangu? Kwa nini mimi niwe kila siku mtu mwenye hatia? Kwa nini mimi tu ndiye niwe mwendawazimu? Nifikapo ukomo huu wa kudadisi huwa sina jibu ingawa ninalo. Kwani nilitambua kwamba jibu la mwenyewe kwa mwenyewe lisingesaidia kitu… (uk.16-17)

Mhusika Mimi kama anavyoeleza katika dondoo hili, anadodosa masuala ambayo kimsingi yanakinzana na hali za kisiasa katika Bara la Afrika. Ambapo, hali hii imekwenda kinyume na matarajio ya wale waliochini. Wengi wa watu wamekuwa hawana haki ya kusema, huonewa, hawahusishwi katika kufanya maamuzi, na wamekuwa wakionekana si lolote wala chochote na wale wachache ambao wamekalia nyadhifa za uongozi. Matokeo yake, ni kutokea kwa machafuko kati ya tabaka tawala ta tabaka la walalahoi. Kutokana na tabaka tawaliwa kukata tama dhidi ya baadhi ya viongozi walioshika hatamu za uongozi.

Vilevile, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* tunaona namna Bwana Hila alivyo na ubinafsi na ufisadi kwa baadhi ya wanajamii, bila kujali maendeleo ya taifa. Jambo hilo linaendelezwa hata hivi sasa na limekuwa suala lenye kutamalaki katika nyoyo za watu. Kwa kurejelea riwaya hii, tunaona wale ambao wamemithilishwa na jamii ya binadamu halisi walivyojaa ubinafsi na ufisadi. Kwa kawaida,matendo haya huenda pamoja. Mathalani, Bwana Hila (babake Nana), amejaa ubinafsi pamoja na ufisadi uliokithiri dhidi ya wanyonge kutokana na kuyatumia vibaya madaraka yake na kuwanyanyasa wakulima ambao ni maskini. Mwandishinasemaa:

> Bado mpaka leo wakulima wananung'unika, na hawatasita milele ingawa hawajui wamlalamikie nani. Vipi Yule mfua vyoo jana leo awe tajiri mkubwa kiasi hiki? Wao walikuwa wapi alipojitutumua? Hakusomba mali tu, bali kaiba heshima ya wakulima baada ya kuwanyang'anya ardhi na uhuru wao. Na uhuru ni nini kama si kipato?

> Ghafla amepata nguvu zilizomsimamisha kumsuta kila mtu. Nguvu ambazo watu huziona kila siku zikiharibu, lakini hawawezi kuzizuia. Wanabaki kujiuliza kinatokea nini katika maisha yao? Laana ya Mungu au mapuuza ya binadamu mwenyewe? Ya wapi waliyoelezwa kuhusu usawa? Ya wapi yale waliyoahidiwa? Uhuru na kazi. Uhuru na haki. Uhuru na maendeleo. Uhuru na nini sijui…Yako wapi matunda waliyoambiwa watagaiwa akishaondoka Mzungu na Mwarabu? (uk.37).

Dondoo hili linatuonesha dhahiri kwamaba, kabla ya uhuru watu walikuwa kitu kimoja na kuweza kuhangaikia uhuru wao kwa pamoja. Lakini, mambo yalionekana kubadilika mara tu baada ya uhuru kupatikana. Wakulima walianza kunyanyaswa na viongozi wao mara tu baada ya mkoloni wa kizungu na wa kiarabu kuondoka. Walitarajia mabadiliko yenye neema, lakini, ikawa ikawa kinyume chake. Matokeo yake ikawa ni afadhali ya jana kuliko ya leo. Hili si jambo la ajabu kwa nchi za Kiafrika, kwani viongozi wengi wanaonekana kujilimbikizia mali mara tu baada ya kutawala, na kuwaacha wananchi wakihangaika kwa shida za ugumu wa maisha.

**4.6.5 Utamaduni wa kigeni**

Ann (2013) anasema kwamba, utamaduni wa kigeni umepenya na kuathiri pakubwa utamaduni wa jamii ya Mwafrika. Utamaduni huu mpya umeathiri masuala mbalimbali ya jamii kama vile; muziki, ndoa, mavazi, ngono, ujipodozi na uhusiano wa wazazi na watoto wao. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* nyimbo za muziki wa taarabu katika jamii ya Nana zilionekana za thamani ndogo, na hivyo kupuuzwa. Nafasi hiyo ilichukuliwa na muziki wa *hip hop* ama wa *rap* na wenye arki za kimarekani, ndio ambao ulithaminiwa(uk. 140).

Aidha, Nana kama tulivyokwishaona, ni mkereketwa wa usasa na mwimbaji aliyetakiwa kuimba kwa mtindo wakisasa, ambao nyimbo zake ni zenye mwelekeo wa mipasho ya matusi, misubukuo, tashtiti na kung’ong’ana vichwa. Hili linaonekana pale, wakati Nana anapokwenda kwa Meneja ili kufanyiwa usaili iwapo

anafaa kuwa muimbaji au la. Hata hivyo, Nana anakataa vikali masharti hayo. Msanii anatusimulia kuwa, Nana anasema hivi:

> …Sikutaka kulazimishwa nyimbo za kuimba- nyimbo za matusi na masimango, nyimbo za mipasho na rusha roho. Nilizizarau mno nyimbo hizo zisizo mwala wala murua. Zisizofikia viwango na upeo mkubwa wa kisanaa. Pia, sikutaka kulazimishwa kuvaa nguo wanazotaka watu wengine, fupi au ndefu. Nilitaka nivae nguo ninazopenda kuvaa mimi mwenyewe. Basi hatimae nikapasukwa na kicheko cha kejeli tu. Nilicheka tu. Kisha nikamwambia meneja 'asante' sikuwa tayari kuifanya kazi hiyo (uk. 144-145).

Usasa uliolikumba bara la Afrika, kama unavyoelezwa katika dondoo hilo hapo juu, umewagawa wanajamii. Wapo wanaouchukulia kuwa, ni mzuri moja kwa moja, hawa huthubutu kudharau utamaduni wao huku wakisukumwa na utashi wa *Id*katika nadharia ya Saikochanganuzi, na wapo wanaouchunguza upi ni usasa wenye kufaa na upi haufai. Hawa hulinganisha kati ya utamaduni na usasa. Kundi hili hutumia fursa ya *Super Ego* katika nadharia ya Saikochanganuzi. Hivyo, Nana anakataa masharti anayopewa na Meneja, kwa sababu anaona ni usasa usio na maana.

Pia**,** Ann (2013), anasema, katika usasa tuliomo wanajamii, hasa wanawake wamejipata wenye dukuduku kutokana na hali za ndoa zilizokosa kuafikiana. Suala hili hushinikiza sana ubongo juu ya fikra nyingi. Hivyo, kuokoa jahazi na wengi huhudhuria vikao vya ushauri nasaha ili kuauniwa. Jambo hili limedhihirika vyema katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, wakati Nana alianzisha kipindi cha dukuduku ambapo wanawake hueleza masaibu yao ya ndoa. Katika jumba la *Karibu Mwanamke*, kuna ghorofa ya sita ambayo ilitengwa kama kitengo cha kushughulikia matatizo ya wanawake. Msanii anatueleza hili kwa kusema:

> "Hapo ndipo panapoendeshwa shughuli zote za kumsaidia mwanamke yeyote aliyekabiliwa na matatizo ya unyumba, ya kubaguliwa,ya kubakwa, ya magonjwa ya akili kwa kukadamizwa, ya magonjwa ya ngono...Ni ofisi

> yenye mabingwa na washauri wa mambo na matatizo mbalimbali ya wanawake" (uk. 198).

Kwa ujumla,masuala ya mahusiano ya kijamii leo hii yamechafuka. Matokeo yake ni kutokea kwa mifarakano ya mtu na mtu, kundi na kundi, na hata mtu binafsi. Hali hii inasababisha msongamano wa mawazo miongoni mwa wanajamii. Mathalani, wapo wanaonyanyasika katika ndoa, wapo wanaobakwa nakadhalika. Hivyo, makundi kama haya yanahitaji kusaidiwa kwa ushauri nasaha.

Aidha, Ukengeushi huu unaotokana na utamaduni, pia, tunauona katika riwaya ya *Dunia Yao*. Mhusika Mimi anajikengeusha kwa kukataa kula nyumbani kwake na kujitenga na familia yake. Mhusika huyu anasukumwa na nguvu za kiutamaduni ambapo, anaona matendo ya umalaya anayoyafanya Yungi. Hali hii inatokana na mila na desturi za jamii yake kutokubaliana na vitendo vya uasharati. Mhusika Mimi anaona ni aibu kubwa mbele ya jamii yake, kuwa na mtoto mzinzi na mlevi. Ili kuonesha kutoridhishwa na hali hiyo, anaamua kujitenga na familia nzima (uk.2).

### 4.6.6 Habari na Mawasiliano

Owino, Simala na Choge (2013:14) wanasema kwamba, dhana ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa upana hurejelea aina za teknolojia zinazotumiwa kuvumbua, kuhifadhi, kutengeneza, na kutumia habari katika maumbo mbalimbali. TEHAMA hutumiwa kwa lengo la utendaji kazi; kuimarisha utendaji kazi, kuimarisha ufundishaji, uwazi na kuongeza ufanisi. TEHAMA imetambuliwa na wataalamu wa elimu kuwa ni muhimu katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.

Mhusika Mimi anatumia mbinu ya matumizi ya kompyuta katika kuendeleza masimulizi ya visa mbalimbali katika riwaya ya *Dunia Yao*. Mhusika huyu amekuwa akitumia kompuyta kama kifaa ambacho, kimekuwa kikimrahisishia kueleza yale yaliyomo moyoni. Msanii anasema:

> Kompyuta iwazi.La! Sizungumzi na wewe baba. Huwezi kunifahamu. Wala wewe kukufahamu tena. Upepo umeshachukua mbali. Nami pia umenikimbizia kwengine. Labda mkutano wetu utakuwa mmoja kwenye ufu. Unapojibu baruapepe, sauti yako inazidi kuwa dhaifu. Siisikii. Haina nguvu tena sauti yako. Heshima yako imegubikika… (uk. 116)

Katika riwaya hii ya *Dunia Yao*, mhusika Mimi anaonekana akijikengeusha kwa kutumia mawasiliano ya mtanadao wa kielektoniki. Mawasiliano haya tunayaona yanafanywa kati ya mhusika Mimi na mtoto wake aliyeko nje ya nchi.

Aidha, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke,* suala la habari na mawasiliano linatumiwa na Nana, ambaye amefungua kituo cha redio ambacho kimekuwa kikitumika kutoa madukuku. Kituo hicho kinatoa fursa kwa wanawake kueleza yale ambayo yamewasibu (uk.198).

### 4.6.7Matukio ya Usomi

Mhusika Mimi katika *Dunia Yao,* anaonekana kuwa ni msomi ambaye amebobea katika taaluma ya fasihi na nadharia za uchambuzi wa kazi za fasihi. Hivyo basi, katika riwaya ya *Dunia Yao*, mhusika Mimi anaamua kutumia nadharia ya wigo ambayo inahusu dhana ya chimbuko la fasihi ulimwenguni. Nadharia hii kama anavyoileza Mulokozi (1996), na Mwamzandi (2013:50-53), kwamba, inaona chimbuko la fasihi ni Mungu. Hali hii inamuathiri mhusika Mimi na kuamini kwamba, vile anavyoandika fasihi ni kutokana na nguvu za Mungu. Tunaliona hili wakati mhusika Mimi anapofanya majadiliano ya ana kwa ana na mhusika Muse. Katika kulisawiri hili, mwandishi anasema:

> Mimi ni Muse […] "Kwa asili hasa, Ugiriki-lakini siku hizi naishi popote. Mara nyingine hujificha katika vina virefu vya ardhi kabla sijachomoza kumdhuru niliyemchagua. Na leo nimekuchagua wewe. Kwa hivyo, nimechomozekea chini ya mnazi palipofukiwa kitovu chako baada ya kupiga mbizi Bahari ya Hindi kuja kukuingia kichwani mwako…(uk. 61).

Huu ni mtindo wa kipekee ambao unaonesha ukengeushi kati ya mhusika Mimi na mhusika Muse. Mhusika Muse, kwa vile anahusishwa na sifa ya Mungu wa Wayunani, si hali ya kawaida katika maisha ya kila siku Mungu kukaa pamoja na binadamu na kujadiliana. Kinachojidhihirisha hapa, ni mjadala wa msanii juu ya nadharia ya chimbuko la fasihi. Kupitia ukengeushi huu tunaona kwamba, riwaya hii ina sifa za riwaya za kisasa, kama asemavyo Madumulla (2009), kwamba, riwaya hizi za kimajaribio pamoja na mambomengine, huwa zimejaa wingi wa nadharia. Vilevile, kutokana na hali hii ya ukengeushi wa mhusika Mimi katika riwaya ya *Dunia Yao,* Mwamzandi (2013:5), anasema, ndiyo sababu *Dunia Yao* inafafanua uhusiano wa Ndi- na Bi Muse kuwa mke na mume, wanaoliwazana na kubembelezana hadi wanapooana na kuwekana nyumbani,hii inauchora uhusiano kati ya mhusika Mimi. Ni taswiira ya unganiko la kufukuza utasa na baadae kuzalisha kazi za kisanaa baada ya wahusika hawa kusuhubiana na hata kupata mtoto, yaani, kazi inayotungwa. Hali hii ianaelezwa na Ndi- kama msanii anavyosema:

> Ndiyo, jina lake nimekuwa nikilisikia na kulisoma siku nyingi. Kama alivyosema mwenyewe si kiumbe wa sasambure turore. Hujifichuwa anapohitajiwa kwa mapenzi ya dhati au kutoa msaada. Na mimi nimefika balekhe ya kusalitika naye. Nina haja naye. Ninamhitaji. Ninataka anisaidiye. Anisaidie kuwasaidia wengine ikiwezekana. Anisaidie kuukata ugumba wa utunzi. Ninahamu kurutubisha na kutia mbolea pahala fulani. Nipate kizazi kipya cha sanaa katika ukame wa ubunifu. Nipate kurutubisha kizazi kipya cha utu katika ukame usio na utu. Ninahitaji mtekenyo wake unipandishe jazba (uk:61).

Kama maelezo ya dondoo la hapo juu yanavyojidhihirisha, ni wazi kwamba,*Dunia Yao* ni miongoni mwa riwaya za kimajaribio ambazo zimekuja kuipa sura mpya riwaya ya Kiswahili. Ni miongoni mwa riwaya ambayo imeonesha majaribio makubwa katika historia ya Riwaya ya Kiswahili kutokana na ukengeushi wa kuzichambua nadharia.

Pamoja na hali hiyo, tunaporejelea nadharia ya Saikochanganuzi, tunaona kwamba, uhusiano wa mhusika Mimi na Muse pamoja na kujadiliwa kama nadharia ya uchambuzi wa fasihi, kwa upande mwingine, mhusika Bi. Muse ametumika ili kuibua matendo yasiyo na utu katika jamii.

Kwa upande wa Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, tunaona matukio kadhaa yanyotendwa na wahusika kutokana na sababu za kiusomi. Kutokana namendeleo ya taaluma ya usomi, Nana anaanzisha ofisi ya ushauri nasaha, ambayo imekuwa ikiwasaidia wanawake ambao wamekumbwa na matatizo kadhaa. Kwa mfano, msaniianatunasimulia hivi:

> Hapo ndipo panapoendeshwa shughuli zote za kumsaidia mwanamke yeyote aliyekabiliwa na matatizo ya unyumba, ya kubaguliwa,ya kubakwa, ya magonjwa ya akili kwa kukadamizwa, ya magonjwa ya ngono...Ni ofisi yenye mabingwa na washauri wa mambomatatizo mbalimbali ya wanawake (uk. 198).

Pia, kutokana na taaluma aliyonayo Nana, anajitambua na kujua utu wake na haiba yake. Anaakataa kupangiwa mavazi, na nyimbo za kuimba,hii inatokana na kutambua kwamba, hilo ni suala la hiari ya mtu binafsi (uk.144-145). Pia, Nana anaamua kuanzisha mradi ambao una tija ndani yake, anaamua kuanzisha miradi kama vile; taarab ambayo inamfanya ajiajiri na kuwaaajiri watu wengine (uk. 166-167).

## 4.7 Hitimisho

Shabaha kubwa ya kuwapo kwa sehemu hii, ni kutokana na mwendelezo mzima wa kumtafiti mwandishi teule wa utafiti huu, ili kukamilisha lengo mahusi la tatu la utafiti wetu. Ambapo, lengo mahusi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini sababu za wahusika wa kimimi kujikengeusha na jamii iliyochorwa na mwandishi katika riwaya teule, ambazo si nyingine, bali ni *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Tulichobaini ni kwamba, mwandishi alitumia sababu za msingi za wahusika hao wa kimimi kutaka kujikengeusha katika jamii. Ukengeushi wa wahusika hao, ulikuja pale ambapo, waliona jamii yao bado inang'ang'ania kuishi katika misingi ya maisha iliyopitwa na wakati.

Hatahivyo, mwandishi aliwatumia baadhi ya wahusika wake kama vile; Bori, Yungi na wengineo, wakionekana kutokuwa na ajira yoyote, ijapokuwa walikuwa wamemaliza masomo yao. Aidha,sehemu hii inaonesha sababu nyingine za wahusika kujikengeusha na jamii kupitia riwaya teule zinazoongoza utafiti huu. Sababu ziko nyingi, lakini baadhi yake ni kama vile; ukosefu wa ajira, athari za utandawazi, ukombozi wa Mwanamke, changamoto za siasa, habari na mawasiliano, pamoja na matukio ya usomi.

## 4.8 Muhtasari wa Sura ya Nne

Katika sura hii tumeelezea namna wahusika wa kimimi walivyosawiriwa na mwandishi Said Ahmed Mohamed katika riwaya zake za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Hivvyo, miktadha ambayo wahusika wa kimimi wamesawiriwa na mwandishi imebainishwa. Kadhalika, katika sura hii mtafiti amejaribu kufafanua upekee wa wahusika wa kimimi katika kujikengeusha na jamii iliyosawiriwa na mwandishi.

Vile vile, sura hii imejikita katika kutathmini sababu mbalimbali za wahusika wa kimimi kujikengeusha na jamii iliyosawiriwa na mwandishi. Shabaha kubwa ya mtafiti kuvitupia jicho vipengele hivyo ni kuionesha jamii ya wasomi namna mwandishi nguli wa riwaya, yaani Said Ahmrd Mohamed alivyotumia ulumbi mkubwa wa lugha adhimu ya Kiswahili katika kuwasawiri wahusika wa kimimi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Mchakato mzima wa utafiti huu ulilenga kuyafikia malengo mahsusi matatu. Lengo mahususi la kwanza lilikuwa, ni kubainisha miktadha ambayo wahusika wa Kmimi wamechorwa katika riwaya teuele za Said Ahmed Mohammed.Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa, riwaya teule zimewasawiri wahusika wa Kmimi katika miktadha mbalimbali, ambapo, katikautafiti huutumegundua kuwa, riwaya ya *Dunia Yao*na *Nyuso za Mwanamke* zimewasawiri wahusika wa Kimimi katika miktadha kama vile; miktadha ya chimbuko fasihi, miktadha ya changamoto za kisiasa, miktadha ya shereheni, miktadha ya kazini, miktadha ya kifamilia, miktadha ya mahakamani na miktadha ya mitaani.

Kwa upande wa Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, msanii amewasawiri wahusika wa Kimimi katika miktadha hiyo, kwa lengo la kuonesha ukengeushi huo wa wahusika. Mathalani, msanii amemtumia mhusika Faisal, ambaye anafanya sherehe za mara kwa mara nyumbani kwake. Hali hii inaonesha namna watu wengi leo hii wanavyotumia pesa ovyokutokana na sherehe za mara kwa mara, ambazo matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa pesa.

Vilevile, mtafiti amebaini kuwa, kumekuwa na upekee wa wahusika hao katika kujikengeusha na jamii.Aidha, utafiti uligundua kuwa, kuna mwangi wa upekee miongoni mwa wahusika katika kujikengeusha na jamii. Kadhalika, katika riwaya teule, wahusika hao wamejikengeusha kwa namna ya pekee, kama vile; kugomea chakula, kuonesha kutojali, matumizi ya mhusika kivuli, kutokata tama, mijadala ya

nadharia kuhusu imani, kushiriki ngono, kupenda usasa,kutumia ulevi na uongozi mbaya.

Kwa upande wa *Dunia Yao*, mhusika Mimi anaamua kugoma kula nyumbani kwake, kwa kuamini kwamba, chakula kinachopikwa katika nyumba hiyo kinaletwa na Yungi. Hivyo basi, hataki kula chakula cha ukahaba. Pia, kutokana na hali hiyo, anaamua kukaa na kutozungumza na mtu yeyote nyumbani kwake. Vilevile, mhusika huyu anajikengeusha na jamii kwa kudai kuwa, haoni umuhimu wowote wa uhuru,kwa kusema kuwa, hakuna uhuru wa mtu binafsi na haki huwa haitendeki. Mgomo kama huu, unaendelezwa na Mhusika Nana katika *Nyuso za Mwanamke* pale anapogomea chakula, pamoja na kupelekwa na kurudishwa shuleni kwa gari, jambo ambalo linamkwaza kwa kiasi fulani.

Pia, Bori anaamua kujikengeusha kwa kuokota vitu kwenye madampo. Hii inatokana na kushindwa kufaulu mtihani wa kidato cha pili. Hivyo, anajiingiza katika biashara hii ya kukushanya makachara, ili kujinasua na maisha magumu yaliyomkabili. Hata hivyo, binafsi yake anaamini kwamba, iko siku atajikomboa na hali hiyo ya maisha magumu.

Vilevile,Bi. Miza ambaye ni mhusika wa kinadharia anayehusishwa na Mungu wa Wayunani amejikengeusha. Ukengeushi huounatokana na vile Mungu huyo kukaa pamoja, ana kwa ana na mhusika Mimi, ili kumpa msukumo wa utunzi wa kazi yake. Aidha, kuna ukengeushi wa mhusika Nana ambapo, anajikengeusha kifikra, kimawazo na kuwa na mwono wa ulimwengu mpya. Hakubaliani na mambo mengi katika jamii yake. Tangu mwanzo aliamua kuishi na kutembea na wakati. Yeye aliamini hali ya kuwa na ndoto mpya na fikra mpya za kumjenga mtu kutoka hali moja hadi nyingine.

Aliamini kwamba, binadamu asipotumia fikra zake, atakuwa mtumwa wa jamii. Nana alijiamini, Nana alikataa utamaduni unaomrudisha nyuma. Ailsoma na kujitambua. Pia, Nana anakuwa kiongozi. Mwisho, anajenga jumba kubwa la kibiashara na kuendeleza shghuli mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha. Aidha, Nana anafanya mazoezi ya viungo jambo ambalo ni geni kwa jamii za Uswahilini.

Kutokata tama kwa wahusika ni jambo jingine ambalo tuliligundua katika utafiti huu, ambapo, mwandishi amemtumia mhusika Nana kama mtu asiyekata tamaa hususani, wakati wa kudai haki zake. Hii ilikuwa ni kwa upande wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Aidha, katika riwaya ya*Dunia Yao*, mhusika Bori anaonekana kujipa matumaini ya kwamba, iko siku atashinda.

Jambo jingine ambalo ni la ukengeushi katika riwaya teule, ni suala zima la uongozi. Tunaona wahusika wamekuwa wakiwaongoza wananchi wao katika hali isiyo yakuwajali. Mathalani, mhusika Mimi katika *DuniaYao* na Faisal katika *Nyuso za Mwanamke*, hawa wanapigiwa mfano katika kuendeleza uongozi mbaya.

Pia, utafiti ulibaini kuwa, Said Ahmed alikuwa na sababu za msingi zilizosababishawahusika kujikengeusha katika jamii. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba, wahusika katika riwaya teule wamejikengeusha na jamii kwa sababu anuai, ambapo miongoni mwazo ni kama zifuatazo:

Wahusika wamejikengeusha kutokana na sababu za utamaduni. Utamaduni mkongwe umekuwa ukipingwa na baadhi ya vijana wa kizazi kipya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Yao*, mhusika Yungi anapinga mikatale ya wazazi wake kwa kutompa uhuru, hivyo, anaamua kuikiuka. Pia, Mhusika Nana katika *Nyuso za*

*Mwanamke*, anapingana na utamaduni wa jadi wa kuchaguliwa mchumba na wazazi wake.

Vile vile, katika *Dunia Yao* tumeona kuwa, sababu nyingine inayowasukuma wahusika kujikengeusha ni kutokana na ukosefu wa ajira. Vijana wengi baada ya kumaliza masomo yao hawajui la kufanya. Hivyo, hujikuta wakiwa wazururaji, kama vile, Bori na wengineo kujiingiza katika biashara haramu, ikiwamo ile ya ngono kama anavyofanya Yungi.

Pia, katika Riwaya ya *Dunia Yao* na riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* tunaona kuwa, wahusika wamekuwa wakijikengeusha kutokana na sababu za kupata elimu. Mhusika Mimi katika *Dunia Yao* ni msomi wa kiwango cha juu cha elimu. Hivyo, yale yanayotendeka katika jamii, hasa yanayofanywa na viongozi pamoja na wakoloni hakubaliani nayo. Pia, anamtumia mhusika Muse, kwa sababu ya kutambua nadharia mbalimbali za chimbuko la fasihi. Vilevile, katika *Nyuso zaMwanamke*,Nana anajikengeusha kutokana na kupata elimu, na kuamua kuanzisha miradi mbalimbali. Kutokana na hali hii, anakataa utamaduni wa jadi wa kumfanya mwanamke amtegemee mwanamme tu.

Kama tulivyokwishaeleza kuwa, Utafiti huu ulifanyika kwa lengo la kuchunguza wahusika wanaobeba dhana ya Umimi, kama inavyojitokeza katika riwaya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* za Said Ahmed Mohammed. Kwa kufanya hivyo,tuliweza kubainisha miktadha ya wahusika wa Kimimi, kufafanua upekee wa wahusika wa kimimi na kutathmini sababu za wahusika kujikengeusha katika jamii. Utafiti huu uliongozwa na mkabala wa Saikochanganuzi.

Aidha, utafiti huu umebaini kuwa, riwaya teule zimekuwa zikitumia miktadha kama vile ya chimbuko la fasihi, miktadha ya changamoto za kisiasa, miktadha ya shereheni, miktadha ya kazini, miktadha ya kifamilia, miktadha ya mahakamani na miktadha ya mitaani,katika kuwasawiri wahusika wa kimimi. Wahusika hawa ni wahusika wanaobainisha ubinafsi wao na vile wanavyopendelea, ama wanavyochukia. Hivyo,  tumebaini kwamba, kuna mambo wanayapendelea na kuna mambo wanayachukia kupitia miktadha hiyo.

Pia, utafiti umebaini kuwa, wahusika katika riwaya teule wamekuwa wakijikengeusha na jamii katika vipengele mbalimbali. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* mhusika Bori anajikengeusha na jamii kwa kuokota vitu majalalani na kuvipeleka nyumbani kwao. Pia, mhusika Yungi anajikengeusha kwa kufanya ngono holela na kulewa. Vilevile, mhusika huyu anajikngeusha kwa kutaka uhuru wake huku akiwaeleza wazazi wake waziwazi kuwa, wamekuwa wakikosea kumzuia kutoka na kwenda vilabu vya usiku. Mhusika Mimi anajikengeusha kutokana na kugoma kula chakula nyumbani kwake kutokana na tabia mabaya ya Yungi. Vile vile, anajikengeusha kutokana na kueleza hisia zake chanya dhidi ya uhuru ambao umejaa ukandamizaji, ubinafsi na ukosefu wa demokrasia.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanmke,* tunaona namna mhusika Nana anavyojikengeusha na jamii kutokana na kupinga tamaduni za jadi, ambazo zimekuwa zikimkandamiza. Mhusika Nana anaamua kupinga kuchaguliwa mchumba na wazazi wake. Pia, anajenga jumba kubwa la kibiasahara pamoja na kushiriki katika mazoezi ya viungo.Mhusika Ngware, anajikengeusha na jamii kutokana na kujiingiza katika kutumia mihadarati, hivyo, ili kupata pesa lazima aibe

kwa kutumia nguvu. Aidha, bwana Hila anajikengeusha na jamii kutokana na kutojali, na kutumia pesa nyingi kwa sherehe nyumbani kwake.

Kwa ujumla tumebaini kwamba, riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na *Dunia Yao,* wahusika wake wamejikengeusha kutokana na sababu za utamaduni wa kisasa, elimu, masuala ya kisiasa, harakati za ukombozi wa mwanamke, maendeleo ya sayansi na teknolojia, ukosefu wa ajira na sababu za utandawazi.

**5.2 Hitimisho**

Sura hii imegawika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni; sehemu ya kwanza, inahusu muhtasari wa utafiti huu, sehemu ya pili, inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu, inatoa mapendekezo ya utafiti huu kwa mujibu wa mtafiti. Aidha, katika utafiti huu, tumeshughulikia suala la wahusika wa Kimimi katika riwaya mbili za Said Ahmed Mohamed ambazo ni *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Mchakato huu tumeuanza kwa kutoa maana ya baadhi ya istilahi muhimu, ambazo zinaenda sambamba na zinaelekea kuwa na mchango mkubwa katika kuiendea mada yetu. Aidha, tumejaribu kutoa ufafanuzi wa mhusika Mimi kwa mujibu wa mkabala wa Saikochanganuzi, kama ndio dira inayotuongoza kulingana na malengo yetu katika utafiti huu.

Lengo kuu la utafiti huu, lilikuwa ni kuchunguza wahusika wanaobeba dhana ya Umimi kama ianavyojitokeza katika riwaya teule.  Aidha, utafiti huu una malengo mahsusi matatu, ambayo ni; Kubainisha miktadha ambayo wahusika wa Kimimi wamesawiriwa katika riwaya teule za Said Ahmed Mohammed. Kufafanua upekee wa wahusika wa kimimi katika kujikengeusha na jamii, na kutathmini sababu za wahusika wa kimimi kujikengeusha katika jamii iliyochorwa na mwandishi.

Katika kuhakikisha tunayafikia malengo hayo, data za utafiti zilikusanywa kwa kupitia maandiko ya riwaya teule za Said Ahmed Mohamed, pamoja na maandiko mengine ya wataalamu mbalimbali kwa madhumuni ya kufikia malengo ya utafiti huu. Sampuli ya utafiti huu ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa, ambapo, sampuli lengwa iliundwa na riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*. Uteuzi wa mapitio ya maandiko tulioufanya, ulionesha pengo ambalo limezibwa na utafiti huu. Pia, tumebaini kuwa, watafiti mbalimbali walitafiti maandishi ya Said Ahmed, kwa kuangalia vipengele vya maudhui na wachache katika vipengele vya kifani. Wako waliodai kuwa, mwandishi huyu anajenga dhamira za ukombozi. Hata hivyo, tumebaini kuwa, hakuna kazi iliyoshughulikia suala la wahusika wa Kimimi katika riwaya za Said ahmed Mohamed, hususani, zile za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*, jambo ambalo tumeliakisi katika tasnifu hii kwa kutumia riwaya hizo.

Uchanganuzi wa data wa utafiti huu, tumeufanya kwa kutumia mbinu ya ufafanuzi katika riwaya mbili tulizozitumia tulizozitaja hapo juu. Uchanganuzi huo umezingatia malengo yetu yote matatu, kama ambavyo tumeyaorodhesha hapo juu. Tuna imani kwamba, matokeo ya utafiti huu yatakuwa na mchango mkubwa kwa wanataaluma wabobevu, na wsiowabobevu katika uga huu wa kifasihi na nyuga nyingine.

**5.3 Mapendekezo**

Utafiti huu umefanywa kwa kutumia riwaya mbili za *Dunia Yao na Nyuso za Mwanamke za Said Ahmed Mohammed,* ambazo zina sura ya riwaya za kisasa. Utafiti huu unapendekeza kuwa, tafiti zingine zinaweza kufanyika kwa waandishi wengine kwa kutumia kazi zao za fasihi. Tafiti kama hizo, zinaweza kutusaidia

kuelewa utunzi wa msanii na mbinu zake za utunzi ili kubaini upekee wake katika utunzi. Aidha, utafiti unaweza kufanyika kwa kuchunguza kazi za watunzi tofauti, lengo likiwa ni kufanya utafiti wa kina kuhusiana na mbinu ya matumizi ya mhusika Mimi katika utunzi wa tamthiliya na riwaya. Vilevile, tafiti nyingine zinaweza kufanyika kwa kina zaidi, ili kuchunguza vipengele vingine vya fani na maudhui katika riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke.*

## MAREJELEO


Adam, O. A. (2014). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii katika Riwaya za Kiswahili: Mifano kutoka Vutankuvute na Kuli*. (Tasnifu kwa ajili ya kukamilisha shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Ali, A. R. (2015*). Kuchunguza Dhana zilizobebwa na Wahusika na Zinavyolandana na Majina yao: Uchunguzi katika Riwaya ya Kiu na Kiu ya Haki.* (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ann, S. S. (2013). *Usasa na Mwanamke wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya Said AhmedMohamed*. (Tasnifu kwa ajili ya kukamilisha shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Kenya: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Balisidya, M. L. (1982). *The Image of the Woman in Tanzania Oral Literature: A Survey*. Katika Jarida la Uchunguzi wa Taasisi ya Kiswahili, Toleo Na. 49/2 uk.2-3.

Chuachua, R. (2010). *Suala la Itikadi katika Riwaya za ShaabanRobert* (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: TATAKI.

John, J. na Mdude, F. (2011). *Kiswahili Kidato cha Tano na Sita*. Dar es Salaam: Oxford University Press (T) Ltd.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.

Kezilahabi, E. (1983). Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi. Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. Na.3, Dar es Salaam: TUKI. Uk. 235.

Khamis, T. Y. (2014). *Wahusika wa Kimajazi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho waRiwaya za Said Ahmed Mohamed na Shaaban Robert.* (Tasnifu kwa ajili ya kukamilisha shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Krober, A. & kluckhon, C. (1952). *Kamusi Elezo Huru.* Iliyosomwa Agosti 9, 2017 katika sw.wikipedia.org/wiki/utamaduni.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Manzi, Z. M. (2007). Civics for Secondary School (2nd ed.). Dar es Salaam PBL Publishers.

Mapunjo, C. G. (2014). *Usawiri wa Mwanamke kama Kiongozi katika Tamthiliya: Uchunguziwa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama*. (Tasnifu kwa ajili ya kukamilisha shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbogo, E. (2002). *Watoto wa Mamantile*. Heko Publishers.

Mlacha, S. A. K. na Madumula, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, A. S. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Mohamed, A. S. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Mtobwa, B. R. (1998). *Dar es Salaam Usiku.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Muhando, P. na Balisidya, N. O. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M.M. (1996).*Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Ndugo, C. W. & Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two: Misingi ya Nadharia yaKiswahili*. Nairobi: Universty of Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R.M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: The Jomokenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomkenyatta Foundation.

Nkwera, F. (1978). *Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TPH.

Nyenye, (2011). *Taswira katika Nathari za Euphrase Kezilahabi*:*Nagona na Mzingile*. (Tasnifu ya kukamilisha mahitaji ya Uzamili, haijapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Said, A. S. (2015).*Matumizi ya ndoto katika riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa riwaya za Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed.* (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Salim, M. A. (2015). *Kuchunguza Ufasihi simulizi unaojitokeza ndani ya hadithi ya Kusadikika na Adili na Nduguze*. (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji yashahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Salum, S. S. (2013). *Wahusika na Usawiri wa Halihalisi ya Visiwa vya Zanzibar*. (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya shahada ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Sengo, T. S. Y. (1982). *Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja.* Katika *Nordric Journal of African Studies*.

Sengo, T. S. Y. M. (2014). *Falsafa ya Maisha*. Dar es Salaam: Hakijachapishwa.

Senkoro, F. E. M. K. (1977). *Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Umma*. (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya shahada ya Uzamili, haijachapisha). Chuo Kikuu Dar es Salaam.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi, Kenya: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (1999). *What'sin a name: Towards Literary Onomestic in Kiswahili Literature*. Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Kiswahili Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2013). *Mikakati ya Uhalisia katika Riwaya ya Kiswahili.* Mulika Na.33 uk.1-12. Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wanyonyi, M. C. (2011). *Uhakiki wa Riwaya ya Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: University of Nairobi.

Wikimedia Foundation, (2013). *Kamusi Elezo Huru*. Last edited on 11 March, 2013 at 04:48. Iliyosomwa Novemba 12, 2017 katika sw.wikipedia.org/wiki/nafsi.

## VIAMBATISHO

### A: Barua ya Ithibati ya kufanya Utafiti

### A1: Barua kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma

**THE UNIVERSITY OF DODOMA**

**DEPUTY VICE CHANCELLOR ACADEMIC, RESEARCH & CONSULTANCY**

**OFFICE OF GRADUATE STUDIES AND CONTINUING EDUCATION**

P.O. BOX 259, DODOMA, TANZANIA

Tel +255 26 23 10173 Fax +255 26 23 10005 Email [illegible] website [illegible]

REF: UDOM/GRF/13 VOL II/57

Tuesday, 21 November 2017

**To Whom It May Concern:**

**RE: INTRODUCING MR ALI, HAJI B.**

The above named candidate is enrolled at the University of Dodoma for the degree of Master of Arts in Kiswahili (MA KL) with registration number HD/UDOM/235/T.2016

As an essential requirement of the study programme, each candidate is required to submit a dissertation report on a research undertaken within an industry and supervised by a member of the University's academic staff. Where possible the research should relate to a practical situation in an organisation or firm selected by the candidate. Candidates are expected to use their own initiative to identify a possible research and negotiate access with a local firm or organization.

The above named candidate has developed the proposal titled **"WAHUSIKA WA KIMIMI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA DUNIA YAO NA NYUSO ZA MWANAMKE."** which has been approved for data collection. The work may take the form of a survey, ethnography, case studies, etc. Where the research may contain confidential information and its publication could be harmful to the organization, confidentiality is assured by the University. Such reports will be seen only by the Supervisor and Examiner for examination purposes.

I would be grateful if you would provide the candidate with this opportunity to facilitate his Studies while at the same time gaining some useful inputs for your own organization through the results of the research report.

Sincerely,

Waziri, A.

**For: Director, Graduate Studies and Continuing Education**

C.c: Director, GS&CE

**B: Maswali ya Mwongozo kwa Mtafiti**

**B1: Maswali yahusuyo Utafiti**

(i) Unaelewa nini kuhusu dhana ya Umimi?

(ii) Ni katika miktadha ipi ambayo wahusika wa kimimi wamesawiriwa katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke*?

(iii) Kwa maoni yako, unaelewa nini kuhusu dhana ya ukengeushi?

(iv) Kuna upekee gani wa wahusika wa kimimi kujitenga katika jamii?

(v) Unadhani ni kwa nini wahusika wa kimimi hujikengeusha katika jamii?

(vi) Kwa maoni yako unadhani kuna haja ya wahusika hao kujikengeusha?